

www.ccoq.org

UNABII WA HABARI ZA BIBLIA



MIEZI YA RANGI KAMA DAMU:
Je, Yesu Atarejea 2014?

Mardi Gras:
Ni Sherehe ya Ibilisi?

Yesu Alimaanisha Nini
“Nataka Rehema, Wala si Sadaka”?

UNABII WA HABARI ZA BIBLIA



3



8



15



27



32

NDANI YA TOLEO HILI:

- 3 Wakristo Wameifundisha Injili ya Ufalme!** Je, Wakristo wa karne ya kwanza na ya pili walikuwa wanaelewa na walihubiri juu ya Ufalme wa Mungu? Vipi kuhusu Wakristo wa karne ya 20 na ya 21?
- 8 Miezi ya Rangi kama Damu: Je, Yesu Atarejea 2014?** “Miezi ya Rangi kama Damu” inatarajiwa kutokea katika mwaka 2014. Je, hali hiyo yaweza kuwa inaashiria kwamba Yesu atarejea mwaka 2014?
- 15 Jisomee Kozi ya Biblia Somo la I: Kwa nini Tujifunze Biblia?** Hili ndilo somo la kwanza la Kozi ya kuwasaidia watu kuelewa Biblia.
- 27 Mardi Gras: Ni Sherehe ya Ibilisi?** Mardi Gras; ambayo ni sikukuu ambapo watu siku hiyo huvaa mapambo na vinyago vya kutisha usoni yaonekana kuongezeka umaarufu. Baadhi wanaamini kwamba ni sherehe sahihi hata kwa Wakristo. Lakini hili ni sawa?
- 32 Yesu Alimaanisha Nini – “Nataka Rehema, Wala si Sadaka”?** Kulingana na Yesu, rehema ni moja ya mambo yaliyo “mambo makuu ya sheria” (Mathayo 23:23). Hapa tunakuletea makala iliyoandikwa kwenye gazeti la zamani la Good News, ifafanuyayo juu ya hili.

Jarada la Nyuma: Internet na Radio. Hii inaonyesha ni wapi watu wanaweza kuupata ujumbe toka Kanisa la Continuing Church of God.

Kuhusu Jarada la Mbele: Baadhi wanaamini kwamba “miezi ya rangi ya damu” itakayotokea mwaka 2014 na/ au 2015 ni dalili kwamba Yesu anakaribia kurejea. Lakini Biblia yatufundisha nini?

Unabii wa Habari za Biblia huchapishwa na Kanisa la Continuing Church of God, 1248 E. Grand Avenue, Suite A, Arroyo Grande, CA, 93420. <http://www.ccog.org>

©2014 Continuing Church of God. Limechapishwa katika U.S.A. Haki zote zimehifadhiwa.

Kunakiri makala yote ama sehemu yake pasipo ruhusa ya kimaandishi toka kwa mmiliki hairuhusiwi. Tunaheshimu haki zako hivyo hatutoi, kuuza ama kukodisha orodha ya mawasiliano yetu. Endapo haungependa kuendelea kupokea gazeti hili, wasiliana na office yetu iliyoko Arroyo Grande. Maandiko yamenukuriwa toka New King James Version (©Thomas Nelson, Inc., Publishers, used by permission) Isipokuwa pale tu tumeelekeza vinginevyo.

Unabii wa Habari za Biblia-HUWEZESHA KWA MICHANGO YENU

Bible News Prophecy has no subscription or newsstand price. This magazine is provided free of charge by the Continuing Church of God. It is made possible by the voluntary, freely given tithes and offerings of the membership of the Church and others who have elected to support the work of the Church. Contributions are gratefully welcomed and are tax-deductible in the U.S. Those who wish to voluntarily aid and support this worldwide Work of God are gladly welcomed as co-workers in this major effort to preach and publish the gospel to all nations. Contributions should be sent to: Continuing Church of God, 1248 E. Grand Avenue, Suite A, Arroyo Grande, CA, 93420.

Mhariri Mkuu: Bob Thiel

Mpigachapa/Mhariri Msaidizi: Joyce Thiel

Masahihisho na: Kayla Morgan

Maandalizi & Uchapaji: Burdine Printing

Picha: Picha zote zimetokana na familia ya Thiel ama na vyanzo vya mitandao ya kijamii kama vile Wikipedia (ikiwa chanzo hakikutajwa, itakuwa ni kwa sababu inaaminika kwamba chanzo husika kililichia picha iwe kwa matumizi ya umma pasipo masharti yeyote).

TOKA KWA MHARIRI MKUU: BOB THIEL

WAKRISTO WAMEIHUBIRI INJILI YA UFALME



Sote tunapaswa tujue kwamba Yesu alihubiri Injili ya Ufalme (Marko 1:14-15), aliwatuma mitume nao wakaihubiri (Luka 9:1-2), na walifanya hivyo (2 Petro 1:10-11; Matendo 19:8).

Lakini je, kunaviashiria vyovyote ikiwa wale waliofuatia baada ya mitume waliomkiri Kristo nao waliihubiri na walikuwa wanajua?

Jibu ni NDIYO.

Maandiko ya kale zaidi ya Kikristo yaliyohifadhiwa (ya mwishoni mwa karne ya kwanza) ni Barua kwa Wakorintho inayosema:

Mitume kwa ajili yetu...walienda huko na huko...wakihubiri injili kwamba Ufalme wa Mungu ulikuwa karibu kuja (xlii).

Hivyo ni dhahiri kwamba Wakristo wa awali walielewa juu ya ukweli kwamba mitume walizunguka kote wakihubiri injili ya Ufalme wa Mungu.

Ufalme wa Mungu ilikuwa pia sehemu muhimu katika kile kinachoaminika kuwa ni “hubiri la Kikristo la kale zaidi lililopo hadi leo “ (Holmes M.W. Ancient Christian Sermon. The Apostolic Fathers: Greek Texts and English Translations, 2nd ed. Baker Books, Grand Rapids, 2004). Hubiri hili ndani yake lina maelezo yafuatayo:

5:5 Zaidi ya hayo mnajua, ndugu, kwamba kuishi kwetu

katika ulimwengu wa mwili siyo kwa muhimu na kunapita, lakini ahadi ya Kristo ni ya umuhimu mkuu na ya kupendeza: pumziko katika ufalme ujao na katika uzima wa milele.

Maelezo ya hapo juu yanafundisha kwamba ufalme utatimia baadaye, lakini utakuja na utadumu milele. Zaidi ya hapo, hubiri hili la kale linaeleza:

6:9 Sasa ikiwa hata watu wenye haki kama hawa wameshindwa, kwa njia ya matendo yao wenyewe ya haki, kuwaokoa watoto wao, tutakuwa na hakika gani ya kuingia kwenye Ufalme wa Mungu endapo tukishindwa kuulinda ubatizo wetu ubaki pasi na ila wala mawaa? Ama ni nani atakuwa mtetezi wetu, ikiwa hatukuonekana kuwa na matendo matakatifu na yenye haki?

9:6 Hivyo na tupendane sisi kwa sisi, ili sote tuweze kuingia kwenye Ufalme wa Mungu.

11:7 Hivyo, ikiwa tunajua kile kilicho sahihi machoni pa Mungu, tutaingia kwenye ufalme wake na kuipokea ahadi ambayo “sikio halijawahi kuisikia wala jicho kuwahi kuiona wala moyo wa mtu haujawahi kufikiria.”

12:1 Na tuongojee, Ufalme wa Mungu saa baada ya saa katika upendo na haki, kwa kuwa haitujui siku ya kutokea kwake Mungu.

Maelezo haya hapo juu yanaonyesha kwamba bado hatujauingia ufalme wa Mungu, na kwamba utatimia baada ya siku ya Mungu kurudi/kutokea –hii ni baada ya Yesu kurudi tena. Hubiri hili la kale pia linaeleza:

12:6 anasema, ufalme wa Baba yangu utakuja.

Maelezo haya yanabainisha kwamba ni ufalme wa Baba na kwamba bado unapaswa kuja. Ufalme si juu ya Yesu pekee.

Inastaajabisha, angalau kwangu, kwamba hubiri la Kikristo la kale zaidi miongoni mwa yaliyopo (lafanana na labainisha kuwa yaweza kuwa lilitokana na kundi la Church of God, japo ufinyu wa uelwa wangu wa Kigiriki unanifanya nisiweze kutamka kwa kujiamini juu ya hili) ambalo Mungu ameruhusu lidumu kuwepo linafundisha juu ya Ufalme wa Mungu sawa na kanisa la Continuing Church of God lifundishavyo sasa.

Viongozi wa Kanisa wa Karne ya Pili na Injili ya Ufalme

Inapaswa ieleweke kuwa Papias, aliyehubiriwa na Mtume Yohana ambaye pia alikuwa rafiki wa Polycarp (ambaye pia anachukuliwa kuwa ni mtakatifu na Roman Katoliki), mwanzoni mwa karne ya pili alifundisha juu ya ufalme. Eusebio

alituandika kwamba Papias (kiongozi wa mwanzoni mwa karne ya 2) alifundisha:

...kutakuwa na kipindi cha miaka elfu moja baada ya ufufuo wa wafu, na kwamba Ufalme wa Kristo utasimikwa kiuhalisia hapahapa duniani...(Eusebio. The History of the Church, Book III, Chapter XXIX, Verse 12, p. 69).

Papias alifundisha kwamba kipindi hicho kitakuwa ni wakati wa neema tele:

Katika hali hiyohiyo, [Alisema] kwamba punje moja ya ngano itazaa masuke elfu kumi, na kwamba kila suke litakuwa na punje elfu kumi, na kila punje itatoa kilo kumi za unga safi, mweupe na laini; na kwamba matunda ya tufaha (apples), na mbegu, na nyasi nazo zitazaa katika hali ya kiwango kilekile; na kuwa wanyama wote, watalisha kile kinachooota juu ya ardhi, watageuka kuwa wanyenyekevu na watulivu, na watawatii wanadamu pasi na mawaa.” [Ushuhuda umetolewa juu ya mambo haya kupitia maandiko ya Papias, mtu wa kale, ambaye alimsikia na kufundishwa na Mtume Yohana na pia alikuwa rafiki wa Polycarpo, yamo katika kitabu chake cha nne; kwani aliandika vitabu vitano...] (Fragments of Papias, IV).

Polycarpo wa Smyrna alikuwa kiongozi wa awali wa Kikristo, ambaye alikuwa mfuasi wa Yohana, mtume wa mwisho kufariki miongoni mwa mitume wa awali kumi na wawili. Kati ya mwaka 120-135 B.K. Polycarpo alifundisha:

“Wanayo heri wale walio maskini, pamoja na wale wateswao kwa ajili ya haki, kwani Ufalme wa Mungu ni wao “ (Polycarpo. Barua kwa Wafilipi, Sura ya II. Toka Ante-Nicene Fathers, Volume 1 as edited by Alexander Roberts & James Donaldson. American Edition, 1885).

Hivyo, tukijua kwamba, “Mungu hadhihakikiwi,” tunapaswa tuenende katika ustahili wa amri na utukufu wake...Kwani ni vema kwamba wanapaswa watengwe mbali na tamaa zilizomo ulimwenguni, kwani “kila tamaa inapiga vita dhidi ya roho; “na wala” si wazinzi, wala mashoga, wala si wajitiao wenyewe unajisi kupitia wanadamu, watakaourithi ufalme wa Mungu,” wala wale wafanyao mambo yasiyosahihi wala yasiompendeza (Polycarpo. Barua kwa Wafilipi, Sura ya V. Toka Ante-Nicene Fathers, Volume 1as edited by Alexander Roberts & James Donaldson. American Edition, 1885).

Hivyo sawa na Paulo na wengine wa wakati wa Agano Jipya, Polycarpo naye alifundisha kwamba wenye haki, siyo wavunja amri, wangeurithi ufalme wa Mungu.

Melito wa Sardi, ambaye ndiye alikuwa mrithi wa Polycarpo, mnamo 170 B.K., alifundisha:

Kwa maana ni dhahiri sheria iliyotolewa katika Injili—ya kale katika mpya, zote zikija pamoja kutoka Sayuni na Yerusalemu; na amri iliyotolewa katika neema, na kielelezo katika ukamilisho wake, na mwanakondoo akiwa ni Mwana wa Mungu, na kondoo katika mwanadamu, na mtu akiwa Mungu...

Lakini injili ilifanyika ufafanuzi wa sheria na utimilifu wake, wakati kanisa likiwa jumba la hazina ya ukweli...

Huyu ndiye aliyetukomboza toka utumwani kwenda kwenye uhuru, kutoka gizani kuja kwenye nuru, kutoka mautini kuja kwenye uzima, kutoka utawala wa kidhalimu kuja kwenye ufalme wa milele (Melito. Homily On the Passover. Verses 7,40,68. Translation from Kerux: The Journal of Online Theology (<http://www.kerux.com/documents/KeruxV4N1A1.asp> 09/14/05).

Hivyo ufalme wa Mungu ni jambo lililo la milele, na wala si ule Ukristo wa sasa ama kanisa la Kikatoliki kama wengi wadhaniavyo, na unahusu pia sheria ya Mungu.

Maandiko mengine ya kipindi cha katikati hadi mwishoni mwa karne ya pili yanawaasa wanadamu wautarajie ufalme:

Hivyo basi, na asiwepo yeyote kati yenu ajitengaye mwenyewe wala aangaliaye nyuma, bali na tujitoe katika kuifuata Injili ya ufalme wa Mungu (Roman Clement. Recognitions, Book X, Chapter XLV. Excerpted from Ante-Nicene Fathers, Volume 8. Edited by Alexander Roberts & James Donaldson. American Edition, 1886. Online Edition Copyright © 2005 by K. Knight).

Zaidi, japo inawezekana haikuandikwa na aliyekuwemo kwenye kanisa la kweli, maandiko ya kipindi cha kati cha karne ya pili yenye kichwa cha habari The Shepherd of Hermas yaliyotafasiriwa na Roberts & Donaldson nayo yanatumia neno “Ufalme wa Mungu” mara kumi na nne.

Ni kweli, na ni wengi wa walioukiri Ukristo, wa nyakati za karne ya pili walijua juu ya kuja kwa ufalme wa Mungu.

Hata mzushi Irenaeus alielewa kuwa baada ya ufufuo, Wakristo wangeingia kwenye ufalme wa Mungu. Gundua juu ya kile alichandika, mnamo 180 B.K.:

Kwa maana hiyo ndiyo hali yao walioamini, kwani ndani yao daima Roho Takatifu inakaa, ambayo ilitolewa kwao na Mungu siku ya ubatizo, na huhifadhiwa na anayempokea ndani yake, endapo atatembea katika ukweli na utakatifu na haki na subira na uvumilivu. Kwani hii nafsi inao ufufuo kwa hao wanaoamini, mwili ukiipokea nafsi tena, na pamoja nayo, uweza wa Roho Mtakatifu, wakifufuliwa na kuingia kwenye ufalme wa Mungu (Irenaeus, Mtakatifu., Askofu wa Lyon. Imetafsiriwa toka “Waarmenia na Armitage Robinson. The Demonstration of the Apostolic Preaching, Chapter 42. Wells, Somerset, Oct. 1879. As published in SOCIETY FOR PROMOTING CHRISTIAN KNOWLEDGE. NEW YORK: THE MACMILLAN CO, 1920).

Matatizo katika Karne ya Pili na ya Tatu

Mnamo karne ya pili, kiongozi aliyekuwa mpinzani wa sheria ya Mungu aliyeitwa Marcion aliinuka akifundisha kinyume dhidi ya Sheria, Sabato, na hata uhalisia wa ufalme wa Mungu kuja duniani. Pamoja na kwamba alipingwa vikali na Polycarpo na

wengine, yeye alikuwa na mawasiliano na Kanisa la Rumi kwa kipindi kirefu na hata kufikia kukubalika huko.

Katika karne ya pili na ya tatu, wale waaminio juu ya kila jambo katika Biblia ni mfano tu (Waallegoristi) walianza kupata umaarufu na kukubalika kule Alexandria (Misri). Hawa waliipiga vita imani juu ya kuja kwa ufalme. Jionee taarifa juu ya Dionysio na waallegoristi:

Dionysio alizaliwa katika familia tajiri na yenye heshima iliyokuwa ya kipaganai kule Alexandria, na hivyo alifundishwa falsafa ya Waallegoristi. Baadaye aliondoka kwenye shule za kipagani na kuwa mwanafunzi wa Origen, ambaye ndiye alikuwa amerithi majukumu ya shule ya kidini ya Alexandria...

Clement, Origen, pamoja na shule ya Wagnosti walikuwa wakiyapotoa mafundisho ya imani takatifu kwa kila swala kulifafanua liwe ni mfano/mbadala na fumbo tu...Kutokana na mtazamo wao huo wakajipatia jina la "Waallegoristi." Nepos alipambana waziwazi na Waallegoristi hawa, akisisitiza kwamba kutakuwa na utawala wa Kristo wa hapa hapa duniani...

Dionysio alibishana na wafuasi wa Nepos, na madai yake yalikuwa..."hali hiyo tayari imetimia katika ufalme wa Mungu uliopo." Hapa ndipo tunakutana na tamko la awali kabisa la kutajwa kwa ufalme wa Mungu kuwa ni kanisa katika hali yake ya sasa ...

Nepos alikemea upotofu na makosa yao, akionyesha kwamba ufalme wa mbinguni si wa kimfano tu (allegorical), bali ni kitu halisi kitakachokuja duniani kikiwa ni Ufalme wa Milele wa Bwana kupitia ufufuo wa uzima wa milele...

Hivyo wazo la kwamba ufalme tayari umeshatimia kupitia kanisa likiwa katika hali yake ya sasa lilibuniwa na kuenezwa kutokea kwenye shule ya Wa-Gnostic wa ki-Allegoristi kule Misri, Kati ya mwaka 200 hadi 250 B.K., kadri ya karne nzima kabla ya maaskofu wa utawala huo walipoanza kuchukuliwa kuwa ni wameketi juu ya kiti cha enzi cha ufalme huo wa Kristo ...

Clement yeye alibuni wazo la kwamba ufalme wa Mungu ni hali ya uelewa sahihi wa mambo ya Mungu. Origen yeye akalibadiri wazo hilo kuwa ni maana za kiroho zilizojificha ndani ya maelezo fasaha ya Biblia (Ward, Henry Dana. Injili ya Ufalme: Ufalme usio wa ulimwengu huu; Si Ulimwengu huu; Bali utakuja katika Nchi ya Kimbingu, juu ya Ufufuo wa Wafu na Juu ya Kufanywa upya kwa Mambo yote. Published by Claxton, Remsen & Haffelfinger, 1870. Original from the New York Public Library, Digitized Jul 18, 2006, pp. 124-125).

Hivyo, wakati Nepos alifundisha juu ya Injili ya Ufalme wa Mungu, Waallegoristi walijaribu kuingiza ufafanuzi tofauti, wa uongo, na upingao juu ya uhalisia wa kutimia kwake duniani. Apollinaris wa Hierapolis alijaribu kupambana na upotoshaji huo wa waallegoristi katika kipindi hichohicho.

Herbert W. Armstrong Alifundisha Juu ya Ufalme wa Mungu

Katika karne ya 20, kupitia kitabu chake kiitwacho "The Mystery of the Ages" – Kikimaanisha "Siri ya Zama", marehemu Herbert W. Armstrong aliandika:

Yesu alienda kila mahali akihubiri HABARI NJEMA ya UFALME WA MUNGU. Alifundisha kwa mafumbo juu ya UFALME WA MUNGU. Aliwatuma wanafunzi sabini waende wakahubiri, na akawaagiza wahubiri juu ya UFALME WA MUNGU (Luka 10:9). Baadaye aliwatuma Mitume, ambao juu yao ndipo Kanisa la Mungu limejengwa, akawaagiza kuuhubiri UFALME WA MUNGU (Luka 9:1-2). Baada ya kufufuka kwake, kabla hajapaa kwenda mbinguni, Yesu aliwafundisha tena wanafunzi wake juu ya ufalme wa Mungu (Matendo 1:3).

Je, si swala la kustaajibisha kwamba ulimwengu UMEPOTEZA elimu juu ya Injili inahusu nini?

Mtume Paulo alihubiri juu ya UFALME WA MUNGU (Matendo 19:8; 20:25; 28:23, 31)...

Ni kwa sababu waliikataa Injili ya Kristo takribani miaka 1,900 iliyopita, ulimwengu ulilazimika kubuni kitu mbadala badala yake. Wakalazimika kubuni mbadala bandia! Hivyo tumesikia ufalme wa Mungu ukifundishwa kuwa ni kitu cha kuvutia kilichoko sayari ingine – ama ni tulizo la kujisikia vizuri moyoni – na hivyo kuipunguza umuhimu na ukuu wake kwa kuifanya kitu cha kufikirika tu, kisicho halisi, KISICHO MUHIMU! Wengine nao wamepotosha kwa kufundisha kwamba "KANISA" ndiyo ufalme. Wengine huuchanganya na Umillenia. Bado wengine, mapema katika karne yetu, walidiriki kudai kwamba Himaya ya Kiingereza (British Empire) ndiyo ilikuwa ufalme wa Mungu; japo kwa sasa hakuna anayediriki kutoa madai ya kipuuzi kama hayo. NI JINSI GANI ULIMWENGU HUU HUDANGANYIKA! Nabii Danieli, ambaye aliishi miaka takribani 600 kabla ya Kristo, yeye alijua wazi kwamba ufalme wa Mungu ulikuwa ni serkali halisi – ni serkali yenye madaraka makuu itakayowatawala WANADAMU wote hapahapa duniani...

Hapa tunakuletea, katika LUGHA WAZI, ufafanuzi wa Mungu juu ya UFALME WA MUNGU ni nini: "Na katika siku za wafalme hawa..."—hapa inazungumzia juu ya vidole kumi, vilivyvo sehemu ya nusu udongo nusu chuma. Hili tukiunganisha unabii wa Danieli 7, na Ufunuo 13 na 17, tunakuta inaeleza juu ya MUUNGANO MPYA WA ULAYA ambao tayari kwa sasa unajitengeneza, kutoka kwenye Soko la Pamoja la Ulaya (European Common Market), jambo linalotokea mbele ya macho yako mwenyewe! Ufunuo 17:12 inafunua wazi taarifa kwamba utakuwa ni muungano wa WAFALME KUMI AMA FALME KUMI ambazo (Ufu. 17:8) zitaifufua MILKI YA RUMI ya Kale. Hivyo, chukua tahadhari kuhusu muda unaotabiwa! "Katika siku za wafalme hawa"—yaani ndani ya nyakati za mataifa ama kundi la mataifa ambayo, KATIKA NYAKATI ZETU,

yataibua japo kwa mda mfupi Milki ya Rumi –ona kile kitakachotokea: “...Mungu wa mbinguni atausimika ufalme, ambao hautaangamizwa...bali utavunja vipandevipande na kuangamiza falme hizi zote, nao utadumu milele!”

...Pale Kristo ajapo, anakuja akiwa MFALME wa wafalme, akiitawala dunia yote (Ufunuo inaeleza: ATAZIANGAMIZA falme zote hizi za kiulimwengu). Ufunuo 11:15 inaeleza kuwa: “Falme za dunia hii zimekuwa FALME ZA BWANA WETU, NA ZA KRISTO WAKE; naye atatawala milele na milele!” Hiki kinachoongelewa hapa ndicho UFALME WA MUNGU. Ni MWISHO WA SERKALI ZA SASA – ndiyo, ni mwisho hata wa serkali kuu na yenye uwezo kama Marekani au Uingereza. Muda huu ukifika zote zitakuwa falme—SERKALI – za Bwana YESU KRISTO, akiwa tangia hapo ndiye MFALME wa wafalme juu ya dunia yote. Hili ndilo linaufanya ueleweke WAZI ukweli kuwa UFALME WA MUNGU ni halisi na dhahiri, si ufalme wa kufikirika. Sawa na jinsi Milki ya Wakaldayo ilivyokuwa MILKI—sawa na jinsi Milki ya Rumi ilivyokuwa MILKI – hali kadharika UFALME WA MUNGU ni serkali. Utaziondoa na kuzirithi SERKALI zote za MATAIFA ya ulimwengu. Yesu Kristo ALIZALIWA ili aje kuwa MFALME -- MTAWALA....!

Yesu Kristo yuleyule aliyetembea kupita vilima na mabonde vya Nchi Takatifu pamoja na katika mitaa ya Yerusalemu zaidi ya miaka 1900 iliyopita anakuja tena. Alisema kuwa angekuja. Baada ya kusurubiwa, Mungu alimfufua kutoka mautini baada ya mchana tatu na usiku tatu (Mat. 12:40; Mdo 2:32; I Kor. 15:3-4). Kisha akapaa kwenda kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu. Kwenye Makao Makuu ya Serkali ya Mbingu na Nchi (Mdo. 1:9-11; Ebr. 1:3; 8:1; 10:12; Ufu. 3:21)... yuko mbinguni hadi “zije zama za kufanywa upya vitu vyote” (Mdo 3:19-21). Kufanywa upya inamaanisha kurudishwa kwa kila kitu kwenye hali yake ya mwanzo kama kilivyoumbwa. Katika hili, kufanywa upya kwa serkali ya Mungu hapa duniani, na hivyo, itaambatana na kurejeshwa kwa amani ulimwenguni, na hali kamififu ya kufikirika.

Vurugu za ulimwengu wa sasa, vita vinavyozidi kuongezeka pamoja na mapambano zitapelekea matatizo ya ulimwengu makubwa mno kiasi kwamba, Mungu asipoingilia kati, hakuna mwanadamu yeyote ambaye angeokolewa akiwa hai (Mat. 24:22). Kufikia kwenye hatima yake ambapo kuchelewa kuingilia kati kungepelekea kuangamizwa kwa uhai wote ulioko kwenye sayari hii, Yesu Kristo atawajibika kurejea. Huu ndio wakati ajapo akiwa ni Mungu mtakatifu. Anarejea katika uwezo wote na utukufu wa Mwumbaji atawalaye mbingu na nchi. (Mat. 24:30; 25:31). Anarejea akiwa “Mfalme wa wafalme, na Bwana wa mabwana” (Ufu. 19:16), kuja kusimika serkali ya kiuwezo ya ulimwengu na kuyatawala mataifa yote “kwa fimbo ya chuma” (Ufu. 19:15; 12:5)...

Kristo anakuja...

Kristo Hapokelewi?

Lakini je wanadamu watapiga kelele kwa furaha, na kumpokea/kumkaribisha kwa shangwe na vifijo? Je hata makanisa ya Ukristo wa jadi yatashangilia kwa kurudi kwake?

Haitakuwa hivyo! Hawataamini, kwa sababu walimu wa uongo wa Shetani (II Kor. 11:13-15) wamewapotosha, wataamini kuwa huyo wamwonaye akija ni Mpingakristo. Makanisa na mataifa watakasirika kwa kuja kwake (Ufu. 11:15 na 11:18), nayo majeshi ya vita kwa kweli yatadiriki kujaribu kupambana naye ili kumwagamiza (Ufu. 17:14)!

Mataifa yatahusika katika mapambano ya hitimisho ya Vita ya Dunia ya III, na Yerusalemu ikiwa ndipo uwanja wa mapambano (Zek. 14:1-2), na hapo ndipo Kristo atakaporejea. Kwa uwezo mkuu wa Kimungu “atapigana dhidi ya hayo mataifa “ yaliyokuja kupigana dhidi yake (aya ya 3). Atawashinda kabisa na kuwaangamiza (Ufu. 17:14)! “Na siku hiyo miguu yake itasimama juu ya Mlima wa Mizeituni” ulio mwendo mfupi tu mashariki mwa Yerusalemu (Zek. 14:4).

Hivyo, Yesu atarudi na atashinda, hata kama wengi watadai (kutokana na kutouelewa vema unabii wa Biblia, na kwa sehemu ni kutokana na manabii wa uongo na madanganyo) kwamba Yesu wamwonaye akirejea kuwa ni Mpingakristo.

Biblia inafundisha kwamba “Mungu ni pendo” (1 Yohana 4:8,16) na kwamba Yesu ni Mungu (Yohana 1:1,14 – ufalme wa Mungu utakuwa na Mtawala awapendaye watu wake kwani ni upendo na sheria zake ni za upendo.

Yafuatayo pia yanatoka katika kitabu cha Herbert W. Armstrong, The Mystery of the Ages:

Dini ya kweli – ukweli wa Mungu uwezeshwao kwa upendo wa Mungu utolewao na Roho Takatifu...FURAHA ISIOSEMEKA ya kumjua Mungu na Yesu Kristo – ya kuujua UKWELI – na uzuri wa PENDO takatifu la ki-Mungu!...

Mafundisho ya Kanisa la kweli la Mungu kwa ujumla ni yale ya “kuishi kwa kila neno” la kwenye Biblia Takatifu...

Wanadamu watageuka kutoka njia ya “kupata” na kugeukia njia ya “kutoa” – njia ya Mungu ya upendo.

USTAARABU MPYA sasa utatapakaa kwenye nchi!

USTAARABU MPYA ndiyo ufalme wa Mungu. Kutangaza kwamba ustaarabu mpya utakuja na utajikita kwenye upendo ndiyo sehemu kuu ya kile injili ya kweli ya ufalme ambayo Yesu na wafuasi wake walifundisha. Na hilo ndilo sisi tulio wa Kanisa la Continuing Church of God tunahubiri vilevile.

Herbert Armstrong aligundua kwamba Yesu alikuwa akifundisha kwamba jamii ya wanadamu, hata pale idhaniapo kwamba iko tayari na ingependa kutii, haiwezi kwani imekataa njia ya maisha ya utoaji, ambayo ni njia ya upendo. Karibia hakuna yeyote aonekanaye kuelewa barabara umuhimu wa kile

ambacho Yesu alikuwa akihubiri.

Katika kutusaidia ili tufanyike sehemu ya ufalme huo, Mungu aliwapenda wanadamu kwa kiasi kikubwa mno kiasi kwamba alimtuma Yesu aje afe kwa ajili yetu (Yohana 3:16-17).

Injili ya Ufalme ndicho Kitu ambacho Ulimwengu unakihitaji, Lakini...

Ijapokuwa wanadamu wanahitaji Kristo arejee na kusimikwa kwa ufalme wake, wengi ulimwenguni hawataujali ujumbe huu katika karne hii ya 21. Hata hivyo ulimwengu utakuwa umepewa ushuhuda.

Kumbuka kuwa Yesu alifundisha:

“14 Na injili hii ya ufalme itahubiriwa ulimwenguni kote kwa ushuhuda kwa mataifa yote, na ndipo mwisho utakapokuja” (Mathayo 24:14).

Gundua inaeleza kwamba injili ya ufalme itayafikia mataifa yote kama ushuhuda, ndipo mwisho uje.

Zipo sababu kadhaa dhidi ya hili.

Moja ni kwamba Mungu anataka ulimwengu uisikie injili ya kweli kabla ya kuanza kwa Dhiki Kuu (ambayo imeonyeshwa kuanza katika Mathayo 24:21). Hivyo ujumbe wa injili ni ushuhuda na ni maonyo (Ezekia 3; Amosi 3:7).

Sababu nyingine ni kwamba kiini cha ujumbe wa injili ya kweli kitakuwa kinyume cha mitazamo ya Mnyama anayeinuka, Mamlaka ya Mfalme wa Kaskazini, pamoja na Nabii wa Uongo, Mpingakristo wa mwisho. Hawa kimsingi wataahidi kupatikana kwa amani kupitia jitihada za kibinadamu, lakini hilo litapeleka uharibifu (1 Wathesalonike 5:3).

Kwa sababu ya ishara na miujiza ya uongo itakayoambatana nao (2 Wathesalonike 2:9), ulimwengu utachagua kuwaamini na kuuamini uongo (2 Wathesalonike 2:9-12) badala ya ujumbe wa injili.

Wanafiladefia waaminifu (Ufunuo 3:7-13), watakuwa wakiiambia dunia kile ambacho viongozi hawa wa kidunia wanachoenda kufanya. Watasaidia jitihada za kuushitua ulimwengu kupitia ujumbe kwamba Mnyama, mamlaka ya Mfalme wa Kaskazini, pamoja na Nabii wa Uongo, Mpingakristo wa mwisho, hatimaye wataziangamiza (wakishirikiana na wenzao) Marekani na Mataifa ya Kiingereza ya Uingereza (United Kingdom), Canada, Australia, pamoja na New Zealand (Danieli 11:39). Kwamba mda mfupi baada ya hilo watayaangamiza mataifa yaliyoungana ya Umoja wa nchi za Kiarabu/Kiislamu (Danieli 11:40-43), wakitenda kazi kama vyombo vya mashetani (Ufunuo 16:13-14), na hatimaye yatapambana na Yesu Kristo pale arudipo (Ufunuo 16:14; 19:19-20). Wanafiladefia waaminifu (Ufunuo 3:7-13) watakuwa wakitangaza kwamba utawala wa kimillenia hivi punde karibu unawadia.

Na viongozi hawa (yaweza kuwa kuja kwa namna fulani ya

kiongozi mkuu wa Ulaya akiwa pamoja na kiongozi mkuu wa kidini kama Papa) hawatapenda kusikia wala kuona dunia ikihubiriwa ujumbe huu – hawatapenda ulimwengu ujifunze kile ambacho wanakusudia kutekeleza (na hata wao wenyewe mwanzoni hawataamini kuwa wao ndio wanaosemwa, Isaya 10:5-7). Wao ama/pamoja na wafuasi wao nao watahubiri kiuongo kuwa Wanafiladefia waaminifu hao wanahubiri imani chafu (Umillenia) inayomhusu Mpingakristo.

Shutuma zozote zile ambazo watazitoa juu ya Wanafiladefia waaminifu na juu ya Kanisa la Continuing Church of God zitapeleka kuteswa kwa watakatifu hawa (Danieli 11:29-35, Ufunuo 12:13-15. Hili nalo litausababisha mwisho ufike/uje – kuanza kwa Dhiki Kuu (Mathayo 24:21; Danieli 11:39; Mathayo 24:15; Danieli 11:31) pamoja na kuwadia kwa muda wa kuhifadhiwa kwa Wakristo Wanafiladefia waaminifu (Ufunuo 3:10; 12:14-16).

Mnyama na Nabii wa Uongo watajaribu kulazimisha, kujaribu kutumia hongo ya pesa na uchumi, ishara, miujiza ya uongo, mauaji, na mbinu zingine (Ufunuo 13:10-17, 16:14; Danieli 7:25; 2 Wathesalonike 2:9-10) ili wote wawatii.

Pamoja na hayo, Yesu atarejea na ufalme wa Mungu wa millennia utasimikwa juu ya dunia. Mungu pamoja na Wakristo waaminifu watashinda.

Maoni ya Hitimisho

Ufalme wa Mungu ni ufalme halisia utakaosimikwa juu ya dunia. Utaendeshwa kwa sherai za Mungu za upendo ukiongozwa na Mungu wa upendo. Ufalme huu utahusisha wale walio katika Kanisa la Mungu kikwelikweli, lakini hakuna andiko lielekezalo kwamba Kanisa ndilo ufalme wa Mungu (kama Wakatholiki na wengine wadhaniavyo).

Katika hatua yake ya awali, watakatifu watatawala pamoja na Kristo kwa miaka elfu moja juu ya mataifa yote. Katika hatua yake ya mwisho, utahusisha “Yerusalemu Mpya, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mungu” na maongeo (kuongezeka) ya ufalme huo hayatakuwa na mwisho. Hakutakuwa tena na uovu ama kutokuwa na haki, hakutakuwa tena na majonzi, wala hakutakuwa na mauti tena.

Kuihubiri na kuelewa injili ya ufalme wa Mungu ndiyo dhamira kuu ya Biblia. Waandishi wa Agano la Kale walifundisha juu yake. Hotuba ya kale zaidi ya Kikristo iliyodumu kuwepo hadi leo itokanayo na Agano Jipya pia inahubiri juu yake. Viongozi wa Kikristo wa kipindi cha mwanzoni mwa karne ya pili, kama vile Polycarpo na Melito, nao walifundisha juu yake. Sisi tulio wa Kanisa la Continuing Church of God tunafundisha juu yake (fuatilia pia mahubiri yetu katika “Mtandao wa YouTube”, juu ya The Gospel of the Kingdom).

Kumbuka kwamba ufalme wa Mungu ndilo somo la kwanza kabisa ambalo Biblia inaonyesha Yesu alianzia kuhubiri juu yake. Ilikuwa ndilo swala alilolihubiri juu yake mara tu alipofufuka. Injili si juu ya maisha na kifo cha Yesu (japo maandiko na taarifa za awali zaonyesha, Yeye ni sehemu muhimu ya injili), msisitizo wa injili ambayo Yesu na wanafunzi wake waliihubiri ulikuwa

ni kuja kwa ufalme wa Mungu. Injili ya Ufalme inahusisha wokovu kupitia kwa Kristo, lakini pia inahusisha mafundisho juu ya kukoma kwa serkali za kibinadamu.

Vilevile, Yesu alifundisha kwamba mwisho usingewadia hadi baada ya injili ya ufalme kuwa imehubiriwa kwa ulimwengu kama ushuhuda kwa mataifa yote (Mathayo 24:14); na wengi hawatataka kuisikia ama kuiamini. Hivyo, kuihubiri injili ya ufalme wa Mungu ndilo somo muhimu. Hiki ndicho sisi tulio katika Kanisa la Continuing Church of God tumeweka mkazo katika kutekeleza.

MIEZI YA RANGI YA DAMU: JE, YESU ATAREJEA MWAKA 2014?



Mwezi wa Rangi ya Damu

Na Bob Thiel

Je, yawezekana Yesu akarejea 2014? Baadhi ya watu wanadhani hivyo. Mchungaji wa imani ya Kiprostanti Pastor John Hagee, pamoja na Mark Blitz, wanaelekeza kwenye kutokea kwa miezi yenye rangi ya damu ifikapo 2014 kama ndio uthibitisho.

Miezi ya rangi ya damu ni kitugani? Husababishwa na nini? Biblia inafundisha nini juu ya hilo? Vipi kuhusu mafundisho ya Kiyahudi? Je, taasisi ya anga ya Marekani NASA, imebashiri kutokea kwa miezi ya rangi ya damu?

Je, kutakuwa na mwezi maalum wa rangi ya damu ambao ndio utakuwa ishara toka kwa Mungu? Je, anaweza kurejea 2014 au 2015? Vipi juu ya 'Kanisa Kunyakuliwa'?

Makala hii itayajibu maswali haya na zaidi.

Miezi ya Rangi ya Damu ni Kitu Gani?

Mwezi wa rangi ya damu ni nini?

Sayansi ya tukio la "mwezi wa rangi ya damu". Husababishwa na kupatwa kwa nusu ya mwezi. Pale kivuli cha Dunia kinauziba mwezi kikamilifu, tunapata kupatwa kwa mwezi moja kwa moja. Kupatwa kwa mwezi nusu hutokea pale kivuli cha Dunia kinapoufunika mwezi sehemu tu. Dunia inapokuwa imekinga, mionzi ya mwezi hupinda kuzunguka mwisho wa dunia, na kutawanya miali mifupi (ya rangi ya kijani hadi hudhurungi), ikiacha ile miali

mirefu (miekundu, ya rangi ya chungwa na ya manjano) ikibakia kwenye kivuli cha dunia. Hii ndiyo sababu hata pale jua linapochomoza ama kuzama huwa la rangi nyekundu. Sawa na matukio yote ya kimiujiza ambayo yanaweza kufafanuliwa kisayansi, mwujiza si katika hali yake ya uasililia, bali ni katika majira ya kutokea kwake. (Yanover Y. Messianic 'Miezi ya Damu' Kutokea kwenye Usiku wa Pasaka. Jewish Press. <http://www.jewishpress.com/news/breaking-news/messianic-blood-moon-rising-on-passover-seder/2013/10/06> viewed 10/07/13).

Katika nchi za magharibi mwezi wa rangi ya damu pia hujulikana kama "Hunter's Moon" – Mwezi wa Mwindaji. Ndio mwezi wa kwanza kamili baada ya "Harvest Moon"— Mwezi wa Mavuno. Mwezi wa Mavuno ni ule mwezi kamili utokeo katika nchi za magharibi kwenye majira ya kati ya majira ya baridi na majira ya joto karibia kabisa na jua linapovuka Ikweta (equinox). Toka (Miezi ya Rangi ya Damu ni Nini? http://answers.ask.com/Society/Ethnicity/what_is_a_blood_moon viewed 10/08/13).

Mwezi wa Damu hutokea pale kupatwa kwa jua kikamilifu kunaufanya mwezi uonekane mwekundu. (Mwezi wa Damu ni Kitu Gani? <http://www.chacha.com/question/what-is-a-blood-moon#sthash.CACJZOWd.dpuf> viewed 10/08/13).

Kimsingi tafsiri ya 'mwezi wa rangi ya damu' ni pale mwezi uonekanapo mwekundu kutokana na miali jinsi inavyoweza kuonekana.

Kupatwa kwa mwezi siyo sababau pekee inayoweza kusababisha. Ebu ona yafuatayo:

Kuna hali chache zingine zinazoweza kusababisha mwezi uonekane mwekundu. Njia ya kawaida zaidi ya kusababisha Mwezi ubadirike kuwa mwekundu ni pale mwezi unapokuwa eneo la chini angani, punde tu mara baada ya mwezi kutoka ama pale unapotaka kuzama mwishoni mwa anga. Sawa na Jua, mwanga kutoka kwenye Mwezi sharti upite kuvuka eneo kubwa la angani wakati ukiwa umefika upande wa chini pembeni/ukingoni mwa eneo la dunia, tofauti na unapokuwa juu katikati angani. Anga la Dunia husababisha mwanga kusambaa, na kwa vile mwanga wa mwezi hutokana na miali ya jua iliyogonga na kusambaa kwenye mwezi, inaweza kusambaa hivyo pia. Miali miekundu huweza kupita kwenye anga na kutosambaa kwa kiwango kikubwa, wakati miali ya mwanga kwenye mwisho wa kibuluu wa taswira angani yenyewe husambaa kwa urahisi. Pale uonapo mwezi mwekundu, unachooni ni miali miekundu ambayo haikusambaa, lakini miali miekundu na ya kibuluu imesambazwa kuelekea kwingine. Hiyo ndiyo sababu kwa nini mwezi unaonekana mwekundu.

Sababu ya pili isababishayo mwezi mwekundu ni ikiwa kuna chembechembe katika anga...

Njia ya tatu – na ya kuvutia – ya mwezi kuwa mwekundu ni pale kunapotokea kupatwa kwa mwezi. Wakati wa kupatwa kwa mwezi, Mwezi huwa umepita nyuma ya kivuli cha Dunia, ambacho huufunika. Ikiwa ungeweza kuiangalia Dunia ukiwa ndani ya kivuli chake, ungeona kwamba anga lote linaloizunguka sayari hii limeng'ara wekundu. (Cain F. Red Moon. Universe Today, October 23, 21008. <http://www.universetoday.com/19969/red-moon/> viewed 10/09/13).

Na ninapaswa kuongeza hapa kwamba Mungu anaweza kusababisha mwezi uonekane kama damu kupitia njia zingine.

NASA na Miezi ya Rangi ya Damu

Taasisi ya Mambo ya Anga ya Marekani (The National Aeronautics and Space Administration -NASA) imetoa taarifa juu ya kutokea kwa miezi ya rangi ya damu huko nyuma.

Hapa nakuletea niliyowahi kuyaona kwenye tovuti ya NASA miaka kadhaa iliyopita:

Kisayansi pale panapokuwa na mifuatano minne ya kupatwa kwa mwezi wote, kundi hilo la miezi kupatwa mara nne huitwa "tetrad". Tetrad zifuatazo zimebashiriwa na NASA kwamba zitatokea katika kipindi cha karne hii:

Tetrad (Mifuatano Minne ya Mwezi Wote Kupatwa): 2003 – 2004.

Tetrad (Mifuatano Minne ya Mwezi Wote Kupatwa): 2014 – 2015.

Tetrad (Mifuatano Minne ya Mwezi Wote Kupatwa): 2032 – 2033.

Tetrad (Mifuatano Minne ya Mwezi Wote Kupatwa): 2043 – 2044.

Tetrad (Mifuatano Minne ya Mwezi Wote Kupatwa): 2050 – 2051.

Tetrad (Mifuatano Minne ya Mwezi Wote Kupatwa): 2061 – 2062.

Tetrad (Mifuatano Minne ya Mwezi Wote Kupatwa): 2072 – 2073.

Tetrad (Mifuatano Minne ya Mwezi Wote Kupatwa): 2090 – 2091. (<http://eclipse.gsfc.nasa.gov/LEcat/LE2001-2100.html> viewed 5/01/08).

Kwa kuwa siamini kwamba Biblia inaruhusu Yesu kurudi ama Siku ya Bwana kuanza katika 2014 au 2015 hivyo siyo sahihi kwamba kurejea kwa Yesu kunauhusiano wowote na orodha hiyo hapo juu ya kutokea kwa miezi miekundu katika miaka hiyo.

Kwa wakati huu, inaweza kuonekana kwamba unabii wa Ufunuo na wa Yoeli juu ya miezi ya rangi ya damu HAUWEZI kuhusiana na miezi yoyote ya rangi nyekundu ya ubashiri wa Taasisi ya NASA (hadi labda NASA walete orodha nyingine ama kitu kingine) au ikiwa kurudi kwa Kristo bado hadi mwaka 2032. Miezi ya rangi ya damu ya unabii wa Biblia inaweza kuhusiana na hali ya kiasili isiyoeleweka kwa wanasayansi kwa wakati huu

ama inaweza kuwa ni miujiza toka kwa Mungu – ama yaweza kuwa kwamba Mungu atafanya mambo fulani kwenye sayari ili kusababisha miezi hiyo itokee.

Ebu jionee madai ya mtu mmoja aliyetembelea tovuti ya Taasisi hiyo:

Tovuti ya NASA inabashiri kwamba kupatwa kwa mwezi wote kutatokea tarehe 15 Aprili 2014. Kupatwa huko kwa mwezi kutakoufanya mwezi uonekane kama damu kutatokea kwenye sikukuu ya Pasaka ya Wayahudi... (<http://redmoonrapture.com/2014-2015/2014-passover-ecilpse.html> viewed 10/09/13).

Tovuti ya NASA inabashiri kutokea kupatwa kwa mwezi wote kwenye tarehe 8 Octoba 2014. Kupatwa huko kwa mwezi kutakoufanya mwezi uwe wa rangi ya damu kutatokea kwenye siku ya Sikukuu ya Kiyahudi ya Vibanda... (<http://redmoonrapture.com/2014-2015/2014-tabernacles-eclipse.html> viewed 10/09/13).

Tovuti ya NASA inabashiri kutokea kupatwa kwa mwezi wote kwenye tarehe 4 Aprili 2015. . Kupatwa huko kwa mwezi kutakoufanya mwezi uwe wa rangi ya damu kutatokea kwenye siku ya Sikukuu ya Kiyahudi ya Pasaka... (<http://redmoonrapture.com/2014-2015/2015-passover-eclipse.html> viewed 10/09/13).

Tovuti ya NASA inabashiri kutokea kupatwa kwa mwezi wote kwenye tarehe 28 Septemba 2015. Kupatwa huko kwa mwezi kutakoufanya mwezi uwe wa rangi ya damu kutatokea kwenye siku ya Sikukuu ya Kiyahudi ya Vibanda... (<http://redmoonrapture.com/2014-2015/2015-tabernacles-eclipse.html> viewed 10/09/13).

Tarehe zilizotajwa hapa kuhusiana na Sikukuu ya Pasaka zitachelewa kwa siku kadhaa na hivyo haziashirii Pasaka yenyewe ya Kibiblia (Ona Kalenda ya Sikukuu Takatifu). Tarehe za Sikukuu ya Vibanda zi karibu na zile halisi; za 2014 zinaendana na tarehe ya kuanza kwa Sukukuu hiyo, ambapo za 2015 yaonekana zinaangukia kwenye siku baada ya Sikukuu hiyo kuanza, japo pengine kutokana na tofauti ya saa ya siku kuanza kati ya bara na jingine, labda tarehe hiyo inalenga siku ileile ya kuanza kwa sikukuu.

Biblia na Miezi ya Damu

Sehemu ya kwanza kabisa katika Biblia palipotajwa damu na mwezi pamoja ni katika Kitabu cha Yoeli kama ifuatavyo:

“30 Nami nitaonyesha maajabu katika mbingu na juu ya nchi, damu, moto na wimbi la moshi. 31Jua litageuzwa kuwa giza na mwezi kuwa damu kabla ya kuja siku ya BWANA iliyo kuu na ya kutisha” (Yoeli 2:30-31).

Baadhi yaonekana wanadhani kwamba aya hizi juu zinaongelea juu ya “miezi ya rangi ya damu” ya kawaida, na wengine wanaamini kuwa tukio hili ni la kipekee.

Sehemu inayofuata katika Biblia ambapo damu na mwezi zimetajwa kwa pamoja ni katika Kitabu cha Matendo ya Mitume, ambako Mtume Petro anaeleza yafuatayo:

17“Katika siku za mwisho, asema Bwana, nitamimina Roho yangu juu ya wote

wenye mwili. Wana wenu na binti zetu watatabiri, vijana wenu wataona maono na wazee wenu wataota ndoto. 18Hata juu ya watumishi wangu nitamwaga Roho yangu, nao watatabiri”. 19Nami nitaonyesha maajabu mbinguni juu na ishara duniani chini, moto na mvuke wa moshi mnene. 20Jua litakuwa giza na mwezi utakuwa mwekundu kama damu, kabla ya kuja siku ile kuu ya Bwana iliyo tukufu. 21Lakini ye yote atakayeliita jina la Bwana, ataokolewa” (Matendo 2:17-21).

Katika Kitabu cha Ufunuo tunasoma:

“12 Nikaangalia, Naye alipokuwa akiivunja ile lakiri ya sita, pakatokea tetemeko kuu la nchi na jua likawa jeusi kama nguo ya gunia iliyotengenezwa kwa singa za mbuzi, mwezi wote ukawa mwekundu kama damu. 13Nyota zilizo angani zikaanguka ardhini kama vile matunda ya mtini yasiyokomaa yaangukavyo wakati mti wake unapotikiswa na upepo mkali. 14Anga ikatoweka kama vile karatasi isokotwavyo na kila mlima na kila kisiwa kikaondolewa mahali pake. 15Ndipo wafalme wa duniani, wakuu wote, majemadari, matajiri, wenye nguvu na kila mtu, mtumwa na mtu huru, wakajificha katika mapango na kwenye miamba ya milima”. (Ufunuo 6:12-15).

Tukio la kibiblia lihusishalo mwezi kugeuka kuwa damu vilevile limeunganishwa na jua kugeuka jeusi. Wakati baadhi yaonekana wanaamini hili ni kielelezo cha kupatwa kwa jua kwa kawaida, ukweli ni kwamba kiashilio hicho kinalenga tukio lililo zaidi ya hapo. Fahamu kwamba hayo yanatokea baada ya kitasa cha sita kufunguliwa, ambayo ni baada ya kitasa cha tano kufunguliwa (Ufunuo 6:9), ambapo ni kuanza kwa Dhiki Kuu, ambayo kwa sasa bado haijaanza na haiwezi kuanza hadi angalau mwaka 2018 (Danieli 9:27,11:31; Mathayo 24).

Matukio yaliyotajwa hapo juu katika Yoeli 2, Matendo 2, na Ufunuo 6 pia yanafanana na yale aliyoyazungumzia Yesu katika Mathayo 24. Jionee:

29“ Mara baada ya dhiki ya siku zile, jua litatiwa giza, nao mwezi hautatoa nuru yake, nazo nyota zitaanguka kutoka angani na nguvu za anga zitatikisika.’ 30“Ndipo itakapotokea ishara ya Mwana wa Adamu angani na makabila yote ya dunia yataomboleza. Nao watamwona Mwana wa Adamu akija juu ya mawingu ya angani, katika uwezo na utukufu mkuu. 31Naye atawatuma malaika zake kwa sauti kuu ya tarumbeta, nao watawakusanya wateule wake kutoka pande zote nne za dunia, kutoka mwisho mmoja wa mbingu hadi mwisho mwingine” (Mathayo 24:29-31).

Baadhi ambao wanaamini juu ya “Kunyakuliwa kabla ya dhiki”

wamependekeza kwamba mwezi kugeuka kuwa damu ni ishara kwamba Yesu anakaribia kurudi. Pamoja na kuwa Yesu atarejea, gundua kwamba muda wa tukio hilo ameliaminisha kuwa ni BAADA ya dhiki kulingana na yale Yesu aliyofundisha. Gundua pia:

25“ Kutakuwa na ishara katika jua, mwezi na nyota. Hapa duniani, mataifa yatakuwa katika dhiki na fadhaa kutokana na ngurumo na misukosuko ya bahari. 26Watu watazimia roho kutokana na hofu kuu na kuyaona yale mambo yanayotokea duniani, kwa maana nguvu za vitu vya angani zitatikisika. 27Wakati huo ndipo watakapomwona Mwana wa Adamu akija mawinguni pamoja na uweza na utukufu mkuu. 28Mambo haya yatakapoanza kutendeka, simameni na mkaviinue vichwa vyenu, kwa sababu ukombozi wenu umekaribia.” (Luka 21:25-28).

Kumbuka kwamba kutakuwepo pia kusukasuka kwa bahari – kielelezo hiki cha bahari kutikisika hakitatokea kwenye mwaka 2014 wala 2015—kwani ni mapema mno (Ufunuo 16:12-16,18).

Vilevile, angalau mmoja amedai kwamba usulubisho wa Kristo uliambatana na miezi kuwa damu:

Mifuatano 4 ya mwezi kupatwa wote na kugeuka Mwekundu kama Damu ilitokea kwenye Pasaka ya Wayahudi na Sikukuu za Vibanda katika mwaka 32 na 33 BK. Yesu mwenyewe aliishuhudia mifuatano miwili ya kupatwa kwa mwezi na kuonekana ya rangi ya damu katika mwaka 32 BK. Kristo alishuka kuzimu punde tu kabla ya Pasaka ya Wayahudi iliyoambatana na kupatwa kwa jua kwa mwaka 33 B.K. akiwa kesho surubishwa masaa kadhaa kabla, na tayari alikuwa keshapaa kwa Baba Mbinguni wakati Sikukuu ya Vibanda ya mwaka 33 BK. iliyoambatana na mwezi kupatwa na kugeuka damu ilipowadia. (<http://redmoonrapture.com/crucifixion.html> viewed 10/09/13).

Lakini kwa kuwa kusulubishwa hakukuwa katika mwaka wa 32 au 33 BK. (Kulitokea mwaka 31 au hata 30 BK. Ndiyo miaka inayoonekana kupatana zaidi na Kalenda ya Kibiblia), kudai hivyo kwa kutumia taarifa za Injili, wakati mwaka 32 au 33 BK. haiendani; basi ni dhahiri madai hayo hapo juu yana makosa mengi.

Mila za Kiyahudi na Kupatwa Kwa Miezi na Miezi ya Damu

Baadhi wanafuatilia kuja kwa miezi ya damu kwa vile wanaamini kwamba inaashiria kutokea kwa swala fulani muhimu, kulingana na mila za Kiyahidi na matukio fulani ya kihistoria.

Yafuatayo ni kutoka kwenye Talmud (Kitabu) cha Mila za Kiyahudi:

Succah 29a Rabbi (Viongozi wa kiyahudi) wetu walifundisha, Pale jua liwapo kwenye kupatwa, ni dalili ya mkosi kwa dunia yote. Hili laweza kufafanuliwa na fumbo.

Hili laweza kulinganishwa na nini? Laweza kulinganishwa na mwanadamu aliyeandaa karamu kwa ajili ya watumishi wake na akawawekea taa. Na alipowakasirikia alimwambia mtumwa wake, ‘Waondolee taa, ili uwaache wakae gizani’. Ilielekezwa kwamba: R. Meir alisema, Kila pale mianga mikuu ya anga inapokuwa kwenye kupatwa, ni dalili ya mkosi kwa Israeli kwa kuwa wanaachwa wapate majanga. Hili laweza kufananishwa na mwalimu wa shule afikaye shuleni akiwa na fimbo mkononi. Ni nani apataye hofu? Ni yeye aliyezoea kila mara kuadhibiwa. Rabbi wetu walifundisha, Pale jua liwapo kwenye kupatwa ni ishara ya mkosi kwa waabudu sanamu; pale mwezi unapopatwa, ni ishara ya mkosi kwa Israeli, kwa kuwa Israeli hutumia mwezi kuhesabu siku na waabudu sanamu hutumia jua. Endapo kupatwa kunatokea wakati jua ama mwezi uko mashariki, ni ishara ya mkosi kwa wale waishio mashariki; na endapo viko magharibi, ni ishara ya mkosi kwao waishio magharibi; Endapo hayo yanatokea jua ama mwezi vikiwa utosini mwa anga ni ishara ya mkosi kwa ulimwengu wote. Ikiwa muonekano wake ni mwekundu kama damu, [ni ishara kwamba] upanga unawajia katika ulimwengu; ikiwa ni mweusi kama gunia la singa, mishale ya njaa inaijia dunia; na endapo inafanana na vyote, basi upanga na njaa vyote vinakuja kwa ulimwengu. Ikiwa kupatwa kunatokea wakati wa jua kuzama inaashiria majanga yatachelewa katika kuwafikia; ikiwa ni wakati wa mapambazuko, inaashiria majanga yanawajia kwa kasi na upesi: lakini baadhi hudai itokeapo hivyo basi ufafanuzi sharti ugeuzwe. Na hakuna taifa ambalo hushambuliwa ambapo miungu yake haishambuliwi pamoja nao, sawa na ilivyosemwa, Na dhidi ya miungu yote ya Misri nitatoa hukumu.

Ijapokuwa hii ni mila ya Kiyahudi, inatakiwa ieleweke kwamba ni jadi tu. Pamoja na kwamba ziko ishara ambazo Yesu aliziaminisha, Biblia inakemea mafanuzi kadhaa za ishara za mikosi (Torati 18:10-11). Vilevile, kumbuka kwamba Yesu wakati mwingine aliwakemea Wayahudi ambao waliamini kuwa mila zao zilikuwa juu ya kile inachofundisha Biblia:

“9Naye akawaambia, “Vema, mnazikataa amri za Mungu ili mpate kuzishika desturi zenu! 10Kwa mfano, Musa alisema, ‘Waheshimu baba yako na mama yako’ na ‘Ye yote amtukanaye baba yake au mama yake auwawe’”. (Marko 7:9).

Hivyo, Wakristo wanapaswa kuwa waangalifu wasiziamini mila za Kiyahudi ama mafundisho mengine ikiwa hayapatani na Biblia. Hakukutokea vita vya dunia ama njaa kubwa kila ambapo kupatwa kulitokea kwa aina iendanayo na hayo, iwe ni miezi ya damu ama la.

Wengine wamedai kwamba kwa kuwa kulikuwa na mwezi wa damu mwaka 1967 (na baadhi ya miaka mingine) hilo linaonyesha kwamba matukio kadhaa yaliliathiri taifa la Israeli, ikiwemo vita vyao na waarabu; na hiyo yaonyesha kuwa kila kunapokuwa na mwezi wa damu dharula itatokea.

Sasa sipingi kwamba matukio yaliyoliathiri taifa la Israeli yalitukia mwaka 1967, kama vile, kwa mfano, vile Vita vya Siku 6 ambavyo nitukio la kihistoria. Pamoja na hilo, hii haimaanishi kwamba Yesu atarejea mwaka 2014 au 2015 ama hata Siku ya Bwana itanza ndani ya miaka hiyo.

Kwa upande mwingine, ninaamini inawezekana, japo si lazima, kwamba tutashudia matukio maalum yatakayoliandama taifa la Israeli kwenye mwaka 2014 au 2015.

Miezi Minne ya Damu Na John Hagee

Mwanzoni mwa makala hii nilimtaja John C. Hagee. Yeye ni mwanzilishi na Mchungaji Mkuu wa kanisa la Cornerstone Church la San Antonio, Texas, Marekani.

Katika video ya mwezi Disemba 2012 ya kwenye tovuti ya "YouTube" iitwayo Coming Four Blood Moons By John Hagee part 1 (Miezi Minne ya Damu Inayokuja Na John Hagee Sehemu ya 1), Ameonyesha matarajio ya "miezi ya damu" kutokea wakati wa Pasaka na Sikukuu ya Vibanda ya mwaka 2014 na 2015.

Baada ya kunukuu Yoeli 2:30-31 na Matendo 2:, John Hagee alisema: "Mungu... Anatuma ishara kwenye sayari dunia, lakini hatujazipokea wala kuelewa hilo."

John Hagee alisema Taasisi ya NASA imesema hayo yanakuja, Yoeli na Petro walisema yanakuja, na kwamba Mungu anatupa maonyo kupitia ishara kama hizi za miezi ya damu ya mwaka 2014 na 2015.

Haya ndiyo mchapishaji wake alichandika katika kitabu chake kilichochapishwa na Amazon kiitwacho: Four Blood Moons Something is About to Change (Miezi ya Damu Minne, Mambo Karibu Yatabadiriwa):

"...Kutakuwa na ishara katika jua, katika mwezi, na nyota... basi haya yaanzapo kutokea, changamkeni mkaviinue vichwa vyenu, kwani ukombozi wenu umekaribia." Luka 21:25a, 28.

Ni mara chache sana ambapo Maandiko, sayansi, na historia huenda pmoja, lakini kupitia video hii ya "Four Blood Moons" inaeleza kuwa vimeendana. Je, hizi ndizo "ishara" ambazo Mungu anazitaja kwenye Neno lake? Ikiwa ndizo zenyewe, zinamaanisha nini? Umuhimu wake wa kiunabii ni upi?

Katika kitabu hiki kilichojipatia umaarufu na kuuzika kwa kiwango kikubwa, mwandishi huyu ambaye ametangazwa na gazeti laq New York Times kuwa kitabu chake kinaongoza kwa mauzo, Pastor John Hagee, anafafanua uhusiano uliopo baina ya matukio haya yakimiujiza na unabii wa kibiblia —na juu ya hatima ya watu walio wateule wa Mungu na hatima ya mataifa ya ulimwengu.

Sawa na ilivyokuwa wakati wa enzi za kibiblia, Mungu

anaendesha...

Hapa kuna maoni toka kwa mchambuzi wa kitabu cha Hagee:

"Miezi Minne ya Damu: Mambo Karibu Yatabadiriwa" ni kitabu kinachotumia Maandiko toka Biblia, ubashiri wa NASA, pamoja na taarifa za kihistoria kuonyesha kufika kwa mwisho wa dunia – kama tujuavyo – yaweza kuwa u karibu kufika...

Hili lilipotokea kwa mara ya kwanza, ilikuwa mnamo 1493, miezi mine ya damu ilitokea kwenye Sikukuu za Kiebrania za Pasaka pamoja na Sikukuu ya Kuzipiga Baragumu. Pastor Hagee anaandika, "Hili liliashiria kuanguka kwa Hispania kufuatia kuwafukuza kwake Wayahudi mwaka mmoja kabla na ilikuwa ni tangazo toka kwa Mungu kwa dunia kwamba fimbo ya mafanikio ilikuwa sasa inahamia kwa taifa ambalo baadaye ndilo lilifanyika kuwa Marekani kwa kuwa ndilo liligeuka kuwa kimbilio la Wayahudi hao."

Safari ya pili ambapo miezi mine ya damu ilitokea kwenye sikukuu za Kiebrania ilikuwa mnamo 1949-1950. Ilitokea kwenye Pasakana kwenye Sikukuu ya Vibanda na siku iliyofuata Israeli ilitangazwa kauwa taifa.

Safari ya tatu ilitokea mnamo 1967-1968, wakati vita vya siku sita (The Six-Day War) vilipotokea, vikasababisha mji wa Yerusalemu uunganishwe kwa mara ya kwanza katika miaka 2,000, "tukio kuu sana kiunabii," kulingana na kitabu cha Hagee...

Mhubiri huyu ajulikanaye ulimwengu mzima anaendelea kueleza zaidi, "Hakuna swala la mwezi ama jua kupatwa kwa bahati mbaya; kila kitu cha angani kinaendesha na mkono usioonekana wa Mungu ili kutuletea ishara sisi wanadamu juu ya matukio yanayotujia."

Hagee anaamini kwamba Mungu atatumia miezi hii ya damu kutoa ishara kwamba anajiandaa kufanya mageuzi kwenye mwelekeo wa historia ya wanadamu. "Hakuna yeyote ajuaye mawazo ya Mungu lakini matarajio ya matukio haya yanatufahamisha kwamba kitu fulani kinaenda kutokea." (Exum R. Roy Exum: Rev. Hagee's 'Blood Moons'<http://www.chattanooga.com/2013/10/8/260792/Roy-Exum-Rev.-Hagees-Blood-Moons.aspx> viewed 10/09/13).

Kimsingi anachosema ni kwamba, Yesu anarudi hivi karibuni na hii miezi ya damu inatokea ili iweze kututaarifu kitu fulani.

Biblia haikubaliani kwamba kutokea kwa miezi hii ya damu ni fundisho kuwa Yesu anaenda kurudi au Siku ya Bwana itanza katika mwaka 2014 au 2015.

Nitawezaje kuwa na uhakika?

Sababu Yesu aliorodhesha matukio ya aina mbalimbali yatakayotangulia kabla ya kurudi kwake na matukio ya jua na mwezi katika Mathayo 24, hayawezi kutokea kabla ya mwishoni mwa 2015. Zaidi, makubaliano ya miaka saba ya Danieli 9:27

bado hayajafanyika kufikia siku hii ninapoandika makala hii. Jisomee:

“27 Naye atafanya agano na wengi kwa muda wa juma moja; Na katikati ya juma ataikomesha sadaka ya kuteketezwa na dhabihu. Na mahala pake atasimamisha chukizo la uharibifu, hadi mwisho ulioamuriwa utakapomiminwa juu yake yeye aletaye uharibifu” (Danieli 9:27).

Kwa vile makubaliano haya bado hayajafanyika, basi anagalao bado kuna miaka hiyo saba kabla Yesu arejee. Kwa vile makubaliano hayo yanatakiwa yavunjike baada ya kufika katikati yake, basi angalau bado kuna miaka takribani 3 1/2 kabla ya kuanza kwa Dhiki Kuu (Mathayo 24:15-21; Danieli 11:31).

Hivyo, muda ambao Yesu harejei, Dhiki Kuu nayo haiwezi kuanza, na Siku ya Bwana haitanza katika mwaka 2014 wala 2015, baadhi ya watu cha kusikitisha waweza kutumia makosa ya akina John Hagee kudanganya kwamba nabii mbalimbali za kwenye Maandiko haziwezi kutimia.

Lakini, hatupaswi kusahau kuwa liko: “19.... neno la hakika zaidi la unabii, ambalo mtafanya vema mkilishika kwa bidii,” (2 Petro 1:19)—ni ukweli wazi tu kwamba si John Hagee wala Mark Biltz ambao wanalo kwa ukweli.

Mark Biltz na Miezi ya Damu

Katika mwaka 2008, Gazeti la World News Daily liliandika kifuatacho:

Mchungaji ambaye huhubiri juu ya Ukristo uliojikita kwenye kushika Agano la Kale amedai kutokea kwa mfuatano nadra wa kupatwa kwa jua na miezi kunakotarajiwa kutokea kwenye sikukuu takatifu miaka saba tangia sasa, kunaweza kuwa ni tangazo la kile kinachojulikana kuwa ni “Kurudi kwa Mara ya Pili” kwa Yesu.

“Mungu anatutaka tuiangalie kalenda ya kibiblia”, anadai Mark Biltz, mchungaji wa El Shaddai Ministries iliyoko Bonney Lake, Washington, Marekani. “Sababu itufanyayo tulazimike kufuatilia ni [kwasababu] Kristo atatoa ishara ya kurejea kwake. Lakini inatupasa tujue ni kipi tunachotakiwa kukifuatilia pia. Hivyo tunatakiwa tuziangalie na kuzifuatilia sikukuu za kibiblia”...

Biltz alianza kufuatilia utimilifu wa nyakati pale jua na miezi itakapopatwa, ambayo pia wakati mwingine huitwa “miezi ya damu” kwa vile mwezi hugeuka na kuwa wa rangi kama damu. Aliingia kwenye tovuti ya taasisi ya mambo ya anga ya Marekani iitwayo NASA kwenye kipengele cha jua na mwezi kupatwa ambayo inaorodhesha nyakati, siku, miezi na miaka ya matukio ya angani.

Akiwa kwenye tovuti hiyo aliona kitu kisicho cha kawaida cha mifuatano mine ya mwezi wote kupatwa, kujulikanako kisayansi kama “tetrad”. (Blood moon eclipses: 2nd

Coming in 2015? Minister uses NASA forecasting to study signals of Jesus’ return WorldNetDaily – April 30, 2008. <http://www.worldnetdaily.com/index.php?fa=PAGE.view&pageId=63076>).

Hivyo, kulitolewa madai kwamba Yesu angeweza kurejea mwaka 2015 kutokana na mahesabu ya matukio haya ya miezi ya damu ambayo Mark Biltz aliyafanyia utafiti. Pamoja na ukweli kwamba Mungu anatutaka tuitumie kalenda yake, ni ukweli kuwa Mark Biltz haelewi sawasawa, na wala Yesu hawezi kurejea mwaka 2015.

Kanisa Kunyakuliwa Wakati wa Mwezi Mwekundu?

Wengine wanaamini kwamba Yesu atakuja ‘kulinyakua kanisa’ punde tu kabla au baada ya kutokea kwa mwezi mwekundu.

Na pamoja na ukweli kwamba Yesu atarejea baada ya mwezi wa damu ambao Biblia inautaja katika Yoeli 2 na Ufunuo 6, bado kurudi kwa Yesu Kristo hakuwezi kutokea hadi kwanza Dhiki Kuu itokee. Ebu fuatilia maelezo yake toka Injili ya Mathayo:

3 Hata alipokuwa ameketi kwenye Mlima wa Mizeituni, wanafunzi wake wakamwendea kwa faragha, wakisema, “Tuambie, mambo hayo yatakuwa lini? Nayo ni nini dalili ya kuja kwako, na ya mwisho wa dunia?”

4 Yesu akajibu akawaambia: “Angalieni mtu asiwadanganye...”

15 “Basi hapo mtakapo liona ‘chukizo la uharibifu’, lile lililonenwa na nabii Danieli, limesimama katika patakatifu” (asomaye na afahamu), 16 “ndipo walio katika Uyahudi na wakimbilie milimani; 17 naye aliye juu ya dari asishuku kuvichukua vitu vilivyomo nyumbani mwake; 18 wala aliye shambani asirudi nyumbani kuichukua nguo yake.. 19 Ole wao wenye mimba na wanyonyeshao siku hizo! 20 Ombeni ili kukimbia kwenu kusiwe majira ya baridi au siku ya Sabato. 21 Kwa kuwa wakati huo kutakuweco dhiki kubwa, ambayo haijatokea namna yake tangu mwanzo wa ulimwengu hata sasa, wala haitakuwako kamwe...”

29 “Lakini mara, baada ya dhiki ya siku zile, jua litatiwa giza, na mwezi hautatoa mwanga wake, na nyota zitaanguka mbinguni, na nguvu za mbinguni zitatikisika. 30 Ndipo itakapoonekana ishara yake Mwana wa Adamu mbinguni; ndipo mataifa yote ya ulimwengu watakapoomboleza, nao watamwona Mwana wa Adamu akija juu ya wawingu ya mbinguni pamoja na nguvu na utukufu mwingi. 31 Naye atawatuma malaika zake pamoja na sauti kuu ya parapanda, nao watawakusanya wateule wake toka pepo nne, toka mwisho huu wa mbingu mpaka mwisho huu” (Mathayo 24:3, 4, 15-21, 29-31).

Wengi waliwahi kudanganywa huko nyuma kuhusu kurudi

kwake Yesu na wengi pia wanaendelea kudanganywa kwa sasa. Yesu atarejea baada ya sauti kuu ya parapanda (tarumbeta) si kuja kulinyakua kanisa kama wengi wadhaniavyo bali Wakristo watakusanyika mbele yake kutoka pande zote za dunia (1 Wathesalonike 4:16-17). Pamoja na hili kuwa ni faraja kwa Wakristo, Yesu hatarejea mwaka 2014 wala 2015. Wote watarajiao kunyakuliwa ama Kristo kurudi katika mwaka 2014 au 2015 watarajie kukatishwa tamaa pale hilo litakaposhindikana kutimia!

Wale waaminio kinyume na hili wamepotoshwa. Yesu hata hivyo, atarejea siku fulani. Sisi tulio miongoni mwa wale waaminio juu ya “Neno hakika la unabii” (2 Petro 1:19) tunalitambua hilo. Lakini wale ambao wanawategemea wahubiri wa Kiprostanti watumainiao mila na historia wanashindwa kufuatilia kweli nyingi pamoja na mafundisho ya Biblia.

Maoni ya Mwisho juu ya Miezi ya Damu

Lipo jambo lijulikanalo kama mwezi wa damu. Ni tulio ambalo limejitokeza mara kadhaa kwa karne nyingi na bado linatarajiwa kutukia tena. Kama ambavyo ingetarajiwa, baadhi ya matukio ya kihistoria nayo yametokea miakai ileile miezi hii ya damu inapotokea, lakini hili halithibitishi kwamba miezi yote miekundu ni matukio ya kiunabii.

Taasisi ya NASA inajua kwa uhakika kuhusu miezi miekundu itakayotokea mwaka 2014 na 2015. Baadhi yake yaweza hata kuendana na tarehe za maswala ya kibiblia.

Biblia imeongelea kuhusu wakati mwezi utageuka mwekundu kama damu punde tu kabla ya Siku ya Bwana, ambayo pia ni punde kabla Yesu Kristo hajarejea.

Miezi hii ya damu inayotegemewa itokee mwaka 2014 na 2015, hata hivyo, matukio haya ni yale yanayoendana na mzunguko wa kawaida wa sayari katika anga na wala hayaelezi chochote kuhusiana na kurejea kwa Yesu Kristo, kunyakuliwa kwa namna yoyote, wala Siku ya Bwana kutokea mwaka 2014 au 2015.

- Makubaliano ambayo yatatimizwa kwa miaka saba ya Danieli 9:27 bado hayajatimizwa kufikia Octoba 2013, hivyo angalao miaka 3 1/2 bado iko mbele kabla makubaliano hayo hayajavunjwa.
- Chukizo la Uharibifu ambalo Yesu alilitaja kuwa lilinenwa na Danieli kwamba lingesimama Mahali Patakatifu, nalo bado halijatokea. Na hilo haliwezi kutokea hadi kwanza mkataba wa Daniel 9:27 uvunjwe.
- Dhiki Kuu aliyofundisha Yesu katika Mathayo 24:21 bado haijaanza.
- Muhuri wa Tano wa Ufunuo 6:9 bado haujafunguliwa.
- Yesu atarejea, lakini si mwaka 2014 wala 2015 kwani miaka hiyo ni mapema mno kuwezesha yote yaliyotabiriwa kutokea kabla ya siku ya mwisho kutimia, maana ishara nyingi zitakiwazo kutangulia bado hazijatukia.

Ijapokuwa kutakuwepo matukio ya kiunabii yatakayotukia katika miaka hiyo, Yesu hatorejea katika mwaka 2014 au 2015. Dhiki Kuu haiwezi kuanza mwaka 2014 au 2015. “Siku ya Bwana” ya mwisho haitaanza mwaka 2014 au 2015.

Kozi ya Kujifunza Biblia

SOMO LA I: KWANINI TUJIFUNZE BIBLIA?



Mwandishi: Bob Thiel

Published 2014 by the Continuing Church of God

Utangulizi: Kozi hii imetokana na kozi ya awaliiliyoitwa “Kozi ya Biblia kwa Mawasiliano” iliyoandaliwa mwaka 1954. Iliyoanzishwa chini ya uangalizi wa marehemu C. Paul Meredith enzi za Radio Church of God. Vipengele kadhaa vimeboreshwa viendane na karne ya 21(japo mengi ya mafundisho ya awali hayakubadirishwa). Pia imeongezewa aya za Kimaandiko, pamoja na taarifa na maswali ambayo hayakuwemo kwenye kozi ya awali.

Kwa nini Tujifunze Biblia?

KWA NINI TUHITAJI kujifunza Biblia katika karne hii ya 21? Biblia ni nini? Tunapaswa tujifunze namna gani, ili tuweze kuelewa? Katika mwanzo kabisa wa kozi hii tunahitaji kujiuliza maswali haya na kuyajibu.

Biblia inafundisha: “JIFUNZE KWA BIDII KUJIONYESHA KWA MUNGU KUWA UMEKUBALIWA NA YEYE” (2 Timotheo 2:15) and “Jifunze kutenda mema” (Isaya 1: 17). Hivyo, Wakristo wanapaswa kujifunza kwa kuwa Maandiko yamewaagiza hivyo.

LAKINI ni kwa nini tuhitaji kujifunza na kukubaliwa na Mungu? Na huku kujifunza kunahitaji kuwe ni WAJIBU wa kuchosha na usio wa kuisimua ambao tunajilazimisha kuufanya sababu

ya kumtii mungu mkali-ama kujifunza huku kunatakiwa kuwe kwa KUBURUDISHA, kuwe kwa KUCHANGAMSHA na kwa KUFURAHIA kuletako FAIDA kuliko tulivyowahi kuona katika uhai wetu?

KWANINI kwa walio wengi kujifunza Biblia ni jukumu la kuchosha, lisilo na msimko, lililojaa mateso-lifanywalo, kwa vile tu ni wajibu na kutokana na kumwogopa Mungu katili?

Ni kwa vile tu walio wengi HAWAJAMJUA Mungu, wala ni wa namna gani- na ni kwa sababu bado hawajaanza KUIELEWA Biblia kiukweli!

Kwanini tujifunze Biblia?

Ziko sababu nyingi.

Wanadamu bila ya Mungu wanajipeleka kwenye uangamizi wa sayari hii kwa vile wamejitenga na Muumba wao Mungu (Mathayo 24:22). Ni watu wachache tu wanalielewa hili kwa usahihi, na kile Mtume Petro alichosema, kwamba Yesu ndiye “aliye na maneno ya uzima wa milele” (Yohana 6:68).

Sehemu muhimu mbalimbali za Biblia ziliandikwa zikiwa na maneno yaliyotamkwa moja kwa moja na Yesu mwenyewe pale alipotembea hapa duniani akiwa katika mwili (Mfano: Mathayo, Marko, Luka, na Yohana), na maeneo mengine yaliandikwa ili tuweze kujua kile ambacho yeye alikifundisha na jinsi gani tunapaswa kuishi (mfano: 1 Wakorintho 1:11; Methali 1:1-7).

Fahamu pia:

“16 Kila andiko, lililovuviwa na Mungu lafaa kwa mafundisho, kwa kuwaonya watu makosa yao, kuwaongoza na kuwafundisha katika haki; 17 ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila kazi njema” (2 Timotheo 3:16-17).

Ikiwa kweli unahitaji kuwa mfuasi wa Yesu, na uwe umekamilika, unahitaji kujifunza na kuyapokea maelekezo, uwe tayari kusahihishwa, na kuonywa kutokana na kile Biblia ilichonacho. Ukweli ni kwamba wengi wanaodai kuwa ni Wakristo na kudai kuwa Biblia ndiyo msingi halisi wa imani yao, wanashika zaidi mila za wanadamu, kuliko imani ya Biblia.

Katika masomo haya tutakuja kufikia kutambua kwamba Mungu kweli ni UPENDO (1 Yohana 4:8, 16) — siyo Mungu katili, wala mkali. Mungu anamtakia kila mmoja wetu awe na furaha, na AYAFURAHIE maisha kwa kiwango kamili, na kuyafanya maisha ya kuisimua. Sheria ya Mungu inaonyesha upendo (Marko 12:28-33; Yakobo 2:8) na ni njia iongozayo kutupeleka kwenye uzima (Torati 10:13; 30:19). Na pale TUTAKAPOANZA kuelewa Biblia, tutaikuta kumbe ni ya KUISISIMUA, ni yenye mvuto na pia ni yenye MANUFAA na ya kupendeza kuliko vyote.

Pale mtakapozama ndani ya Masomo haya, wengi wenu mtafurahia sana kujifunza huku kiasi kwamba hamtapenda kuchelewa kupokea somo linalofuata. Mtakuta kwamba vivutio na michezo ya kidunia SI BURUDANI, si YAKUFURAHISHA, si

ya KURIDHISHA kiroho! Kwa sababu Mungu ni UPENDO, yeye ni mwumbaji wako akupendaye, na anahitaji wewe uwe na furaha na afya na mwenye mafanikio kupitia Biblia. Ni kupitia kwa NENO LAKE ndiyo hutumia kufunua kwako NJIA ya kutoka kwenye ukiwa, woga na mashaka, maradhi na magonjwa, umaskini na uhitaji, maisha matupu na yasiyo ya kuridhisha, na kukupeleka kwenye maisha ya furaha, afya, na mafanikio TELE ambayo atakupa uyamiliki na kuyafurahia milele!

Tunapaswa kuelewa, kabla hata hatujaanza kujifunza Biblia yenyewe, kwamba SHARTI la kufikia uelewa sahihi ni KUJITOA kikamilifu katika utii kwa mafundisho yake, sheria zake na maelekezo. Yesu alisema tunatakiwa TUISHI kwayo (Mathayo 4:4) – sharti tujifunze ili kwamba kila tufanyalo tuhakikishe linaendana na maelekezo ya Biblia. Ndiyo kiongozi wetu katika maisha – iwe ni katika biashara, jamii na mahusiano ya kisiasa, yawe ni maisha ya kielimu ama ya kidini. Mungu anatufundisha TUJIFUNZE Biblia: “uonekane unakubalika kwa Mungu” (2 Timotheo 2:15). Yule ambaye hajifunzi kwa lengo hili – ambaye hajayatoa maisha yake kikamilifu kwa Mungu ili kwamba Mungu ayatawale maisha yake, huyo HAWEZI kuelewa Biblia, hata kama atajitahidi kiasi gani.

Ni kweli kabisa kwamba: “uelewa mzuri wanao wale wazishikao amri zake” (Zaburi 111:10) – na ni wale tu – ambao hawatamtii Mungu ndio ambao huwa hawapati uelewa sahihi! Na ni ndani ya Biblia ndiko ambako Amri zake zimetajwa na kufafanuliwa.

Tunaamini kwamba kozi hii ya Biblia itakuwa ya maana zaidi kwako endapo utaelewa uhusiano wake muhimu kwa maisha yako na matukio ambayo yanatokea duniani. Uhusiano wake wa moja kwa moja na MATUKIO unayoyasoma kila siku kwenye magazeti, unayoyasikia radioni na kuyaona kwenye TV, ama hata kuyakuta kwenye internet. Ili kuelewa ni wapi mengi ya matukio haya yatatupeleka, ni lazima tuelewe, kwanza, kwamba INJILI YA YESU ilikuwa ni UJUMBE wa kimungu uliotumwa TOKA KWA MUNGU KWA WANADAMU – ujumbe wa MPANGO WA MUNGU UNAOTEKELEZWA HAPA DUNIANI – uhusuo MWISHO WA ULIMWENGU HUU, na KUJA KWA UFALME WA MUNGU – ULIMWENGU WA KESHO utakaotimia hivi karibuni!

Endapo ungeifungua na kujaribu kuelewa ramani ya dunia, isingeeleweka vema kwako, hadi kwanza pale utakapopapata na kuweka kidole chako kwenye eneo sahihi la ramani hiyo paonyeshapo pale ulipo kwa wakati huo, na kisha ndipo ungeweza kuelewa vema maeneo mengine ya dunia, kulingana na yaliko kutokea kwenye eneo lako kwenye ramani hiyo, na ndipo kila eneo kwenye ramani litakapoeleweka. Sisi tunaamini utaweza kuelewa Biblia vema zaidi, na kuikuta ni ya kuisimua, ikiwa utaitafakari yote – historia yake na unabii wake – mafundisho na mafunuo yake matakatiifu – kutokea kwenye kilele cha mtazamo utokanao na maisha yako. Ikiwemo, jinsi ulimwengu huu umejiendesha kufikia nyakati hizi zilizopo, na hali iliyopo, ambamo unaishi – ni wapi inaelekea kwenda baada ya hapa. Utaikuta hii ni ya kuisimua zaidi na ni ya kuburudisha zaidi, na ni MUHIMU zaidi ya yote katika maisha yako endapo utajituma na KUJIFUNZA hasa!

KUMBUKA: Hii Kozi ya Kujifunza Biblia ni Kozi ya KUJISOMEA BIBLIA. Siyo kitu ambacho unasoma tu harakaharaka. Kile tumekuandikia ni mwongozo tu wa kukusaidia UJIFUNZE BIBLIA. Kitu muhimu katika kozi hii ni kitabu cha BIBLIA! Daima hakikisha unayo Biblia yako pembeni yako kila uketipo kujisomea kozi hii. Ili ujifunze mengi toka kozi hii, jitahidi kukisoma kila kifungu cha maandiko kilichotajwa kuendana na kipengele unachosoma, siyo maandiko peke yake yale yaliyotajwa kujibu swali lililoulizwa katika mwisho wa kila somo. Yachunguze Maandiko ili ujihakikishie ikiwa yale unayofundishwa ni ya kweli (Matendo 17:11).

Unaishi katika Dunia ndani ya Machafuko!

Wengi leo wamejaa hofu, wakati wengine wamekata tamaa.

Hata wachambuzi wa maswala wengi leo wanalitambua hili kuwa kuna kitu kisichosawa kwenye ulimwengu huu. Wataletaje amani ya ulimwengu? Yapo mapendekezo kadhaa toka kwa wanadamu, lakini yote, yako kinyume na Mungu, na hivyo hayatafanikiwa (Warumi 3:17-18).

Wanasayansi wengi pamoja na wengine kwa ujumla wanasema wazi kwamba hadi tuwe na SERKALI YA ULIMWENGU mapema kuanzia sasa vinginevyo silaha kali za maangamizi zitafuta uhai wote toka duniani. Lakini sasa YAMESHINDWA KUFIKIA KWA AMANI, UUNDWAJI WA SERKALI YA ULIMWENGU! Umoja wa Mataifa, Mikutano ya Hague, Mkatoba wa Paris, Kikao cha Berchtesgaden, Munich, Teheran, Yalta, pamoja na Potsdam vyote vilishindwa kuleta amani. Hata na Baraza la Usalama la Umoja wa mataifa wala Marekani nayo imeshindwa (pamoja na jitihada za kuunda “Pax Americana”).

Kutokana na mabomu ya atomic na mabomu ya hydrogen, mabomu ya neutron, silaha za kemikali, silaha za kibayolojia, silaha za electro-magnetic pulse, pamoja na silaha zingine za teknolojia ya juu ambazo kwa sasa hazijulikani kwa walio wengi (ukichanganya na silaha zitakazozidi kuvumbuliwa na zinazoendelea kuundwa kwa sasa), wanadamu tunazidi kukaribia zaidi kwenye kipindi ambacho Yesu alituonya takribani miaka 2,000 iliyopita kuwa kingekuja, ambapo: “endapo Bwana hatazifupisha siku hizo, hataokolewa mtu akingali hai” (Marko 13:18).

Hakuna mwanadamu wala mnyama, samaki wala ndege ambaye angeepuka kuangamizwa na silaha hizi.

Ndiyo, ustaarabu wa ulimwengu huu umefikia kwenye JANGA! Je, uharibifu na uangamifu huo mbaya utokanao na hizo silaha utawafanya wanadamu wajuziue kuzitumia japo ziko mikononi mwa makundi ya vichaa wenye tamaa ya madaraka? Hilo halijawahi kuwazuia kutumia silaha hizo za maangamizi huko nyuma pale walipoona muda wa kufanya hivyo ulikuwa umewadia! Hata silaha za kemikali ambazo zimepigwa marufuku kidunia zinazoendelea kutengenezwa na wengine hata wanazitumia kuuwa wengi. MUDA WA KUTAFAKARI NA KUAMUA UMEWADIA! Wanadamu wanaonyesha wazi kuwa

HAWANA KABISA uwezo wa kujitawala na kujiongoza wao wenyewe. Kwa kawaida, ukichaa wa kiongozi atakaye madaraka zaidi huishia pale tu yeye auawapo au kufariki—lakini sasa kila huyo aondokapo, viongozi wengine vichaa huibuka kuchukua sehemu yake kana kwamba walikuwa kwenye maandalizi na hivyo mbio za kuelekea kwenye uharibifu na uangamivu huzidi kusonga mbele!

Jibu ni nini?

MWANADAMU ATAANGAMIZANA MWENYEWE TOKA USO WA DUNIA, ENDAPO ATAACHIWA AENDELEE PASIPO MUNGU KUIINGILIA KATI (Ufunuo 11:18)!

Wakati wengi wanatamani kuupuuza unabii na hawaamini juu ya zama hizi kufikia mwisho hivi karibuni, somo hili lilikuwa muhimu mno kwa Yesu kiasi kwamba alijibu maswali ya wanafunzi wake kuhusu hili:

“3 Hata alipokuwa ameketi kwenye Mlima wa Mizeituni, wanafunzi wake wakamwendea kwa faragha, wakisema, ‘Tuambie, mambo hayo yatakuwa lini? Nayoye ni nini dalili ya kuja kwako, na ya mwisho wa zama?’

4 Yesu akajibu na kuwaambia: ‘Angalieni mtu asiwadanganye. 5 Kwa sababu wengi watakuja kwa jina langu, wakisema, ‘Mimi ni Kristo’, nao watadanganya wengi. 6 Nanyi mtasikia habari za vita na tetesi za vita. Angalieni msitishwe; maana hayo hayana budi kutukia, lakini ule mwisho bado. 7 Kwa maana taifa litaondoka kupigana na taifa, na ufalme kupigana na ufalme. Kutakuwa na njaa, maradhi na matetemeko ya ardhi mahali mahali. 8 Haya yote ndiyo mwanzo wa utungu’” (Mathayo 24:3-8).

Yaonekana tuko katika nyakati ambazo Yesu alizitaja kuwa ndizo “mwanzo wa utungu” (Mathayo 24:8, Marko 13:8). Na kamwe hazitafuatiwa na nyakati njema kwa kuwa: “Kwa kuwa wakati huo kutakuweco dhiki Kubwa, ambayo haijatokea namna yake tangu mwanzo wa ulimwengu hata sasa, wala haitakuwapo kamwe. Na kama siku hizo zisingalifupizwa, asingaliokoka mtu yeyote; lakini kwa ajili ya wateule siku hizo zitafupishwa” (Mathayo 24:21-22).

Iwapo hatuwezi kujiponya sisi wenyewe, NI NANI AWEZAYE KUTUOKOA? JIBU la swali linatoka kwa yule ambaye ndiye neno lake limejaribiwa kwa zaidi ya mamia ya nyakati kupitia matukio yaliyokuwa yametabiriwa na Manabii wake, matukio ambayo yote yalitimia.

Huyu alikuwa ni nani? Yesu (Marko 13:20). Hatutakiwi kumwamini yeye pekee, bali tunatakiwa pia kuyaamini na yale aliyoyasema na kudumu ndani ya maelekezo yake (Yohana 8:31).

Kile alichokisema kuwa kinatakiwa kikuamusha wewe na mimi na kila mmoja wetu ni – “Wakati ni mfupi sana!” Ni dhahiri hautakuwa ukipoteza muda wako wakati utakapojifunza masomo ya kozi hii. Badala yake, utaJIFUNZA NJIA PEKEE

ITAKAYOKUWEZESHA kujua MATUKIO MAKUU YAJAYO HIVI KARIBUNI. Utajipatia elimu ambayo itakuweka katika furaha kuu hapo baadaye. Jitihada zako katika hili zitakulipa maradufu kuliko chochote ambacho umewahi kutekeleza huko nyuma! Hivyo weka jitihada zako zote katika kujisomea masomo haya. Jinsi unavyoyasoma yaweza kuwa na matukio juu ya maisha yako ya baadaye na hususani juu ya sehemu yako katika maisha yajayo.

KWANINI Mungu Sharti Aingilie Maswala ya Ulimwengu

Wenye hekima WENGI, wasomi wa kiume na wa kike wanadhihaki wazo kwamba Yesu Kristo yu karibu kurejea. Hawaoni mantiki yoyote juu wazo hilo! Yawezekana hata wewe mwenyewe umewahi kuwafahamu watu wa aina hiyo, ama sivyo?

Katika karne ya 21, umbumbumbu wa Biblia na dhihaka waonekana kuongezeka sawa na Mtume Petro alivyotabiri kuwa hilo lingetokea wakati wa siku za mwisho (2 Petro 3:3-4).

Hawa ni matokeo halisi ya kizazi ambacho kimepoteza mtazamo wa ukweli wa kuwepo Mungu. Hudhihaki na kulipinga neno la Mungu ambalo hasa ndilo “neno la ukweli” (2 Wakorintho 6:7).

Jionee yafuatayo toka Kitabu cha Methali:

“7 Kumcha BWANA ndio mwanzo wa maarifa, Bali wajinga hudharau hekima na maelekezo” (Methali 1:7).

“29 Kwa kuwa walichukua maarifa wala hawakuchagua kumcha Bwana, 30 Hawakukubali maelekezo yangu wakayadharau maonyo yangu yote. 31 Kwa hiyo watakuwa matunda ya njia yao, na watashiba mashauri yao wenyewe. 32 Maana kurudi nyuma kwao wajinga kutawaua, na kufanikiwa kwao wapumbavu kutawaangamiza” (Methali 1:29-32).

“19 Maana hekima ya ulimwengu huu ni upuuzi mbele za Mungu. Kwa maana imeandikwa, ‘Yeye ndiye awanasaye wenye hekima katika hila zao’; 20 na tena, ‘Bwana anayafahamu mawazo ya wenye hekima, ya kwamba ni ya ubatili’. 21 Basi, mtu yeyote asijivunie wanadamu” (1 Wakorintho 3:19-21).

Kizazi cha zama hizi kinajidai kuwa ndicho kilichoelimika zaidi, chenye majiji bora zaidi na chenye “werevu wa kidunia” kuliko wote waliowahi kuishi – lakini ndicho ambacho kimepoteza kabisa mwelekeo wa msingi wa elimu yote: Sisi ni nani, kwa nini tupo, KUSUDI la mwanadamu kuwepo ni nini! Iwapo hawa wasomi na wengine wote wangejua majibu kwa maswali haya, wangejua maana halisi ya SABABU na kwa kweli UMUHIMU HALISI – wa kurejea upesi – kwa Yesu Kristo kuja kuitawala dunia hii.

Lakini kwa vile ni wachache tu ndio wafahamuo, walio wengi wataangamia (Mathayo 24:24).

Machafuko ya Ulimwengu HAYAKWEPEKI!

Pamoja na jitihada za dharti kujaribu kuleta amani inayodumu – VITA KAMILI inazidi kutusogelea. Kuibuka kwa bomu la hydrogen – uwezekano wa KUANGAMIZWA DUNIA NZIMA sasa ni kitu halisi! Japo tumeonywa kwamba jibu pekee ni kuwepo kwa SERKALI YA ULIMWENGU—jitahada za kibinadamu za kufikia azima hii ZOTE ZIMESHINDWA VIBAYA.

Wanasiasa na wanasayansi mbalimbali wameanza kutambua hili linamaanisha nini. Baadhi wanaanza kuogopa! Ukweli wazi na wa kutisha ni kwamba WANADAMU TAYARI WAMESHAFIKA MWISHO WA KAMBA YAO. Wanadamu wamefikia pale ambapo hawawezi tena kujilinda wao wenyewe dhidi ya silaha za kuogofya walizojitengenezea wao wenyewe. KUNINGILIA KATI KWA MAMLAKA YA JUU NDIYO NJIA PEKEE TULIYONAYO KWA MAOVU YA ULIMWENGU HUU.

Wakati Yesu alipokuwa hapa duniani, alifahamu ni wapi ubunifu wa wanadamu ungewafikisha wakati wa miaka ijayo. Yesu alijua kuwa katika wakati huu wa mwisho watu wangekuwa wakipapasa gizani kuitafuta njia ya kufikia amani, lakini kwa kweli wangeishia kwenye ukingo wa kuuangamiza uhai wote: “Kama siku hizo zisingalifupishwa, asingaliokoka (asingalibaki hai) mtu yeyote,” Kristo alionya (Mathayo 24:22).

Chanzo cha Majanga ya Ulimwengu

Katika unabii huu wa kustaajabisha, Yesu pia anatupa ufunguo juu ya KWANINI ulimwengu wetu wa sasa uko katika hali mbaya. Alionya: “Lakini kama ilivyokuwa siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa wakati wa kuja kwake Mwana wa Adamu” (Mathayo 24:37).

Ni kipi walichokuwa wakifanya wanadamu enzi za Nuhu maelfu ya miaka iliyopita, ambacho kiliwasababishia waishie kwenye uangamifu mkubwa?

Ifungue Biblia yako kwenye Mwanzo 6:12-13 ambako ndiko tunalikuta jibu: “Mungu akaiangalia dunia, na tazama imepotoka; maana kila mwenye mwili amejiharibia njia yake duniani. Mungu akasema... wameijaza dunia dhuluma.”

Wanadamu wa asili wametumia fikra zao za kibinadamu na kuondoka toka njia ya maisha ambayo Mungu aliwapa hapo mwanzo. Mabadiriko haya ya kuiacha NJIA ya Mungu na kugeukia KIKRA ZA KIBINADAMU POTOFU ndicho kinachotishia kuangamia kwa ulimwengu. Yesu alisema hali hiyohiyo ndiyo itakayokuwa imeshamiri punde tu kabla ya kuja kwake mara ya pili.

Ebu uangalie ulimwengu huu unaokuzunguka.

Jionee kile ambacho Mtume Paulo alivuviwa kuandika:

“18Ghadhabu ya Mungu imedhihirishwa kutoka mbinguni dhidi ya uasi wote na uovu wa wanadamu ambao huipinga kweli kwa uovu wao, 19kwa maana yote yanayoweza

kujulikana kumhusu Mungu ni dhahiri kwao, kwa sababu Mungu mwenyewe ameliweka wazi kwao. 20Kwa maana tangu kuumbwa kwa ulimwengu, asili ya Mungu asiyeonekana kwa macho, yaani, uwezo Wake wa milele na asili Yake ya Uungu, umeonekana waziwazi ukitambuliwa kutokana na yale aliyoyafanya ili wanadamu wasiwe na udhuru.

21Kwa maana ingawa walimjua Mungu, hawakumtukuza Yeye kama ndiye Mungu wala hawakumshukuru, bali fikira zao zimekuwa batili na mioyo yao ya ujinga ikatiwa giza. 22Ingawa wakijidai kuwa wenye hekima, wakawa wajinga 23na kubadili utukufu wa Mungu aishiye milele kwa sanamu zilizofanywa zifanane na mwanadamu ambaye hufa, ndege, wanyama na viumbe vitambaavyo.

24Kwa hiyo, Mungu akawaacha wazifuate tamaa mbaya za mioyo yao katika uasherati, hata wakavunjiana heshima miili yao wao kwa wao. 25Kwa sababu waliabadili kweli ya Mungu kuwa uongo, wakaabudu na kutumikia kiumbe badala ya Mwumba, ahimidiwaye milele! Amen.

26Kwa sababu hii, Mungu aliwaacha wavunjiane heshima kwa kufuata tamaa zao za aibu. Hata wanawake wao wakabadili matumizi ya asili ya miili yao wakaitumia isivyokusudiwa. 27Vivyo hivyo wanaume pia wakiacha matumizi ya asili ya wanawake wakawakiana tamaa wao kwa wao. Wanaume wakafanyiana matendo ya aibu na wanaume wengine nao wakapata katika maisha yao adhabu iliyowastahili kwa ajili ya upotovu wao.

28Nao kwa kuwa walikataa kumkubali Mungu, Yeye akawaacha wafuate akili zao za upotovu, watende mambo yale yasiyostahili kutendwa. 29 Wakiwa wamejawa na udhalimu wa kila namna, uasherati, uovu, tamaa mbaya na hila. Wamejawa na husuda, uuaji, ugomvi, udanganyifu, hadaa na nia mbaya. Wao pia ni wasengenyaji, 30wasingizaji, wanaomchukia Mungu, wajeuri, wenye kiburi na majivuno, wenye hila, wasiotii wazazi wao, 31wajinga, wasioamini, wasio na huruma na wakatili. 32Ingawa wanafahamu sheria ya haki ya Mungu kwamba watu wanaofanya mambo kama hayo wanastahili mauti, si kwamba wanaendelea kutenda hayo tu, bali pia wanakubaliana na wale wanaoyatenda” (Warumi 1:18-32).

Gundua kwamba tabia zilizopo leo miongoni mwa wengi zitatupeleka kwenye kuangamia. Si tu kwa wale wanaozitenda, bali hata na kwa wale wanaozikubali na kuziruhusu!

Je wanadamu wamekuwa wakimtafuta Mungu na kuifuata njia yake – ama siku zote wanafuata fikra za kibinadamu kuhalalisha kuendelea katika njia yao wenyewe? Sawa na Mtume Paulo alivyoandika juu ya wote waufuatao mwili:

“16 maangamizi na taabu viko katika njia zao, 17wala njia ya amani hawajui. 18 Hakuna hofu ya Mungu machoni pao” (Warumi 3:16-18).

Jisomee utafakari sura hii yote kwa makini.

Pointi muhimu katika kuuelewa mpango wa Mungu imeonyeshwa hapa.

Elewa kwamba Mungu anazungumzia juu ya NJIA maalum ya kuiendea amani – na kwamba anaunganisha kutojua na kitu kimoja: kutokuwa na aina sahihi ya utii na uoga (kumcha) – WOGA wa kimungu. Msingi wa tabia ya utii na heshima hata kufikia KUYABEZA MATAKWA NA MAMLAKA YA MUNGU na ndiyo hali halisi iliyopo miongoni mwa watu wa kila aina ya jamii katika maisha ya leo. Katika “kizazi chetu kilichostarabika” kama tujiitavyo, wanadamu hawaogopi kutenda uovu.

Hili limetupeleka wapi?

Katika Marekani, kutaja mfano mmoja, kuongopa kunachukuliwa kuwa ni haki inayolindwa na katiba ya nchi hiyo kulingana na maelezo ya Mahakama Kuu yao. Kila kitu kimewekewa ufunguo wa neno la siri kukifikia (passwords) na kupata habari zake. Kila mahali kumetapakaa uvunja sheria na umwagaji damu (Ezekieli 7:23).

Watu sasa wanaanza kutambua kwamba kuna tatizo ndani ya jamii hii ya ulimwengu. Na lililodhahiri hata zaidi ya JANGA LINALOZIDI KUONGEZEKA la uvunjaji sheria ni kule kutambua kuwa katika kizazi chetu DUNIA YOTE IKO HATARINI kutokana na majasusi, wauaji wa kujitoka muhanga, madikiteta wa mataifa makubwa ambao sasa tayari wamejipatia uwezo wa kuufuta uhai wote toka sayari hii. Na siyo toka mataifa ama kundi la mataifa pekee ambayo yanaonekana kupenda vita kwamba wao ndio tishio pekee (Isaya 10:5-11).

Imetabiriwa!

Nyakati hizi za kutisha zimetabiriwa na kufafanuliwa katika Biblia yako. Fungua Biblia yako sasa kwenye 2 Timotheo 3:

“1 Lakini yakupasa ufahamu jambo hili, kwamba siku za mwisho kutakuwa na nyakati za hatari. 2Kwa maana watu watakuwa wenye kujipenda wenyewe, wenye kupenda fedha, wenye kujisifu, wenye kiburi, wenye kumkufuru Mungu, wasiotii wazazi wao, wasio na shukrani, wasio watakatifu, 3wasio na upendo, wasiopenda kupatanishwa, wasingizijaji, wasiozuia tamaa zao, wakatili, wasiopenda mema, 4wasaliti, wakaidi, waliojaa majivuno, wapendao anasa zaidi kuliko kumpenda Mungu. 5Wakiwa na mfano wa utauwa kwa nje lakini wakizikana nguvu za Mungu. Jiepushe na watu wa namna hiyo” (2 Timotheo 3:1-5).

Paulo alivuviwa kumwandikia Timotheo juu ya siku za mwisho—karne hii ya 21, pale USTAARABU wenyewe utakuwa hatarini kutoweka!

Fuatilia kwa makini hali ya kumomonyoka maadili ya wanadamu wa siku zetu. Ndiyo, mataifa yote siku hizi yanatamani mali za wengine na yako tayari KUUA NA KUANGAMIZA ili wazipate. Badala ya kumtafuta Mungu Mwenyezi, mataifa yaliyo mengi

hujivunia uwezo wao wa majeshi na silaha zao za maangamizi. WANAMKUFURU Mungu bila kukoma kwa maneno na vitendo.

Mbele za Mungu, wengi leo ni wakorofi. Wengi wana “muonekano wa uchamungu,” lakini wanakana nguvu zake za kujiingiza kwenye maswala ya ulimwengu na mamlaka yake ya KUTAWALA maisha yao binafsi ama wote pamoja. Watu katika kila taifa yaonekana wame pania kutenda mambo kivyao kinyume na Mungu wa kweli wa Biblia.

Njia hiyo inapeleka kwenye MAUTI. Mungu alimuvuvia Yeremia kuandika kwamba: “Moyo ni mdanganyifu kupita vyote, unaugonjwa wa kufisha” (Yeremia 17:9). Asili ya mwanadamu haijabadirika! Lakini wasomi wengi na watu wengine wanajidai kutenda kana kwamba imebadirika.

Kumbuka Kristo alisema hali katika ulimwengu huu kabla ya kuja kwake ingekuwa: “kama katika siku za Nuhu” (Mathayo 24:37). Tofauti na siku za Nuhu, mwanadamu kwa sasa anao uwezo wa kufutilia mbali uhai wote haraka na mara moja utoke katika sayari hii – tena kwa njia nyingi tu.

Mwanasayansi wa Kiingereza Sir Robert Watson – Watts, mvumbuzi wa kwanza wa mawasiliano ya “radar”, anasema, anafunua yafuatayo kwamba: “Sina matumaini kuwa mwanadamu ataendelea kuishi kwa maika 10 mingine ijayo”. Anataja kuwa kuna NJIA TATU ambazo wanadamu wa ULIMWENGU WANAWEZA KUFUTILIWA MBALI ndani ya masaaa MACHACHE tu. Ya kwanza ni BOMU la Hydrogen, Ya pili ni silaha kali ya sumu ya “Toxin” iwezayo kutengenezwa kutoka kimelea kitiwacho BOTULINUS. “Inahitajika KIASI CHA KILO MOJA TU kuweza KUUA wanyama na WANADAMU WOTE WA ULIMWENGU”, anaonya kwa hofu! “Tena inatengenezeka kwa urahisi tu, inajulikana kiasi kikubwa, na, kundi lililofundishwa vema, laweza kuitumia sumu hii kuangamiza. Kama aina ya tatu ya silaha ya maangamizi ya wanadamu, alizitaja silaha za GESI za NEVA (NERVE GASES). Njia tatu za maangamizi ya Ulimwengu wote!

Tafakari hayo!

Miongo kadhaa, Sir Robert Watson na Dr. Brock Chisholm, wa Victoria “waliunganisha nguvu kuuelimisha ulimwengu juu ya elimu ambayo sasa haikutakiwa ibaki siri” (Daily Sun, Vancouver, B. C., Jan. 21, 1959). Afisa mmoja wa juu toka ofisi za jeshi la Marekani – Pentagon, huko Washington, D. C., aliliweka wazi jambo hilo: “Tuko katika hofu kuu kiasi cha kufa hata kutaja tu juu ya silaha za kimelea (Botulinus)”.

Na tokea wakati huo hadi sasa kiwango cha uangamizaji kimezidi kuongezeka.

KITU FULANI CHA MUHIMU LAZIMA KIFANYIKE la sivyo mwanadamu atajiangamiza kabisa yeye mwenyewe.

Tumaini Moja Tu

Msingi wa chanzo cha machafuko ya ulimwengu, na kimsingi

– ufumbuzi wake, imefafanuliwa kwa ufasaha na wanasiasa wawili marehemu wa Kimarekani. Katika hotuba yake ya kutawazwa, Rais Dwight D. EISENHOWER Alieleza:

“Katika matukio makuu yapitayo kasi, tunajikuta tukipapasa kutafuta kujua maana halisi na kusudi la nyakati ambazo tunaishi... Ni mbali kiasi gani tumesafiri katika safari ndefu ya mwanadamu kutoka gizani kuelekea kwenye nuru? Je, tunaikaribia nuru—siku ya uhuru na amani kwa wanadamu wote? Ama ni vivuli vya usiku mwingine vinatunyemelea kwa kasi? . . . Sayansi yaonekana iko tayari kututunuku juu yetu, kama zawadi yake ya mwisho, UWEZO WA KUUFUTA UHAI WA MWANADAMU TOKA SAYARI HII”.

Ndiyo, anaelewa—anatambua kwamba mwanadamu anaweza kujiangamiza mwenyewe. Kisha baada ya kuainisha kanuni tisa ambazo zingeongoza mahusiano ya kimataifa, alitamka ukweli ambao—lwapo ungetumika kwa usahihi – ungekuwa hatua kubwa kuelekea kwenye suluhisho, si wa matatizo yetu pekee, bali na wa ulimwengu wote. Alisema: “Kwani ukweli huu sharti ueleweke kwetu sote: Chochote ambacho America inataraji kukileta kipokelewe ulimwenguni sharti kwanza kipokelewe ndani ya MIOYO ya Wamarekani”.

Iwe alilitambua hili ama la, Rais Eisenhower aliongea sawa kabisa na maneno ya Mungu wakati wa hotuba yake hiyo kwamba katika America—sawa na katika mataifa mengine—moyo, TABIA za wanadamu sharti zibadirike ikiwa tunahitaji kupata amani duniani.

Ebu sasa na tufuatilie maneno ya kipekee na mazito yaliyotamkwa na mtu mashuhuri, marehemu Generali Douglas MacArthur kuhusu swala hili. Pale alipopumzishwa jukumu la kuongoza kikosi cha jeshi na kuagizwa arejee Marekani na Rais Truman, GENERALI MACARTHUR alitoa HOTUBA ya kihistoria mbele ya kusanyiko la Bunge la Marekani. Katika hotuba hiyo ya kulisimua, alitoa maelezo makuu yaliyobainisha weredi wake, alisema:

“Ninajua vita sawa na watu wengine wachache sana waishio sasa wanavyojua, na hakuna kingine kwangu mimi—na hakuna kingine kwangu kinachochukiza zaidi...., Wanadamu tangu mwanzo wa nyakati wameitafuta amani. . . Ushirikiano wa Kijeshi, jitihada za kulinganisha nguvu, Umoja wa Mataifa, yote haya moja baada ya jingine yameshindwa, yakiacha njia pekee kuwa ni kwa kupambana katika vita. Uangamifu mkubwa wa vita sasa unaiziba njia hii kuwa haifai tena. TUMEVUKA FURSA YETU YA MWISHO SASA. Iwapo hatutabuni mfumo mbadala na ulio bora zaid kwa sasa, “HAL—MAGEDONI” yetu itatunyemelea mlangoni. Tatizo letu kimsingi ni la KITHEOLOJIA na LINAHUSU kuwa na roho iliyopondeka zaidi na KUBADIRIKA KWA TABIA YA MWANADAMU ili iendane na mwelekeo wetu wa kasi ya maendeleo ya kisayansi, sanaa, fasihi pamoja na dhana na maendeleo ya kiutamaduni ya miaka 2000 iliyopita”. “NI SHARTI ITOKANE NA ROHO IWAPO TUNATAKA KUUOKOA MWILI”.

Ebu na tuyatafakari maneno haya ya nguvu. Pamoja na kwamba huyu alikuwa ni Jemedari mashuhuri, MacArthur aliamini kwamba—katika vita ya dunia—tulikuwa tayari tumepitia fursa yetu ya mwisho! Wanajeshi wote hawa walijua wazi kabisa kwamba SULUHU PEKEE – TUMAINI pekee la kuepuka kuangamia kwa wanadamu—ilikuwa ni kubadirika kwa roho ya mwanadamu – kubadirika kwa mwenendo wa watu uelekeo kupenda uovu (Mhubiri 7:9; Ezekieli 11:19-20) —kuijenga upya TABIA ya mwanadamu.

Jibu

Iwapo wanadamu waliopotoka wangeachiwa wenyewe kwa muda wa kutosha walete ufumbuzi wa matatizo ya ulimwengu huu, hatima yake ingekuwa KUANGAMIA kwa dunia (Mathayo 24:22; Marko 13:19-20).

Watu wengi wanakusudia kufanya mambo sahihi, lakini hawaijui njia ya kuelekea kwenye amani. Wanadhamira ya kweli, lakini kweli wamepotoka. Sawa na Selemani alivyovuviwa kutuandikia: “Iko njia ionekanayo kuwa ni sahihi mbele ya mwanadamu, lakini hatima yake ni njia za MAUTI” (Methali 14:12).

Mungu anabainisha kwamba njia ya kawaida, ambayo mtu wa tabia ya asili anaitamani kuifuata huishia kwenye mauti. Watu daima hudanganyika kwa kudhani kwamba hakuna hatari yoyote kwa sasa – kwamba siku zote ulimwengu umekuwa hivihivi. Hii ni kweli kwa sehemu fulani.

Asili ya mwanadamu daima imekuwa hivi siku zote. Mtu wa tabia za kimwili siku zote kaleta mauti na uangamifu kwa ulimwengu. Hata hivyo, kumbuka kwamba Paulo alisema: “Bali watu waovu na wazindi watazidi kuwa waovu zaidi na zaidi” (2 Timotheo 3:13). Na la muhimu kupita yote, KUANGAMIZWA KWA WANADAMU WOTE HAKUJAWAHI KUWEZEKANA KABLA YA NYAKATI ZA VITA YA II YA DUNIA – na sasa imezidi kuwa hatari zaidi.

Mwanadamu katengeneza bunduki na mizinga siku nyingi zilizopita. Baadaye, vifaru na ndege za kivita zikaanza kutumiwa. Lakini kwa sasa tunazo roketi ziwezazo kubeba silaha za “hydrogen missiles” na kuweza kuangamiza miji kadhaa kwa kubonyeza swichi ya “remote” tu! Inaaminika kwamba mabomu ya “electromagnetic pulse”, ikiwa yatalipuliwa sehemu iliyokusudiwa, yanauwezo wa kuurudisha ulimwengu wa nchi kama za magharibi hadi karne za enzi za mawe. Uwezekano wa kuangamia kwa wanadamu siyo jambo la kukisia tu bali ni ukweli wa kuogofya!

Na sasa hakuna kiwezacho kumwoko mwanadamu toka kujiangamiza mwenyewe bali tu ni KUBADIRIKA kwa asili ya mtu – katika tabia ya wanadamu. Lakini pamoja na utele wa makanisa yajiitayo kuwa ya “Kikristo” – pamoja na jitihada finyu za Umoja wa Mataifa – pamoja na jitihada zote anazozifanya mwanadamu kuleta amani na furaha, VITA KAMILI inazidi kutosogelea. Japo kutakuwepo nyakati zionekanazo kuwa ni

za amani, matangazo ya amani na usalama yatatolewa punde tu kabla uangamifu utujiapo kwa ghafla (1 Wathesalonike 5:3). Cha kusikitisha, wengi watawaamini wale watakaotangaza kuja kwa amani ya uongo isiyochini ya Mungu wa Biblia (Ezekieli 13:10-16).

Sawa na Suleimani alivyovuviwa kuandika: “NJIA IONEKANAYO KUWA NJEMA MACHONI MWA WANADAMU DAIMA NI NJIA YA MAUTI”. JIBU NI LIPI? NI MUNGU PEKEE NDIYE AWEZAYE KUIBADIRI TABIA YA MTU, na kuwalazimisha wanadamu kujifunza njia ya amani.

Hiyo ndiyo SABABU inayomrudisha Kristo kuja kuchukua “Falme za Ulimwengu huu” (Ufunuo 11:15).

Hiyo ndiyo SABABU “Yeye mwenyewe ndiye atawatawala kwa fimbo ya chuma” (Ufunuo. 19:15). Hiyo ndiyo njia pekee ya kuyaokoa maisha ya mwanadamu yasitoweke toka sayari hii. Yesu Kristo alijua juu ya hali mbovu ya maswala ya watu ambayo wangejiletea wenyewe katika siku hizi za mwisho, pale aliposema: “Na kama siku hizo zisingalifupizwa, HAKUNA MWANADAMU ANGEOKOLEWA HAI” (Mathayo 24:22).

Mungu na akusaidie uelewe umuhimu na uhalisi wa mambo haya kadri usomapo makala hizi.

Zinaonyesha kwamba Mungu aliona kabla juu ya kubuniwa na kuundwa kwa silaha tulizonazo leo za maangamizi makuu mapema kabla hata mwanadamu hajawahi kuota kuwa angeziunda. Na zinafunua kuwa Mungu tayari alikuwa amebuni suluhisho pekee na la maana. Mpango wote kamili wa Mungu ni wa maana na halisi.

Muundo wa MPANGO wa Mungu usioeleweka sana kwa wengi umetolewa ndani ya sura za kwanza mbili za kitabu cha Mwanzo. Ni JUMA la siku saba.

Sawa na Mungu alivyozianzisha nyakati pale mwanzo, mwanadamu amepewa siku sita za kazi zinazofuatiwa na siku ya mapumziko. Katika Waebrania 4:4, 11, siku ya saba pia ni kivuli cha pumziko la amani—pumziko la miaka 1,000 ambalo litafuatia kizazi chetu hiki cha kazi za wanadamu za mahangaiko na taabu duniani.

Fuatilia kwa umakini pumziko lenye amani la baada ya Kristo kujiingiza na kuanzisha utawala wake liitwalo “akatawala miaka elfu” (Ufunuo 20:4). Iwapo “siku ya mwisho” ya mpango wa Mungu wa miaka 7,000 – ni miaka 1,000, basi zile SIKU SITA ALIZOZITENGA KUTUMIWA NA WANADAMU kwa KAZI nazo ni dhahiri zitakuwa sawa na miaka 6,000.

Na hili ndilo hasa matukio ya ulimwengu yanalolithibitisha.

Tazama hali ilivyo! Ulimwengu huu unaelekea kuangukia kwenye KUANGAMIA!

Ukijumulisha miaka mbalimbali ya watu wa Kitabu cha Mwanzo, miaka ya utawala wa wafalme mbalimbali, na kuongezea tarehe za matukio kadhaa ya kwenye Biblia, utakuta kwamba miaka

6,000 ya wanadamu kujisimamia ni dhahiri imefikia kikomo.

Kwa maneno mengine MFUATANO WA MATUKIO YA ULIMWENGU unathibitisha tuko KARIBU SANA na muda ambao maandiko siku zote yameusema kuwa KRISTO ATAREJEA – pale udhahiri wa kufikia kwa muda wa dunia kujiangamiza utafika. Miaka elfu sita ya historia ya mwanadamu umfikia ukingoni. Hapa, sasa, tunakupa uthibitisho-UTHIBITISHO MARA DUFU—kuwa KRISTO ANAKUJA katika nyakati za kizazi chetu!

Mtazamo kuwa wanadamu wameishi katika dunia kwa makumi ya maelfu ya miaka iliyopita ni ngano isiyoweza kuthibitishwa! SAYANSI yenyewe inaithibitisha kuwa si kweli! Hata kama itaonekana kuwa hili ni la ajabu, nadharia ya kuwa mtu katokana na mabadiliko “evolution” nayo si kwamba tu haithibitiki, bali pia inathibitika kuwa ni upuuzi pale tunapoelewa ukweli.

Somo lifuatalo punde litakupa kweli hizi ili uweze kujifunza mwenyewe nyumbani! Hata Mitume nao hawakuwa tayari wamepata uelewa juu ya MPANGO WA MUNGU huu pale Kristo alipokuwa angali hapa duniani. Walifikiri ufalme ungesimikwa wakati wa nyakati zao, ilipokuwa bado ni miaka 4,000 tu ya mpango wa Mungu ndiyo pekee iliyokuwa imekamiliika.

Lakini kabla hawajafariki, MITUME WALIKUWA TAYARI WAMEUJUA MPANGO WA MUNGU. Petro alisema: “Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake (ya kuja kwa Kristo) . . . bali anavumilia” (2 Petro 3:9).

Mungu yu mvumilivu.

Mungu amejizua kuingilia katika maswala ya ulimwengu kwa takribani miaka 6,000.

Kwa nini?

Sababu hawezi kuingilia hadi pale mwanadamu atakapofikia kumlilia Mungu baada ya kukabiliwa na janga la kujiangamiza mwenyewe. Elewa kwamba siku ya Kristo kujiingiza na kutawala imelinganishwa na “miaka elfu moja” (Ufunuo 20:4; Zaburi 90:4).

Petro pia anasema kitu kilekile—kwamba siku moja machoni kwa Mungu ni sawa na “miaka elfu moja” na “miaka elfu moja” ya maisha ya ustaarabu wa mwanadamu ni sawa na siku moja katika mpango wake wa juma moja la miaka elfu moja moja—ya siku saba (2 Petro 3:8).

KRISTO ANAREJEA BAADA YA SIKU SITA ZA MIAKA ELFU MOJAMOJA ya mahangaiko na taabu ya utumwa wa mwanadamu. Wafuasi wa kweli wa Kristo kwa miaka mingi wametambua kwamba Mungu atamtuma Yesu Kristo kuja kuusimika ufalme wake katika mwaka wa siku ya saba ya miaka elfu moja, ambao utaleta nyakati za mapumziko na amani.

Ni wa KUSISIMUA kiasi gani kwamba ni katika nyakati zetu hizi pale ambapo miaka 6,000 tayari IMEFIKIA KIKOMO, ndipo ulimwengu umetiishwa na kuangamizana. Ni wa KUTIA MOYO kiasi gani kwamba Yesu mwenyewe alisema kwamba pale

tutakapoyaona haya yote yakitokea tujue YU KARIBU KURUDI!

Biblia ni Nini?

Neno Biblia linatokana na neno la Kigiriki biblio linalomaanisha kitabu.

Pale kozi hii (sawa na wengine wengi) litumiapo neno “Biblia” au “Biblia Taklatifu” hii inataja vitabu 39 vinavyoaminika kuwa ni “Maandiko” yaliyo andikwa hapo awali kwa Kiebrania na Wayahudi (yajulikanayo kuwa ni maandiko ya Kiebrania ama Agano la Kale), pamoja na vitabu 27 vinavyoaminika kuwa ni maandiko na hapo awali viliandikwa kwa Kigiriki na wale waliokuwa wanafunzi wa Yesu Kristo (yajulikanayo kama maandiko ya Kigiriki ama Agano Jipya). Maandishi yaliyomo katika Biblia yanachukuliwa kuwa ni “Maandiko”.

Hakuna kitabu chochote cha Biblia kilichoandikwa hapo mwanzo kwa lugha ya Kilatini na wala hakuna kilichokuwa hapo mwanzo kimeandikwa kwa Kiingereza ama Kiswahili. Hivyo Biblia ya zamani ya Kilatini cha kale “Vulgate” iliyoandikwa na Jerome ambayo wengi wa Wakatholiki waliitumia pamoja na Biblia mashuhuri iitwayo “King James Version” ambayo wengi wa madhehebu ya Kiprostanti hupenda kuitumia vyote ni tafsiri ambazo MUNGU HAKUZIVUVA MOJA KWA MOJA sawa na Maandiko ya awali! Hizi ni tafsiri zilizotokana na tafsiri tena zingine kiasi cha kupoteza baadhi ya maana zilizokusudiwa hapo awali. Mara nyingi tafsiri huwa na makosa ambayo aidha yalikusudiwa ama yalikuwa ya bahati mbaya.

Maandiko ya awali kabisa ya Biblia hayapo tena kwani yalioza, ama kupotea au hata yaliharibiwa. Hata hivyo, bado kuna maandiko mengi ya awali ambayo yanapatana na Biblia zilizotafsiriwa kwa usahihi, yanayoithibitisha kuliko maandiko mengine ya maelfu ya miaka ya kale. Wayahudi, kwa mfano, walikuwa na utaratibu makini sana wa kunakiri na kuhakiki ili kudhibiti upotezaji wa maana ya awali ya maandiko. Agano Jipya lenyewe lilikuwa na nakala nyingi zilizosambaa kwa wengi ndani ya kipindi kifupi baada ya kuandikwa kwake ili kuhakikisha kutotokea kupotea ama kubadirishwa kwa maana ya awali ya Maandiko.

Lakini sasa ni toleo lipi la maandiko ya awali ndilo liwe msingi wa kutumika wakati wa kutafsiri imekuwa ni hoja yenye mkanganyo. Toleo la “Nestle-Aland NA27” la Kigiriki la Agano Jipya (NA27/UBS4) lenyewe hudai kwamba lilitumia matoleo yote ya Kigiriki ya Agano Jipya yaliyokuwepo wakati wa utafasiriwa wake, na kwa kawaida linadai ndilo lililo karibu zaidi na maandiko ya awali (na wala halikuweka maandiko batiri kama yale ya 1 Yohana 5:7-8 ambayo tafsiri ya “Textus Receptus” inayo). Japo hii haimaanishi kwamba toleo la NA27 halina makosa; ni maandiko ya awali ndiyo yanafaa, na inaonekana maandiko yaliyotafsiriwa toka toleo hili ndiyo yakubalikayo na wengi kuwa yako sawa na yale ya awali “Traditional Text”—ambako ndiko matoleo ya “Textus Receptus” yalitoka—ambayo ndiyo yalikuwa maandiko yatumiwayo na kanisa la kale la Asia Ndogo na lile la Byzantium.

Cha ajabu, pale makanisa ya Kigiriki na Kirumi yalipoanza kupinda kutoka kwenye mtazamo wa Kibiblia juu ya Uungu wakati wa mwishoni mwa karne ya nne, makanisa haya yalianza kupunguza kutegemea “Maandiko ya Awali” kama mwongozo na wakati mwingine yakatumia zaidi nyaraka ambazo hazikuwa sahihi na hazifai kutumiwa (Burgon JW. *The Causes of the Corruption of the Traditional Text of the Holy Gospels*. Cosimo Classics, 2007, p. 2).

Nje ya ulimwengu wa Kirumi na kiorthodox ya masahariki, tafsiri mbili miongoni mwa zile zilizokuwa zikitumika sana zilizo za kiingereza ni ile tafsiri ya “King James Version” (KJV) ya mwaka 1611 na ile ya “New Kings James Version” (NKJV) ya mwaka 1982. Hizi zote zilitafsiriwa ili zilete maana ya neno- kwa - neno ambapo (KJV imetokana na toleo la “Textus Receptus” na NKJV ikiwa imechanganya, toleo hili na pia baadhi ya “Maandiko ya Awali” na mengine ambayo waliotafsiri KJV hawakuweza kuyapata). Tafsiri za neno-kwa-neno ni bora zaidi kwa kujifunza Biblia kuliko zile zilizotafsiriwa kwa kufuata maana ya aya katika Biblia. Tafsiri ya kuonyesha maana ni jitihada za yule anayetafsiri kutoa maana ya aya ama sura ile anayotafsiri kwa kufuata kile anachoon, anachodhani, ama anachokiamini kuwa maandiko ya awali yalimaanisha, kinyume na kutafsiri ya kila neno jinsi lilivyo na hivyo kumwacha msomaji aamua mwenyewe lengo la aya ama sura. Lakini kwa kuwa tafasiri hizi za maana ni nyingi na rahisi kuzisoma kuliko zile za neno-kwa-neno, wengi huzipendelea.

Kwa usomaji wa kila siku mimi siku hizi hupendelea kutumia tafsiri ya Biblia ya “New Kings James Version” (NKJV) kwa kuwa ndiyo iliyo miongoni mwa zilizo sahihi zaidi; ndiyo inayo makosa ya utafasiriji lakini pia inatumia lugha ya siku hizi. Nimesoma tafasiri nyingi mbalimbali kwa ukamilifu.

Huko nyuma nilizoea kutumia tafsiri ya KJV zaidi, lakini ni ngumu kwa walio wengi kuelewa – kwa kuwa wengi wa watu wa siku hizi wanashida ya kukielewa Kiingereza cha kale na wengi wa walio si wazaliwa wa lugha hiyo hupata shida sana. Pamoja na KJV, ijapokuwa wengi huiamini sana, lakini tafsiri hiyo inayo makosa mengi (imeitafsiri vibaya aya ya Matendo 12:4, Waebreania 4:9, 1 Yohana 5:7-8, na kadharika) – kiukweli tafsiri hii si bora kuliko tafsiri nyingine zote zilizopo kama wengi waaminivyo!

Ni muhimu ieleweke kwamba Biblia haikuwahi kueleza kwamba Roho ya Mungu ingewaongoza wale watakaotafsiri Biblia toka lugha za awali kwenda lugha za mataifa mbalimbali (kama ambavyo wengi watumiao KJV na wale wa Septuagint wanavyodai na Kuamini).

Nyakati zingine kwa ajili ya ufafanuzi, nitanukuru toka NIV (New International Version). Japo tafsiri hii siyo mahala pote ya neno-kwa-neno, nyakati nyingine imeyaweke baadhi ya maneno kwa usahihi zaidi kuliko NKJV au KJV.

Katika makala ziongeleazo maswala ya Kikatholiki nitaweza kutumia tafsiri ya Douay Rheims (DRB) ya mwaka 1610 ama tafsiri iliyoifuatia—lakini kwa kuwa ni tafsiri toka tafsiri nyingine

(Jerome aliitafsiri Biblia kwenda Kilatini karibia na mwisho wa karne ya nne na Douay-Rheims ni tafsiri ya Kiingereza iliyotokana na ile ya Kilatini ya Jerome). Sipendekezi kwamba itumike kama tafsiri tegemeo. Wakatholiki pia hutumia tafsiri ya “New Jerusalem Bible” (NJB)—ambayo ni tafsiri ya neno-kwa-neno zaidi kuliko ile ya DRB, japo wakati mwingine inayo makosa yake. NJB yaonekana kuwa ndiyo tafsiri ya Biblia ya Kiingereza itumiwayo zaidi na Wakatholiki nje ya Marekani. Na kwa vile inatumia zaidi lugha ya siku hizi, naiona NJB kuwa ya msaada zaidi, hususani pale nilengapo jamii ya watu wa asili ya Kikatholiki zaidi.

Wakati mwingine inasaidia ukisoma tafsiri kadhaa juu ya aya ama sura fulani unayojifunza kwani yaweza kukusaidia kuelewa zaidi, japo wakati mwingine makosa ya tafsiri yaweza kuwa tatizo. Lakini kadri ujisomeapo Biblia mara kwa mara, hususani ikiwa ni kwa mwongozo wa Mungu, ndivyo utakavyoweza kupambanua zaidi ukweli upi ulikusudiwa kinyume na makosa ya mila za wanadamu zilizojiingiza.

Zaidi kuhusu jinsi vitabu vya Biblia vilivyokusanywa na kuwekwa pamoja na ni vipi vilikubaliwa kuwa ni maandiko matakatifu, haya yataongelewa katika masomo mengine.

Isome Biblia

Pale alipokuwa na njaa kimwili na akijaribiwa na Shetani, Yesu alinukuru toka kitabu cha Kumbukumbu la Torati:

“4 Mtu hataishi kwa mkate pekee, bali kwa kila neno linalotoka kwenye pumzi ya Mungu” (Mathayo 4:4).

Majibu yake mengine pia kwa Shetani vilevile yalitokana na kuyatumia na kuyanukuru Maandiko (Mathayo 4:7, 10) badala ya kutumia fikra za kibinadamu (ama mila zipinganazo za watu).

Sababu mojawapo juu ya ni muhimu kuisoma Biblia, ni kwa vile:

“3 Maana utakuja wakati watakapoyakataa mafundisho yenye uzima, ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe watajipatia walimu makundimakundi, kwa kuwa wana masikio ya utafiti; nao watajipusha wasisikie yaliyo kweli na kuzigeukia hadithi za uongo” (2 Timotheo 4:3-4).

Nyakati zilizokuwa zimelengwa hapo juu yaonekana ni hizi zetu na yamkini zitazidi kuwa mbaya.

Yesu alisali kwa Baba kuomba:

“17 Watakase na ile kweli yako. Neno lako ndilo kweli” (Yohana 17:17).

Zaburi inaeleza: “.....Sheria yako ni kweli” (Zaburi 119:142b).

Kwa kuwa sheria ya Mungu na neno lake ndizo kweli, utawezaje kuujua ukweli pasipo kuisoma ama kuisikia Biblia ikisomwa kwako?

Kuisoma Biblia ndiyo njia ya kupima iwapo kitu fulani ni cha

kweli. Biblia inatufundisha neno la Mungu na jinsi ya kuishi.

Paulo alikuwa mhubiri wa Mungu, lakini watu wangemjua? Wangelimjua kupitia uelewa wao wa Biblia.

Unaipataje elimu ya Biblia? Kwanza kabisa ni kwa kuisoma ama kusomewa. Kisha ni kwa kujifunza unayoyasoma ama kusomewa.

Pale Paulo alipohubiri kule Beroya ilitangazwa kwamba:

“11 Watu hawa walikuwa waungwana (yaani -waelekevu) kuliko wale wa Thesalonike, kwa kuwa walilipokea lile neno kwa uelekevu wa moyo, kisha wakayachunguza maandiko kila siku, waone ikiwa mambo hayo yalikuwa ndivyo hivyo” (Matendo 17:11).

Waberoya waliyachunguza Maandiko kila siku; yatupasa tufanye hivyo pia.

Maandiko yalivuviwa na Mungu (2 Timotheo 3:16) na wala hayakutokana na mawazo ya wale waliyoyaandika. Nabii zake zilitoka kwa Mungu, “Maana unabii haukuletwa popote kwa mapenzi ya mwanadamu, bali wanadamu watakatifu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Takatifu” (2 Petro 1:21).

Ebu jionee yafuatayo toka maandiko ya Biblia:

“19 Nasi tuna lile neno la unabii lililo imara zaidi, ambalo, mkilitii, kama taa ing’arayo mahala pa giza, mwafanya vema, mpaka kutakapopambazuka, na nyota ya asubuhi kuzuka mioyoni mwenu: 20 Mkijua neno hili kwanza, ya kwamba hakuna unabii katika maandiko upatao kutafsiriwa kama mtu fulani apendavyo tu. 21 Maana unabii haukuletwa popote kwa mapenzi ya mwanadamu, bali wanadamu watakatifu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Takatifu” (2 Peter 1:19-21).

Neno la Mungu la unabii ni la hakika. Hili kwa hakika ni faraja kwetu katika siku hizi za mwisho.

Zaidi ya kutupatia maagizo, mafundisho na kutuonya, kuisoma Biblia pia yaweza kukusaidia kuyajua mawazo na makusudi ya moyo wako:

“12Maana neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena linaukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo” (Waebrania 4:12).

Wakristo wanahitaji kuisoma Biblia na kujifunza.

Maelekezo Muhimu ya Mwisho

Sasa tuko tayari kuanza kipengele cha mwisho cha somo. Lakini subiri kidogo! Je, Biblia yako iko mbele yako? Ikiwa haiko, usiendelee kusoma hata neno moja zaidi! ISHIA HAPA KWANZA!

NENDA na KAILETE BIBLIA YAKO.

Vilevile kalete karatasi kadhaa ama daftari, na kalamu ama penseli, ili uweze KUANDIKA NOTISI zitakazokusaidia kujifunza na kukumbuka.

Kozi hii itatumia tafsiri ya Biblia ya “New King James Version (NKJV)” kwa kuwa imekusudiwa ikupe tafsiri ya neno-kwaneno na inatumia lugha ya Kiingereza kinachoeleweka kwa watu wa karne hii ya 21. Kwa masomo mengi yatakyofuata waweza kutumia aina ya tafsiri zingine, lakini maswali na majibu kimsingi yatatokana na NKJV labda tu pale pameelekezwa tofauti. Hivyo, kwa wengi wenu, tafsiri ya NKJV ya Biblia ndiyo chagua bora la kutumia katika Kozi ya Jifunze Biblia.

Sasa tuko tayari kulianza somo hili. KUMBUKA-UNAPASWA KUIFUNGUA Biblia yako KWENYE KILA AYA tunayokutajia katika somo hili. Usituamini sisi tu (timu iliyosimamiwa na marehemu C. Paul Meredith na/au Bob Thiel)—bali unapaswa uamini kile ambacho hasa Biblia inakifundisha.

Unapaswa USOME na KUSOMA, kwa kweli UJIFUNZE kila aya kwenye Biblia. Hii ni kozi ya KUJIFUNZA BIBLIA – kujisomea kujua Biblia, na si tu kujifunza maneno tuliyoyaanisha hapa kwa ajili yako. Maneno yetu yamekusudiwa yakuelekeze ni wapi pa kutazama kwenye Biblia yako – ili kukusaidia uelewe namna ya kujifunza Biblia.

Sasa basi, pamoja na Biblia yako, kamusi (dictionary) nzuri, na karatasi zako za kuandika pointi zote zikiwa mbele yako, hii ndiyo mbinu utakayotumia kujifunza: Andika, kwa ufasaha, kwenye karatasi zako, Kichwa cha habari: “Somo la I,” na ukipigie mstari.

Kisha - “Mwisho wa Ulimwengu ni Nini?”

Chini yake, andika kila namba ya swali, kisha ANDIKA JIBU, kwa mwandiko wako mwenyewe (japo baadhi yenu mtapendelea kuchapa kwenye kompyuta ama kuandika kwenye simu zenu). Kama MFANO kwa maswali, hivi ndivyo utakavyo andika kwenye karatasi ama daftari lako:

1. Mathayo 24:3 – Hata alipokuwa ameketi {Yesu} kwenye Mlima wa Mizeituni, wanafunzi wake wakamwendea kwa faragha, wakisema, “Tuambie, mambo hayo yatakuwa lini? Nayo ni nini dalili ya kuja kwako, na ya mwisho wa zama”.

Kadharika andika wazo ama taarifa zozote zindanazo na swala hili unazohitaji kuzikumbuka. Utakapomaliza kuandika swali hili, na kujifunza majibu yake katika Biblia na kuwa na uhakika kwamba unalielewa, basi soma swali lifuatalo.

2. Andika majibu yako mwenyewe kwa swali, baada ya kuwa umeshasoma kile Biblia isemacho juu ya hilo kulingana na aya zilizoandikwa kuwa zinatoa majibu kwa swali hilo.

Baada ya swali la 3, andika majibu, na pia andika kila maneno ya aya ya Biblia, Mathayo 24:22.

Ikiwa waweza, itakuwa vema ukienda kwenye duka la stationary ama la vitabu na kujinunulia “punching Machine” ya kutobolea karatasi. Pia nunua file ama binder, ili uzitunze karatasi ama daftari la majibu na notisi zako pamoja na jarida hili la somo lenye maswali, yakiwa salama kwenye faili ama binder yako hiyo.

USITUTUMIE MAJIBU ya masomo haya. Yatunze tu kwa ajili ya kuyapitia na kujikumbusha. (Yawezekana tutatoa certificate ya bure kwa wale watakaokamilisha na kuhitimu kozi yote ama sehemu yake muhimu, lakini hili litaanza baada ya 2014, na kabla ya hapo tunatarajia kulitangaza hili kwenye mtandao na mahala pengine. Endapo tutafikia kufanya hivyo, tutakuomba ututumie nakala ya masomo uliyokamilisha na/ama maswali ya sehemu za kozi).

Wengine waweza kujiuliza, “Huku KUANDIKA ni kwa MUHIMU kweli?”

NDIYO!

Ni kwa MUHIMU MNO!

Kwa nini?

Hapa tunakupa sababu!

Tunapenda uielewe Biblia ki-ukweli. Wakristo wanatakiwa waje kuwa walimu (ona Waebrania 5:12) na hivyo wanatakiwa waijue Biblia yao vema ili: “Mwe tayari siku zote kumjibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu, lakini kwa unyenyekevu na upole” (1 Petro 3:15).

Kuyaandika yale unayojifunza kutakusaidia kukumbuka vema.

Zaidi sana, utaweza kufanya mapitio ya masomo yako kwa upesi zaidi, kila itakapohitajika, iwapo utakuwa umeyahifadhi katika mtindo huu. Kadharika, itakusaidia sana kuifafanua Biblia kwa wengine.

Sisi tunakupatia PICHA YA KWELI YA MUHTASARI WA BIBLIA. Siku zote utapenda kufanya mapitio ya masomo haya na KUTUMIA UFAFANUZI ULIOMO kuwaelezea wengine KWA MANENO YAKO MWENYEWI. Katika miaka ijayo kadri unapoyatumia maelekezo yaliyomo kuelewa na kuelezea pointi kadhaa za kwenye Biblia. Kumbuka, utahitaji kutumia angalau nusu saa kila siku katika kujifunza BIBLIA YAKO kupitia Kozi hii ya Kujifunza Biblia. Sasa tuko tayari....

Jifunze Biblia Yako: SOMO La I

“Mwisho wa Ulimwengu” Ni nini?

1. Je, Yesu aliwahi kuulizwa juu ya janga linalotishia kwa sasa ustaarabu wa mwanadamu – MWISHO WA ZAMA HIZI na dalili za kurudi kwake? Mathayo 24:3.

2. Je, aya hii hapo juu inazungumzia kuhusu kuangamia kabisa na kufikia mwisho wa DUNIA YA ARDHI hii? – ama ilihusu kufikia MWISHO WA ZAMA ZA USTAARABU HUU wa utawala mbovu wa mwanadamu? Tafsiri za siku hizi za Biblia zinaitafsiri kwa usahihi namna gani Mathayo 24:3?

MAELEZO: Yapo maneno matatu ya Kigiriki yaliyovuviwa kutumika katika Agano Jipya ambayo yote yametafsiriwa kuwa ni “WORLD- Ulimwengu” katika Kiingereza cha “King James Version” na kwa Kiswahili yalitafsiriwa kuwa ni “DUNIA”. Neno la awali la Kigiriki lililotumika kwenye Mathayo 24: 3 ni “aion”, kumanisha “AGE kwa Kiingereza” na kwa Kiswahili “ZAMA”! – siyo dunia yaani ardhi tunayoishi juu yake. Kwa kuwa wengi wamekua wakisia tafsiri zitokanazo na KJV zikisomwa mara kwa mara, wamepofushwa kwa kuelezwa maana isiyo sahihi juu ya kile Biblia inatoa unabii na kuamini kuwa ni mwisho wa sayari iitwayo dunia. Aya hii kamwe haizungumzii kuisha kwa maisha hapa duniani wala kuangamia kwa sayari yetu, bali ni juu ya kuisha kwa utawala wa kibinadamu wa kizazi hiki. Tafsiri ya Biblia ya NKJV imeliweka hili kwa usahihi (japo nayo, kama tafsiri zingine, inayo makosa sehemu zingine).

YESU, kwa hiyo, aliulizwa na wanafunzi wake juu ya kufikia mwisho kwa “zama” za kizazi hiki—kukoma kwa ustaarabu huu uliopo—na siyo kuteketea kwa sayari hii iitwayo dunia.

3. NI KIPI ambacho Yesu alitangaza kuwa KINGETOKEA IWAPO ASINGEREJEA? Mathayo 24: 22.

Alilolisema halihusiani na wokovu wa kiroho—bali ni kuokolewa toka kifo na maangamizi ya uharibifu utakaotokea. Tafsiri ya Moffatt imeliweka neno hili “asingeliokoka” kwa usahihi zaidi kwa kutafsiri: “HAKUNA NAFSI ingeokolewa IKIWA HALI.”

4. Je, Yesu anatoa unabii kwamba ni Wayahudi pekee, au ni Wakristo pekee, ndio watakaokabiliwa na janga hilo la kuangamia na kuteketea? Ama hapa anatoa unabii kwamba “HAKUNA MWENYE MWILI YEYOTE” angeokolewa toka janga hilo la uangamifu? Je, hili halithibitishi kuwa Mungu SHARTI aingilie kati ili kuzuia kuangamia kwa wanadamu wote?

5. Pale mataifa yatakapokuwa yanaangamizana katika MAJARIBIO YA KUMALIZANA ili kujipatia umilki wa ulimwengu, je, kujiingiza kwa Mungu KUTAZIFUPISHA siku za kusambaa kwa vita – vita ya dunia nzima? Linganisha Mathayo 24:22 na Marko 13:20.

MAELEZO: Aya hizi hazimaanishi kwamba Mungu atabadiri mpango wake wa ujumla wa siku zote wa maswala ya ulimwengu, bali kwamba, sawa na alivyopanga tangu awali, atajiingiza pale ambapo wanadamu watakuwa wamefikia muda wa uangamizana wenyewe. Kulingana na mpangilio wake wa wakati wa kuingilia kati atakuwa amezipunguza SIKU ZA UTAWALA WA MWANADAMU juu ya watu, ambazo kama isingekuwa hivyo ingepelekea kuteketezwa kwa uhai wote wa mwanadamu.

Kwanini SHARTI Mungu Aingilie Kati

1. Je, kumewahi kuwepo kwa NYAKATI ZA TAABU zilinganazo na zile zitakazotokea mwishoni mwa zama hizi? Mathayo 24:21.

Je, Marko 13:19 inasema nini juu ya hili?

2. Je, kuna nabii yeyote ambaye naye aliwahi kutabiri juu ya kipindi hiki cha maangamizi? Yeremia 30:7, Danieli 12:1.

Sawa na kila ya aya hizi zinavyoeleza kuwa hakujawahi kuwepo hapo kabla, na wala hakutatokea tena, kipindi cha taabu kama hiyo, je, wanaweza kuwa kila mmoja anazungumzia kipindi cha matukio tofauti, ama wote wanataja juu ya KIPINDI KILEKILE KIMOJA CHAHITIMISHO la mambo mwhishoni mwa zama hizi?

3. Je, manabii wanatoa picha ya matukio ya kuogofya yatakayotokea mwishoni mwa zama hizi kuwa ni matokeo ya uharibifu mkubwa unaosababishwa na MBINU ZA KIVITA ZA KISAYANSI YA LEO? Yoeli 2: 1-3. Soma pia Isaya 33:11, 12.

Je kutakuwepo tena wakati kama huu? Ni kwanini unabii huu wa Yoeli unazungumzia kipindi kilekile sawa na unabii wa Yesu?—je, yawezekana ufukara uliozagaa sawa na ule anaouzungumzia Yoeli, waweza kutokea kutokana na mbinu mbovu na zilizopitwa na wakati za kivita?

4. Je, uangamifu na uharibifu waweza kutokea sababu ya kuwepo kwa silaha za atomic na MABOMU YA HYDROGEN, ROCKETS, SILAHA ZA KIBIOLOJIA, SILAHA ZA KIELECTRONIC, GESI ziangamizazo, na MBINU ZINGINE ZA KISASA ZA USAFIRISHAJI MAJESHI NA SILAHA ambazo zaweza kufutilia mbali ustaarabu wa mtu? Ufunuo 9:5-10 na 16-19.

Je, vielelezo hapa kwenye Ufunuo yawezekana zinaainisha mateso yatokanayo na gesi ya sumu na MAUJAJI YA HALAIKI yatokanayo na silaha za kisayansi za kisasa? Yohana alikuwa AKIFAFANUA SILAZA ZA KIVITA ZA KIPINDI CHETU kwa kutumia VIELELEZO VYA ENZI ZAKE. Wakristo wa awali walijua hayo yalikuwa ni mafumbo tu kwa kuwa vitu vya aina hiyo havikuwepo kwa wakati huo. Ni dhahiri Yohana asingeweza kutumia maneno ya kileo kama vile “kifaruu” au “rocketi” au “helicopter” au “jet” kwa sababau hakuna yeyote—wala hakuna mtafasiri yeyote—angeweza kuelewa inamaanisha nini.

5. Ebu kwa sasa tutafakari kwa ufupi juu ya wakati, kadri ya MIAKA 4300 ILIYOPITA, pale Mungu ALIPOINGILIA KATI maswala ya wanadamu ili KUAHIRISHA kile tukionacho kikitishia ulimwengu leo. Je, wanadamu walikuwa wanataka wajitengenezee umaarufu wa jina na kuufanya ulimwengu udumu katika muungano chini ya utawala wa kibinadamu? Mwanzo 11:4.

6. KWANINI Mungu aliingilia kati kwa kuzitawanya kabila za watu na kuziparaganya lugha za wanadamu kwenye mnara wa BABELI? Mwanzo 11:6.

7. Je, hili linaonyesha kwamba MUNGU AMEKUWA NA

MPANGO katika kuahirisha na kuzuia maarifa ya ubunifu wa mtu? Je, si kwamba Mwanzo 11:6 pia inathibitisha kwamba pale wanadamu wafikiapo kuanza kutengeneza utawala mmoja ulimwenguni, waanzapo kufikia kuanza kujifunza kuzungumza lugha za wenzao, na hatimaye KUWA NA USHIRIKIANO wa mali na MAARIFA ya kisayansi, hapo ndipo HAKUNA CHOCHOTE ambacho WANAWENZA KUZUIWA?—kiasi kwamba wataangamizana wenyewe kutokana na ubunifu wao?

CHANZO cha MATATIZO ya Ulimwengu

1. Kwa vile Mungu ataingilia kati ili kuzuia kuangamia kwa mwanadamu, kadharika vilevile atazuia vita visitokee tena kwa kuondoa kile kisababishacho vita! CHANZO HALISI CHA VITA ni nini? Yakobo 4:1-2.

2. Je, nia na fikra za ASILI YA MWANADAMU kimsingi ni njema ama ni zenye uovu? Linganisha Luka 11:13 pamoja na Warumi 3:10-19 pia na Mhubiri 7:29.

Elewa, kiujumla, kwamba asili ya mwanadamu ni MCHANGANYIKO WA WEMA NA UOVU. Yakobo 3:9-10 na Luka 6:45.

3. Je, ulimwengu huu ni mchanganyiko wa wema na uovu? Je, matendo na maamuzi yanayoonekana kuwa ni mema mbele ya viongozi wakuu na kwa watu kwa ujumla daima huishia kwenye matokeo ya kutisha? Methali 14:12.

Je, methali hii ni ya muhimu sana kiasi kwamba Mungu aliona ni vema aipe msisitizo kwa kuirudia kuitaja tena? Methali 16:25.

Je, si ukweli kwamba kukabiliwa kwa ulimwengu leo na kujiangamiza wenyewe INATHIBITISHA kwamba MSUKUMO WA ASILI ILIYO YA UOVU ya mtu UNANGUVU kuliko msukumo wa mtu wa asili ya wema?

4. Je, kiukweli MWANADAMU ANAIJUA NJIA YA KUIFIKIA AMANI? Warumi 3:17.

Nabii mmoja wa Agano la Kale alieuelezeaje uelewa wa wanadamu juu ya maswala ya amani? Isaya 59:8.

5. Katika ujinga, chuki na uoga wao, je, watawala wa ulimwengu walimua Mfalme wa Amani (Isaya 9:6), Bwana wa utukufu? 1 Wakorintho 2:8.

6. NI NINI KINAMDANGANYA MWANADAMU aamini kwamba matendo yaishiyo kwenye mauti yataleta amani? Yeremia 17:9, 1 Yohana 2:16.

(Kumbuka kwamba katika Maandiko, moyo huzungumziwa kimapumbo kuwa ndio kituo cha akili ya mtu). Sasa je, watawala waweza kuwa wamedanganywa na TAMAA ZAO wenyewe waamini kuwa matendo yao maovu ni sahihi na yanafaa kwa ulimwengu?

Je, wanaweza kuwapotosha wanaowaongoza na kuchangia katika kuangamia kwao? Isaya 3:12, 9:16.

7. Je, PAULO ALITABIRI kwamba mwishoni mwa zama hizi, watu wangukuwa wasaliti, wavunja maagano, wenye uchu, watamanio mali na maeneo ya wenzao? 2 Timotheo 3:1-5.

8. Je, maarifa daima husababisha majivuno yaongezeke? 1 Wakorintho 8:1. Lakini upendo wa Mungu husababisha kitu gani? 1 Wakorintho 8:1.

Je, madaraka hupelekea mtu kuwa na majivuno? 1 Timotheo 3:6.

Kwa vile tunaishi katika zama za kuongezeka kwa maarifa ya kisansi, kitu kisababishacho watu wachache waweze kujikusanyia uwezo makubwa wa kiviwanda na kisayansi, je, asili ya mwanadamu itamfanya aweze kuzidi kuwa mwema na mwema zaidi ama MUOVU NA MUOVU zaidi katika siku za mwisho? 2 Timotheo 3:1,13.

9. Je, kwa sasa inawezekana, kupitia uwezo wa kisayansi na kiteknolojia, watu wenye uchu kutamani, kunyakua, na kuangamiza zaidi kuliko huko nyuma?

SHITUKA NA USAIDIE!-AMA UANGAMIE!

1. Je kutakuwepo wale WANAODHIHAKI katika siku za mwisho wakipinga kwamba Yesu hatarudi? 2 Petro 3:3, 4.

Pale mamlaka ya Mnyama itakapoinuka na kutambuliwa na Wanafiladefia waaminifu (Ufunuo 3:7-13) walio masalia ya Kanisa la Mungu, ambao watakuwa mbele katika kuitangaza Injili ya Ufalme kwa ulimwengu (Mathayo 24:14-15), je, hili litapelekea waingie kwenye mateso? Danieli 11:28-35.

Je, ustaarabu wa dunia utakabiliwa na janga la kuangamia kutokana na madikiteta vichaa? Mathayo 24:15, 22; Ufunuo 13.

2. Je, asili ya mwanadamu kimsingi imebadirika? Mathayo 24:37-39 na Luka 17:26-30.

Ijapokuwa kimsingi asili ya mwanadamu haijabadirika kuanzia siku za Nuhu, je, njia za kisayansi za kuangamizana zimebakia zilezile? Je, mataifa yanazidi kubuni na kuunda mamlaka kuu na KUU ZAIDI za kuleta amani? -- ama ni kwa ajili ya MAANGAMIZI YA HALAIKI?

3. Je wengi wa watu leo WANAHANGAISHWA na tishio la mauti litokanalo na vita vya maangamizi kugombea kuutawala ulimwengu? 2 Wathessalonike 2:9-12, Mathayo 24:39.

Je, watu WAMEAMUKA vya kutosha juu ya matukio ya ulimwengu au hata tu kuyatarajia? Je, ULIMWENGU unaendelea na mambo yake ya kila siku PASIPO KUJALI WALA KUSIKIA KILE KINACHOENDA KUTOKEA?

4. Je, jitihada za kibinadamu katika kuelimisha ulimwengu na mipango ya amani itazuia uteketezwaji? Isaya 33: 7-8.

Pale mabalozi wa amani watakapokuwa wakilia kwa uchungu—

wakati miji imeteketewa—je, hapo ndipo MUNGU ATAINGILIA KATI ili kuwaokoa wanadamu? Aya ya10.

5. Kote katika Biblia, vita inaonyeshwa kuwa ni malipo ya dhambi—iletwayo kama matokeo ya uchu ama tamaaa mbovu. Yakobo 4: 1-2.

Je, mabalozi wa mataifa wanaweza kusamehe dhambi? Je, wanaouwezo sasa wa kusitisha VITA kabisa ikome milele, ambayo ndiyo malipo ya uovu wao?

MAELEZO: Amani ya ulimwengu haiwezi kuja hadi ADHABU ya dhambi isamehewe kwa malipo sitahiki. Ni dhahiri NI KRISTO PEKEE NDIYE AWEZAYE KUSITISHA VITA VYOTE kwa vile ni yeye pekee ndiye aliyelipa malipo kamili—kifo—kwa ajili ya dhambi. Kristo alikufa ili sisi sote tusiweze kufa wakati wa maangamizi ya kutisha yajayo. Mungu ataisitisha adhabu juu ya familia ya wanadamu kwa kujiingiza mapema katika maswala ya wanadamu. Mwanee tayari alijitoa akaitwaa adhabu ya mauti, akafa badala yetu.

6. Baada ya kuingilia kati, JE, MUNGU ATAANZISHA ELIMU KWA ULIMWENGU NA KUONDOLEA MBALI CHANZO HALISI CHA VITA? Isaya 2:3-4 na Mika 4:1-4.

Badala ya kufundishwa sawa na taasisi za leo za kielimu namna ya kuunda vyombo vya kivita vya kuwaangamiza wanadamu wenzao, je, watu WATAFUNDISHWA kujizuia na kupewa NIDHAMU BADALA YA ASILI YA KIBINADAMU – ili kuiongoza busara ya ubunifu—iunde vyombo vya uzalishaji wa kiamani?

7. Je, MATAIFA muda huo yatahitaji KUKEMEWA kwa nguvu ya kimamlaka kuu? Isaya 34:2.

Je, wataelimishwa juu ya njia sahihi ya maisha—njia iletayo amani? Isaya 30:21.

Hili ndilo swala ambalo Wakristo katika zama hizi watakuwa wakisaidia kulitimiza. Hii ndiyo sababu nyingine ya umuhimu wa wewe kuisoma na kujifunza Biblia kwa sasa.

8. Je, neno la unabii ni la kuaminika? 2 Petro 1:19-21.

Je hili si faraja pale tuonapo mengi ya yanayoendelea katika ulimwengu leo?

MARDI GRAS: SHEREHE YA IBILISI?



Mardi Gras kule New Orleans (Infrogmation)

Na Bob Thiel

Mardi Gras ni kitu gani? Je, ni sikukuu ya Kikristo? Ni kutoka wapi nyingi ya desturi ziambatanazo na sherehe hii zilitoka? Je, Biblia inairidhia?

Makala hii itazungumzia kwa ufupi maswali hayo.

Mardi Gras = Jumanne ya Kunenepa

Mardi Gras ikitafsiriwa inamaanisha “Jumanne ya Kunenepa” katika Kiswahili, au “Fat Tuesday” katika Kiingereza.

Siku inayotangulia “Jumatano ya Majivu” wakati mwingine huitwa “Mardi Gras” na huhitimisha kipindi kijulikanacho kama “carnival” au “carnaval” (ambacho huchukua kati ya siku kadhaa hadi wiki kadhaa kutegemea na mila ya nchi). Kiujumla ni wakati wa kufanya tafrija na karamu pamoja na kuzama katika desturi ambazo baadhi ya Wakatholiki wanaamini kwamba zinatakiwa kuishia kwenye siku ya Jumatano ya Majivu kwa ajili ya Kwaresma.

Mkatholiki wa Kiorthodox wa kale aitwaye Arnobius (alikufa mnamo 330) alionya juu ya aina ya mifungo ambayo wapagani walikuwa wakiishika na yaonekana alikemea juu ya tafrija za Mardi Gras zinazofuatiwa na mfungo, aliasema:

Mnasemaje, Enyi wana werevu wa Erectheus? Ni nini, enyi raia wa Minerva? Nafsi inahamu ya kujua ni kwa maneno yapi mtatetea kile kilicho cha hatari kukiendeleza, ama mnayo mbinu ipi ambayo kwayo mnawapa watu mashuhuri uzima na kuwasababishia waliodhurika mauti hiyo. Hii si kutoaminiana ya uongo, wala hamshambuliwi kwa madai ya uongo: sifa mbaya ya Eleusinia yenu inatangazwa na

vyote mwanzo wake mbovu pamoja na taarifa za nyaraka za kikale, kwa ishara halisi, katika fidia, mnyotumia pale muulizwapo katika kupokea vitu vitakatifu,—” Nimefanya mfungo, na nimekunywa ukame; Nimechukua kutoka guduria la kimiujiza, na kuweka ndani ya kapu la mkeka; Nimepokea tena, na kuahamishia kwenye kikasha kidogo” (Arnobius. Dhidi ya Wapagani, Kitabu cha V, Sura ya 26).

Sikukuu ya Jupiter inatimia kesho. Jupiter, Ninadhani, hula, na ni lazima ashibishwe kwa karamu kuu, na ajazwe vema na hamu kuu ya vyakula kwa kufunga, na baada ya hapo awe mwenye njaa hadi tena mwakani (Dhidi ya Wapagani, Kitabu cha VII, Sura ya 32).

Hislop aliamini kuwa Arnobius alipoandika hayo alikuwa akifundisha dhidi ya kile ambacho baadaye kilikuja kujulikana kama Kwaresma (Babeli Mbili, Uk. 106). Pengine ni vema ikieleweka kwamba mwishoni mwa karne ya 2, Tertullian naye pia alionya dhidi ya “Wakristo” kushiriki katika matukio ambayo pia yalikuwa yanamtukuza Minerva.

Hata hivyo, Kwaresma, kikawa ndicho kipindi ambacho kanisa la Rumi liliamua kukiiga toka kwa wapagani. Papa Gregory Mkuu (Wa mwaka 540-604) akaihamisha siku ya kuanza kwake iwe Jumatano.

Kwa kuwa wale wafuatao imani ya Kanisa la Rumi wanaweza kuepuka kula nyama vitu vitamu na/ama viburudisho vingine vya kimwili wakati wa Kwaresma, wengi wao mbalimbali waliona ni wazo jema na waliamua wafanye karamu jioni inayotangulia na hapo hujihusisha na kufanya mambo ambayo hujizuia nayo siku inayofuata.

Wazo la “Mardi Gras” halikutokea kwenye Biblia.

Mardi Gras vilevile huitwa “Carnaval”

Mardi Gras vilevile huitwa Carnaval (Sikukuu ya cherekochereko ambapo watu huvaa mapambo na vinyago usoni, na kufurika mitaani) katika maeneo mengine.

Ona kifuatacho:

Pamoja na kwamba chanzo cha sherehe ya Carnaval kimegubikwa na usiri na kutokujulikana, baadhi huamini sherehe ilianza kama sikukuu ya kipagani ya kuwadia kwa majira ya vuli zamani enzi za karne za kati. Wareno waliipeleka sherehe hiyo kule Brazili mnamo miaka ya 1500, ambapo ilichukua mwelekeo wa kijadi ya huko kwa kuingizwa mavazi ya kihindi wekundu na ngoma za kiafrika. Neno lenyewe “Carnaval” yamkini linatokana na neno la Kilatini “carne vale,” yaani “kwaheri nyama”, inayoashiria mfungo wa Mila za Kikatholiki wa kujiepusha kula nyama (na vitu vingine vya matamano) wakati wa Kwaresma... (http://www.sltrib.com/travel/ci_7883824).

Chanzo cha haya si kwamba hakijulikani kulingana na toleo la sita la kitabu cha kumbukumbu ya matukio kiitwacho Columbia

Encyclopedia kinachoeleza:

Sherehe ya cherekochereko ya kijamii iitwayo “Carnival”, hususani tafrija ya kidini katika nchi za Kikatholiki itukiayo pindi tu kabla ya Kwaresma.

Tangia kipindi cha awali sherehe za carnivals zimeambatana na magwaride, maandamano ya watu waliovaa vinyago (masquerades), pageants, na aina zingine za kuabudu ambazo asili yake zimetoka kwenye ibada za upagani wa kabla ya Ukristo, hususani ibada za kizaliana (fertility rites) zilizokuwa zinahusiana na kuwadia kwa majira ya vuli na kuchepuka kwa mimea.

Mojawapo ya tukio la aina hiyo lililopo kwenye taarifa zilizohifadhiwa la sherehe za mwaka za majira ya vuli ni lile la Sikukuu ya Osiris katika Misri; iliyokuwa ikiashiria kumbukumbu ya maisha kuwa mapya iliyokuwa ikiletwa kwa Mto Nile Kujaa na Kufurika majira hayo kila mwaka. Kule Athens, wakati wa karne ya 6 K.K., sherehe ya kila mwaka ya kumwabudu muungu Dionysus ndiyo taarifa ya kwanza kuripotiwa juu ya kuanzishwa kwake.

Ilikuwa ni nyakati za Milki ya Kirumi ambapo ndipo sherehe za “carnivals” (gwaride la watu waliovaa vinyago na mapambo) zilipofikia kiwango cha juu cha ghasia na vurugu za wanajamii. Sherehe za cherekochereko mashuhuri za kirumi zilikuwa ni pamoja na ya Sikukuu za “Bacchanalia”, “Saturnalia”, na ile ya “Lupercalia”. Katika Ulaya mila ya sherehe za majira ya vuli yaletayo kuchipuka zilidumu vyema hata nyakati za Ukristo, ambapo sherehe za “carnivals” zilifikia kiwango cha juu nyakati za karne ya 14 na 15.

Kwasababu sherehe za carnivals zimezama mizizi yake kwenye ushirikina wa kipagani pamoja na desturi za Ulaya, Kanisa la Kikatholiki la Rumi halikuweza kuzisitisha na hatimaye likazipokea nyingi kati yake na kuzikubali ziwe sehemu ya maswala ya kanisa (<http://www.encyclopedia.com/doc/1E1-carnival.html>).

Mtandao wa Wikipedia unaeleza:

Sherehe ya “Carnival” ni sikukuu ambayo kwa kawaida huadhimishwa katika Ukatholiki wa Rumi na, kwa kiwango kidogo, huadhimishwa pia na jamii za Kiorthodox ya Mashariki. Maeneo ya madhehebu ya Kiprotestanti kwa kawaida hayana maadhimisho haya ya carnival ama yamezibadiri desturi zake, sawa na kwa mfano, Carnival ya wa Danish. Carnaval ya wa Brazil ndiyo ilyo ya muda mrefu zaidi kwa sasa, lakini miji mingi na mikoa ulimwenguni kote husherehekea kwa matukio makubwa na yajulikanyo. Haya ni pamoja na lile la “Carnevale” la Venice, Italy, lile la Santa Cruz de Tenerife, Canary Islands; la Torres Vedras, Portugal; Rio de Janeiro, Brazil; Rijeka, Croatia; Barranquilla, Colombia; na Trinidad na Tobago. Katika Marekani (United States of America), Sherehe ya Mardi Gras iliyo mashuhuri zaidi ni kule New Orleans, Louisiana, na Mobile, Alabama,

zinazoanzia tangia enzi za makoloni ya Ufaransa na Hispania katika maeneo hayo...

Kichocheo kwa tafrija za carnival kidehuri kilikuwa kwamba ziliruhusu kuburudika na kula na kunywa kwa mara ya mwisho kabla ya mfungo wa Kwaresma. Kipindi cha mfungo wa Kwaresma kiliambatana na kujizuia kula vinono, kufunga na matendo ya kitubio. Kwa kawaida, tafrija hazikufanyika muda huo na watu walijuzuia kula vyakula vinono, kama vile nyama, na wakati mwingine, maziwa, mafuta na sukari. Siku arobaini za Kwaresma zinasaidia kuainisha muda wa kila mwaka wa kumgeukia tena Mungu na kurejea kwenye nidhamu ya kidini.

Pamoja na kwamba hii ni sehemu muhimu ya kalenda ya Kikristo, baadhi ya desturi zilizomo kwenye “carnival” zimekuwepo hata kabla ya nyakati za Ukristo. Sherehe za kale za Kirumi za Saturnalia na Bacchanalia yaonekana ziliingizwa katika Carnival ya Kiitalia. Sikukuu ya Saturnalia, mwanzo wake, yaonekana ilitokana na sherehe ya Kigiriki ya Dionysia pamoja an tafrija za nchi za Mashariki. Wakati tafrija na sikukuu za kipindi cha karnime za kati kama vile “Corpus Christi” zilikuwa ni sherehe zilizoanzishwa na kanisa, carnival nayo iliingiza desturi zake humo katika jadi za kipindi cha karne za kati. Desturi nyingi zilizomo kwenye sherehe za carnival katika sehemu mbalimbali zimeundwa kutokana na vionjo vilivyokuwepo kabla ya Ukristo, kwa mfano desturi ya uvaaji wa mapambo na vinyago iliyotokana na cherekochereko za carnival ya Wa-Swabian-Alemannic.

Ndiyo, wengi miongoni mwa Wakatholiki, waumini wa Kiorthodox ya Mashariki, na wengine watashiriki katika cherekochereko zinazoambatana na sikukuu ya carnival. Wengi pia wataishika Kwaresma!

Hapa kuna ambacho makala ya American Catholic inaeleza kuhusu hili:

Mardi Gras, inayomaanisha “Jumane ya Kunenepa”, imeongezeka umashuhuri katika miaka ya hivi karibuni na kuwa sherehe ya vurugu na wakati mwingine ya tukio la ki-hedonistic zaidi (imani kwamba mtu anatakiwa kujiburudisha kwa tafrija na vinywaji) ...Carnival ni neno la Kilatini carne vale lenye maana ya “kwaheri nyama”. Sawa na sikukuu nyingi za Kikatholiki na sherehe za mwaka, yaonekana mizizi yake imetokana na mila za kabla ya Ukristo zilizoendana na majira hayo. (Catholic Roots of Mardi Gras. American Catholic. <http://www.americancatholic.org/features/mardigras/>).

Kimsingi, hii ni sikukuu ya kipagani ambayo wakatholiki waliiga na kuipokea kama mtego wa kujipatia waumini. Wanasherehe hula kwa ulafi (ndicho chanzo cha jina “jumane ya kunenepa”) kabla hawajaanza mfungo uitwao siku hizi Kwaresma (Lent) – ambayo nayo imeingizwa toka kwenye upagani. Maandamano ya magwaride yenye wanawake waliovalia mavazi ya nusu uchi ni swala la kawida kwenye carnival hizo.

Kiukweli, cherekochereko za Mardi Gras si za Kibiblia, hata kama zinapendwa sana.

Kwaresma, ambayo nayo haikutokana na Biblia, ndiyo inayotumiwa kama sababu ya watu kufanya tafrija na cherekochereko za kelele, ulevi na ulafi duniani kote, ambazo husitishwa usiku utanguliao mfungo huo.

Vinyago vya Ndege na Kubaki Nusu Uchi

Wengine huvalia aina tofautitofauti za vinyago usoni na mavazi mbalimbali kusherehekea Mardi Gras.

Katika maeneo mengine, nimejionea tabia ya wanasherehe ya Mardi Gras kuvalia vinyago vya ndege usoni. Jionee taarifa fulani kuwahusu:

Ndwele kubwa zaidi (Kifadulo – “Black Death”) ya mwaka 1348 - 1351 ilipelekwa Ulaya na mabaharia wa “Genoese sailors” kutoka nchi za Mashafriki...Iliaminika kwamba kinyago chenye mdomo wa ndege kilichowafanya madaktari waonekane kama miungu ya kale ya Kimisri kilisaidia kuufukuza ugonjwa huo. Kazi ya mdomo wa ndege ilikuwa ni kuwalinda madaktari dhidi ya harufu mbaya ya wagonjwa. Mbele ya mdomo wa ndege kwenye kinyago yalijazwa majani ya mimea yenye harufu kali yaliyofanya kupumua ndani ya harufu mbaya ya wagonjwa iwe rahisi. Madaktari wa ugonjwa huu walikuwa wakitafuna vitunguu saumu muda wote walipokuwa mbele ya wagonjwa hao kama kinga, na hivyo mdomo wa ndege uliwakinga wengine dhidi ya harufu kali ya vitunguu saumu. Zaidi ya hapo, madaktari waliweka ubani kwenye sponji na kuiingiza sponji hiyo ndani ya pua na masikio yao. Hii ilisaidia kuzuia kuishiwa hewa kutokana na mchanganyiko huo wa harufu kali mbalimbali, za kutoka kwenye mdomo wa ndege wa kinyago, masikio na pua. Kinyago pia kilikuwa kimewekewa kioo ili kuyalinda macho na kuwezesha kuona. Koti lililopakwa nta ama oili lilihitajika kuvaliwa na daktari kabla hajaenda kumhudumia mgonjwa ili aweze kuepuka kugusana na kuambukizwa ugonjwa huo. Mara nyingi nguo zao zililowekwa kwenye mchanganyiko wa “camphor”, oili na nta. Kwa kweli ilisaidia kuzuia kuambukizwa ugonjwa huo hatari, kuumwa na wadudu—viroboto, na kulinda dhidi ya magonjwa yaenezwayo kwa njia ya hewa, ijapokuwa watu walikuwa hawalijui hili kwa wakati huo. Vazi hilo lilikamilishwa kwa kuwekewa kofia ya ngozi yenye kizuizi kulichofunika kabisa mwili kati ya mwunganiko wa kinyago cha kichwa na vazi la mwili. Mavazi hayo yalitofautiana kulingana na eneo na uwezo wa kifedha wa madaktari (<http://english.pravda.ru/society/stories/11-10-2013/125877-plague-0/>).

Gundua hili kwamba vinyago vya ndege vilitumiwa na madaktari enzi za Karne za Kati, ijapokuwa ziliigwa kutoka kwa miungu ya Kimisri. Wengi wa hawa madaktari pia walidai kuwa na imani ya ama Ukatholiki au U-orthodox ya Mashariki.

Wengine ambako sikukuu ya Mardi Gras/Carnaval huadhimishwa:

Carnival...siku tano katika mwaka za burudani ya miziki, kulewa na ulaji nyama...Mfalme Momo huanzisha Carnival, sherehe ya kupayuka iliyowazi kwa kila mtu ambapo ulafi, ulevi na ngono huhamasishwa na utaratibu wa kawaida hugeuzwa: wanaume huvalia kama wanawake...Zaidi ya hapo kunakuwepo na siku mbili za vikundi vya gwaride la ngoma za samba na pardi na dansi ya umati mkubwa yenye mavazi ya gharama ambako matajiri hutumia pesa nyingi kununua nguo za nusu uchi wanazozivaa kwenye tafrija hii wakiwa miongoni mwa kundi la matajiri wenzao, Jiji la Rio wakati huo wa Carnival ipitayo mitaani iliyo kwa ajili ya wote hutapakaa watu wengi kuliko wakati wowote mwingine. http://www.silive.com/news/index.ssf/2011/03/rio_celebrates_as_carnival_ope.html.

Kwa kadri wenyeji wanavyojionea, watu wakijinyea, kujikojolea na kujitapikia hovyo – na kushuhudia harufu mbaya ya marundo yao ya matapishi na miharisho – hilo ndilo limekuwa kwa kiwango kikubwa sehemu ya sherehe za Carnival ambako wanawake walio nusu uchi, vikundi vya ngoma za samba, chereko za wanawake waliovalia wakipita kimaonyesho, watu waliojipaka rangi mwilini, na waliolewa na wageni waliojianika miili juani (sun-burned). (http://www.huffingtonpost.com/2013/02/06/brazil-pee-patrols-carnival-public-urination_n_2631945.html?utm_hp_ref=world).

Mardi Gras siyo tafrija ya juma-zima kwa wenyeji wa New Orleans pekee wapendao kwenda kwenye baa, mamillioni ya watu toka kote Marekani huja kuisherehekea tafrija hii iliyo maarufu.

Mardi Gras ni mashuhuri kwa mikusanyiko ya watu walio nusu-uchi, pati zenye fujo, na unywaji wa pombe nyingi...

Sikukuu hii inayoitwa ni ya Kikristo hutumika kama fursa ya mwisho ya kujiburudisha kabla ya Kwaresma na kujinyima vinono hadi pasaka (Easter). Watu hujiburudisha kwa pati na anasa nyingi wakati wa juma liishialo kwenye Kwaresma na Jumatano ya Majivu. Kwa kawaida hii huambatana na mkusanyiko mkubwa wa watu waandamano mitaani kwa cherekochereko, baadaye hufuatiwa na tafrija katika vikundi binafsi mbalimbali na miziki ya watu waliovalia mavazi ya rangi za dhahabu, kijani, hudhurungi, kumaanisha uwezo, imani na haki.

Raia hujichia vilivyo, na kutupilia mbali aibu na unyenyekevu, wakati huu wa siku chache za majira ya Carnival. Wanawake kimsingi hubaki uchi na kujipamba kwa shanga za rangi mbalimbali, ambapo huandamana mitaani wakijionyesha, na zaidi hubaki nusu uchi kabisa baadaye waendapo kwenye mabaa. Wanawake kukosa aibu na wanaume hukosa mipaka. (<http://www.fourthestatenewspaper.com/mobile/off-the-wall/mardi-gras-unexposed-mayhem-1.2781767>).

Mardi Gras kamwe si sikukuu ya Kikristo. Ni vema ieleweke kwamba utumiaji pombe kuzidi mpaka, uvaaji mavazi ya kike ama ya kiume kinyume cha maumbile yako, na ubakiji uchi haviendani kabisa na maelekezo ya Biblia juu ya kuwa na kiasi:

“8 Basi, nataka wanaume wasalishe kila mahali, huku wakiinua mikono iliyotakata pasipo hasira wala majadiliano; 9 Vivyo hivyo, wanawake na wajipambe kwa mavazi ya kujisetiri, pamoja na adabu nzuri na moyo wa kiasi...” (1 Timotheo 2:8-9).

“13 Kama tunaohusika na mchana, na tuenende kwa adabu, si kwa ulafi na ulevi, si kwa ufidia (tama mbaya) na uasherati, si kwa ugomvi na wivu. 14 Bali mvaeni Bwana Yesu Kristo, wala msiuangalie mwili, hata kuwasha tama zake” (Warumi 13:13-14).

Wakristo hawapashwi kushiriki mambo ya kipagani wala ubatili na kuyainua.

Wengine Huiita Aina kama hiyo kuwa “Carnival ya Ibilisi”

Hapa tunakuletea ripoti mbili kuhusu aina hiyo kule Bolivia:

Carnival ya Ibilisi – Devil’s Carnival (La Diablada)

Frommer’s

Lini: 19 – 23 Feb 2009 (Kila Mwaka), Wapi: Oruro

Kila ifikapo majira ya vuli, Oruro huzama kwenye sherehe ya carnival. Mapambo ya mavazi yatumikayo kama maonyesho ni ya ajabu na yanachukua sura yoyote toka kufanana na wachungaji wa wanyama waitwao llama hadi hata kuvalia sawa na mavazi ya michezo ya Wahindi Wekundu wa Amazon yenye kofia za manyoya. Mchanganyiko wa rangi mbalimbali, vinyago vya kuvaa usoni vya kutisha, miziki, dansi na milipuko ya fataki vitakuacha mdomo wazi na ukikodoa macho.

Moja wapo ya matukio ya siku hiyo makubwa ni wale wacheza dansi wa ibilisi, ambayo ni jadi iliyotokana na aina fulani ya ibada ya kumwabudu ibilisi. Oruro ni mji wa uchimbaji madini na wenyeji, ambao hutumia mda mwingi sana kwenye mashimo ya migodi, waliamua kumkumbatia muungu wa ulimwengu wa chini ya ardhi (kuzimu). Mila za Kikristo zinaashiria kwamba hii inaweza kuwa ni ya ibilisi na hivyo waumini wa Oruro waliamua kumukumbatia Shetani, au Supay, kama muungu wao.

Hufanya mitambiko kwa ibilisi mara kwa mara ili kuomba wawe na uhakika wa usalama wao wawapo migodini na hii dansi ya ibilisi wakati wa “carnival” imetokana na imani yao kwa Shetani kuwa ndiye mlinzi wao wawapo chini ya ardhi. (http://events.frommers.com/sisp/index.htm?fx=event&event_id=5769).

Sikukuu ya Kukufanya Uandamane

FF, UK – Feb 18, 2009.

Lini: Siku 10 za karibu na Jumatano ya Majivu.

Wapi: Oruro, Bolivia.

Nini: Sherehe ya Carnival ya Oruro ndiyo sikukuu za mwaka kubwa kuliko zote Bolivia ambayo hukusanya washiriki wakadiriwao kufikia watu 400,000 kila mwaka, hii ikichochea na chereko chereko zake za kipekee, ikiwemo La Diablada –Dansi ya Ibilisi.

Mistari ya maandamano ya watu ifikiayo kilomita 4 hufanyika kwenye Jumapili itanguliayo Jumatano ya Majivu ambapo huwa kuna vikundi vya waburudishaji wengi mno kiasi ambacho maonyesho huchukua hadi masaa 20. Chereko chereko hii hufuatia gwaride la watu waliovalia mavazi ya mapambo itwayo San Miguel, ambapo baada ya hilo hufuata maonyesho ya watu waliovalia vinyago vya kishetani usoni na vya wanyama na vitu vingine vya kutisha.

Shetani mkuu, Lucifer, akiwa ametengenezwa kama sanamu kubwa, huvalishwa mavazi ya gharama na yaliyojaa mapambo, na hutembezewa akiwa kavalishwa joho la halili akiwa kabebwa kwenye machela ya dhahabu, na kinyago usoni. Maandamano haya yakimalizika, siku ifuatayo, watu hupita wakiwa wamejipamba kwa shanga na madini ya kumeremeta ambapo baadaye hufanya matambiko kwa muungu mmiliki wa madini ya ardhi, aitwaye El Tio.

Pale maandamano yafikapo kwenye uwanja wa mpira wa mji, hufanyika maonyesho makubwa ya vita baina ya wema na uovu – Uu; baada ya kubainika kwamba wema umeibuka mshindi dhidi ya uovu, hapondipo wacheza ngoma huweza kwenda nyumbani kupumzika. Sikukuu na chereko chereko huendelea kwa wiki nzima hadi ifike hitimisho kuu kwenye siku ya Jumatatu baada ya Jumatano ya Majivu, ambayo hujulikana kama Dia del Agua – “Siku ya Maji” – ambapo kila mmoja huloweshana na wenzake mitaani kwa mabomu ya maji. (<http://www.femalefirst.co.uk/music/events/Festivals+To+Get+You+Going+Next+Week-7201.html>).

Maadhimisho kwa ajili ya ibilisi na/au mipango yake kwa kiwango kikubwa hayafai kwa wale wanaokiri kumfuata Yesu. Kristo hakuwahi kuadhimisha chochote kifananacho na Mardis Gras ama Carnival, na wala wanafunzi wake nao hawakuwahi kuadhimisha au hata wafuasi wao waaminifu. Katika nyakati za Majira ya Vuli, wao waliadhimisha sikukuu kama Pasaka (Passover siyo Easter) na Pentekoste; Biblia iko wazi juu ya hili (Luka 2:41-42; 22:7-13; Matendo 2:1).

Kiukweli, si kwamba tu “carnival” haimo kwenye Biblia, bali hata Jumatano ya Majivu nayo pia haimo wala Kwaresma (ambazo hazikuwepo hadi baada ya karne nyingi baada ya Mitume wa awali kuwa walishafariki); hivyo hakuna moja wapo

iliyo sehemu ya desturi za Kanisa la kweli la awali. Wala hazimo katika DESTURI za Kanisa la Continuing Church of God leo (tunaadhimisha sikukuu zilezile ambazo Yesu na Mitume wake walizishika, kama Pasaka (Passover siyo Easter) na Pentekoste.

Mardi Gras mara kwa mara huambatana na ulevi, ulafi, pamoja na matendo mengine ambayo Biblia inayakemea. Haipaswi kabisa kuchukuliwa kama kitu ambacho Wakristo wa kweli wangeweza kushiriki.

Desturi ziambatanazo na Mardis Gras na Carnival zinamwanzo wake kwenye enzi za “kabla ya Ukristo” na wala hazikuhalalishwa kwenye Biblia. Kwa sehemu, kutokana na watu kuadhimisha, kumewafanya washindwe kuelewa mpango wa Mungu wa wokovu kwao.

Pengine wale wanaomkiri Kristo wanapaswa kuufuata mfano wake kwa kuadhimisha sikukuu zilezile alizo adhimisha yeye wakati wa majira ya Vuli, kama vile Pasaka (Passover siyo Easter).

Yesu Alimaanisha Nini –

“NATAKA REHEMA, WALA SI SADAKA”?

Awali ilichapishwa kama: Yesu Alimaanisha Nini – “Nataka Rehema, Wala Si Sadaka”? Gazeti la Good News, Julai – Septemba 1973, Ukurasa wa 13-15.



(Photo na Nikodem Nijaki)

Na Charles F. Hunting

Je tunajua kwa usahihi kile alichomaanisha? Kristo alisema, “Nendeni MKAJIFUNZE maana yake maneno haya” (Mat. 9:13). Kuyaelewa yaweza kuwa ndiyo uzima wako wa milele!

Lengo letu—hasa ni nini? Je, lina ukungu, haliko dhahiri, si kitu kielewekacho wazi, kama vile “kuingia kwenye Ufalme,” “kuonyesha upendo,” ama “kuifanya kazi ya Mungu”?

Kila mmoja wetu amnapaswa kuwa na lengo lililo wazi, la kudumu muda wote kuliko hayo. Lengo lililo wazi na linaloeleweka kiasi kwamba tunaweza kujua kwa kujiamini kwamba tunayatimiza matakwa ya Mungu— kusudi lake kwa maisha yetu.

Pointi ya Kuanzia

Kila mmoja anataka aishi milele. Lakini kwa vile sisi tu wanadamu wa kimwili tu sote tunakabiliwa na mauti.

Kifo ni ukweli wazi usiopingika. Sawa na Daudi alivyosema, maisha yetu ni “mafupi kama pumzi” (Zab. 39:5). Leo tupo kesho tumeondoka.

Mauti ni hatua ya mwisho katika maisha haya – kisha hatuendelei kuishi tena baada ya hapo. Hakuna kilicho cha kimwili kinachodumu. Tunaisha.

Lakini roho hudumu. Hivyo lengo letu kuu linapaswa liwe la kudumu kiroho.

Kudumu Kiroho Inamaanisha Nini

Liangalie hili kwa mtazamo huu. Ebu tuchukulie unataka usikie muziki, hivyo unatunga wimbo. Kisha unawaajiri wapiga mziki wa ala na muongozaji. Baadaye unarekodi ala zao kwa njia ya chombo cha kurekodia (Tape Recorder).

Baada ya hapo wapiga ala wanatawanyika. Karatasi ya muziki inateketezwa. Chochote kilichotumika kutengeneza zile sauti nzuri zinakuwa zimetoweka. Lakini kanda nzuri ya jitihada zote za kuupiga wimbo na mziki huo inasalia. Kanda hiyo inaweza kusikilizwa kwenye cassette player wakati wowote.

Katika hali kama hiyo, roho iliyo ndani ya mtu ni recordi ya kiroho ya kila mmoja wetu. Hiki ndicho kinachodumu tufapo.

Mungu aliweka hii roho ndani ya mtu kwa kusudi kuu na maalum. Ikiungana na akili zetu za kimwili, hutuwezesha kutafakari, kubuni, na kuunda. Hutupa uwezo wa kumtafakari na hata kumtamani Mungu mwenyewe. Na humpa Mungu rekodi ya mienendo yetu, utu wetu, ufahamu tuliojipatia, kwa ujumla tabia zetu kamili zilivyo— vyote vile vinavyotufanya SISI tuwe – baada ya kufariki kwetu. Kile kilicho cha kimwili hufa, huoza na kuharibika, lakini roho iliyoko ndani ya mtu hubakia pasi kuharibika, milele.

Lakini ni kwa nini Mungu huhitaji abaki na rekodi, taarifa? Jibu ni kwamba Mungu anakusudia “kuisikiliza” tena, “kuitengeneza tena”, kuijenga upya – kutufufua – sawasawa kulingana na mpangilio wa kile maisha yetu ya sasa yametuandaa kuja kuwa – mtu wa nafsi, mwenye mwelekeo uleule, mwenye tabia ileile. Na hivyo kipengele cha kimsingi cha sisi tulivyo kitakacho dumu baada ya kufariki kwetu ni TABIA zetu. Isipokuwa tu sasa tutaumbika kuwa wa mwili wa kiroho kamili.

Sasa ni kipi kinachohifadhiwa kwa upande wako? Tafakari kabla ya kujibu. Vyovyote vile kitakavyokuwa, ni lazima kitambuliwe na Mungu kuwa ni kitu fulani ambacho amekikusudia kidumu milele – la sivo, “hataisikiliza” tena rekodi itakayohifadhiwa iwapo haitakuwa ni ya kukuwezesha kufufuliwa ili ujangwe upya upate maisha ya milele.

Na hapa ndipo ambapo tatizo lilipo. Baadhi yetu tutautimiza unabii wa kutisha wa kutotambuliwa upatikanao katika Mathayo 7:21-23, ambako Kristo alisema: “Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakaye ingia katika ufalme wa mbinguni.... Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana ... ndipo nitawaambia dhahiri, Sikuwajua ninyi kamwe...”

Kazi za Kimwili Siyo Kigezo

Je, umegundua kitu fulani chenye kutisha sana katika maneno haya? Kristo hapa alikuwa akizungumzia juu ya wale waliokuwa wamemtambua na walikuwa wanamuita Bwana na Mwokozi sawa kama tufanyavyo sisi. Hawa walimjua kuwa yeye ndiye Masihi. Lakini Kristo yeye hawajui. Kashindwa kuwatambua. Anatafuta kitu fulani katika roho zao ambacho kashindwa kukiona. Hivyo basi kutokana na hilo hawezi kuipiga cassette ya rekodi zao za uzima wa milele.

Tunaishika Sabato, tunatoa zaka, tunazishika Sikukuu Takatifu za mwaka, tunaweza kuongoza nyimbo katika ibada ama

kufungua au kufunga ibada kwa maombi, ama hata kuwekewa mikono kuwa mashemasi. Fursa hizi zaweza kutufanya tuamini kwamba tuko njiani kuelekea kuingia kwenye Ufalme.

Yawezekana hata tukawekewa mikono kuwa watumishi katika huduma ya Yesu Kristo, tukahubiri, tukawea wagonjwa mafuta na hata wakapona, na hata tukakemea na kutoa pepo! Je, hudhani kwamba kufanya haya yote ni ishara wazi ya mtu wa Mungu, ambaye yu katika safari ya kuingia kwenye Ufalme wa Mungu?

Lakini soma kile ambacho Kristo alisema: “wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukutoa unabii kwa jina lako? Na kwa jina lako hatukutoa pepo? Na kwa jina lako kufanya miujiza mingi?” (Aya ya 22).

Je, linakuelea hilo? Hawa wamefanya yote ya mambo ambayo wengi wetu tungechukulia kuwa ndiyo mhuri wa mwisho wa kukubaliwa na Mungu. Wametenda kazi kuu – wamehubiri kwa msisimko, wamewaponya wagonjwa, na wakatoa pepo.

Lakini si kwamba Mitume waliponya wagonjwa na kufukuzwa pepo – hata kabla hawajajazwa na Roho ya Mungu? Je, si kwamba hata Yuda Iskariote naye aliyafanya haya yote? Ndiyo waliyafanya! Na hata Wayahudi wanadini wa kipindi cha Kristo nao pia waliyafanya (Mat. 12:27).

Sasa wewe unayo fursa ipi? Wewe ni mshiriki wa kawaida wa Kanisa. Pengine umechukua kozi ya uongozi wa kanisa japo bado huna “nafasi yoyote”. Je, umefeli? Pengine – lakini si kwa sababu haukuwekewa mikono kuwa mchungaji au kupewa jukumu la kutembelea washirika. Iwapo hayo yangekuwa kweli, ingekuwa vipi kwa wanawake walio katika Kanisa ambao hawana nafasi hata ya kuongoza uimbaji wakati wa ibada wala kufungua au kufunga ibada kwa maombi, ambao majukumu yao makuu ni maswala ya nyumbani kwao tu?

Ebu na tuelewe jambo fulani! Mchango wako wa shughuli za kimwili siyo kile kinachokuhakikishia kupokea kwako uzima wa milele katika Ufalme wa Mungu!

Kumbuka Mathayo 5:3-7. Yesu alisema: “Heri walio maskini wa roho: kwa maana ufalme wa mbinguni ni wao.... Heri walio wanyenyekevu.... Heri wenye njaa na kiu ya kutenda haki. ... Heri wenye rehema...” n.k.

Gundua kwamba vyote hivi hapo juu ni sifa (mitazamo) ya nafsi aliyonayo mtu– ihusianayo na tabia. Na hizo ndizo sifa zinazotakiwa awe nazo mwana wa milele wa Mungu.

Washika—Amri Wasiofaulu!

Kijana mmoja alimwendea Yesu na kumwuliza, sawa na sisi sote tuulizavyo: “Nifanye nini nipate kuurithi uzima wa milele?” (Marko 10:17). Elewa kwamba alienda kwa mtu sahihi, sawa na wengi tufanyavyo. Kristo alimpa jibu lilelile tunalolijua: “Wazijua amri...” (Aya ya 19).

Kijana alimwambia Yesu kwamba alikuwa amezifuata amri na kuzishika tangia utoto wake. Kisha Kristo alimpenda kijana

huyo. Akatamani amsaidie. Lakini kulikuwepo tatizo, na Kristo alijua wazi kwamba jambo fulani halikuwa sawa. Jambo hilo halikuwa la kimwili; lilitajwa tu kimwili, lakini swala lenyewe lilikuwa ni tatizo la kiroho. Mtu huyu alikuwa na nafsi iliyokuwa ikitamani. Hivyo sasa alikuwa ni mshika—amri asiye faulu, sawa na walivyokuwa Waisraeli waliojaribu kuzishika amri za Mungu enzi za Musa.

Kuhusu Israeli ya kale Mungu alisema: “Laiti wangukuwa na moyo kama huu ndani yao siku zote, wakunicha na kushika amri zangu zote siku zote ...” (Torati. 5:29). Kwa maneno mengine, kulikuwepo na upungufu wa kiroho – kukosekana kiroho – kulikowazuia washindwe kuelewa maana halisi ya kiroho ya sheria kuu za Mungu. Lakini ndugu, hatupaswi kuwa na upungufu huo; Tunapaswa tuwe na Roho ya Mungu katika nafsi zetu. Sheria za Mungu ni za kiroho, na kupitia Roho yake ndipo tunaweza kuzishika kiukweli sheria hizo katika kusudi lake la kiroho.

Aina ya Nia Tunayotakiwa Kuisaka

Jionee swali muhimu lililoulizwa katika Mika 6:6-7:

“6 Nimjie BWANA na kitu gani na kusujudu mbele za Mungu aliyetukuka?7Je, BWANA atafurahishwa na kondoo dume elfu, au mito elfu kumi ya mafuta?” Je, Mungu atafurahishwa na sadaka za kuteketezwa (kazi za kimwili)? Je, tutapata kibali kwa Mungu kwa kutoa zaka kubwa na sadaka?”

Sasa ebu jionee jibu la kushangaza katika aya ya 8:

“8Amekuonyesha yaliyo mema, ee mwanadamu. BWANA anataka nini kwako? Ila kutenda kwa haki, kupenda rehema na kwenda kwa unyenyekevu na Mungu wako”

Hiki ndicho Mungu anachohitaji: Anataka wewe “upende rehema”. Je swala hilo lina umwili wowote juu yake? Ukweli halina. Hivyo jitahidi kuisaka roho ya rehema.

Je, unakuwa na furaha pale mtu anayestahili adhabu kali anasamehewa na hawajibiki kulipia hatia ya dhambi? Je, unauhakika?

Inatokea nini pale mtu anapokuwa amekukosea wewe? Je, unakuwa na matarajio ya siri moyoni kwamba wataadhibiwa – kwamba watawajibika kulipia hatia yao ya kukusingizia ama kuumiza? Tunapaswa tufikie kuwa na roho yenye rehema/huruma ambayo inapenda daima kuona watu wakisamehewa na kuachwa waepuke malipo ya adhabu za makosa yao walizostahili. Maana hii ndiyo roho ya Kristo! Hii ndiyo rula ya kiroho ya kimawazo ambayo tunaweza kuitumia kupima na kuchunguza roho zetu katika kila tendo la maisha yetu.

Ukuu wa Mungu

“Hili ndilo asemalo BWANA: “Mbingu ni kiti changu cha enzi, nayo dunia ni mahali pa kuweka miguu yangu: Iko wapi nyumba mtakayojenga kwa ajili yangu? . . . (Isa. 66:1.)

Kijumla, Mungu hapa ansema, “Upana wote wa dunia na anga lake ni langu. Dunia ambayo kwenu ni kubwa mno ambamo ndani yake hamjui kikomo, kwangu mimi ni kama vile kishemum unachoweka tu unyayo wa mguu wako katika nyumba yako. Hii ni sehemu tu ya ukuu wangu. Sasa basi ni lipi muwezalo kulifanya kwa ajili yangu?”

“2Je, mkono wangu haukufanya vitu hivi vyote . . .” (Aya ya 2) – tazameni ni finyu kiasi gani jitihada zenu za kimwili ukilinganisha na upana mkuu wa uumbaji wangu katika nchi na anga na uwezo wake usiopimika!

Je tunaweza kutenda lolote lilinganalo na haya? Ukweli hatuwezi. Lolote la kimwili tuwezalo kufanya ukilinganisha na yote ambayo Mungu ameyafanya kwa ujumla, yetu ni utupu.

Lakini pamoja na udhaifu wetu, Mungu bado anahaja ya kutujua, kututambua na hatimaye anataka atumie rekodi za taarifa zetu za roho – iliyo—ndani ya mtu kwa sababu ya kitu kimoja. Anahitaji kuziangalia akitarajia (ama akiwa na “matarajio”) kwamba pengine kila mmoja wetu ikiwa yu “mpole na mwenye roho iliyopondeka, atetemekaye asikiapo neno (la Mungu)” (Isa. 66: 2b). Kristo alisema kwamba Mungu anawatafuta wale wanaomwabudu katika roho na na katika ukweli (Yohana 4:24).

Je, umeona lolote hapa lihusikanalo na matimizo ya kimwili? Wala si uwezo wa kifikra ama kutokuwa nao, wala si uasili wa taifa la mtu, ama jinsia yake, wala si umasikini alionao haviwezi kumfanya ashindwe kufikia mambo ambayo Mungu anayatarajia watu wawe nayo. Mlemavu aliye fukara wa kutupwa bado anaweza kuwa na roho ya unyenyekevu na iliyopondeka, kwani Mungu anahitaji hali fulani ya kiroho.

Hivyo kuipata na kuistawisha tabia hii ya kiroho ndilo linalotakiwa kuwa swala letu la kila siku, la kujibidisha saa—baada ya—saa kama lengo kuu katika maisha yetu.

Musa Alielewa

Musa ataingia kwenye Ufalme wa Mungu si kwa sababu ya yale aliyoyatenda kimwili, lakini ni kwa sababu “alikuwa ni mpole mno, kushinda wanadamu wote waliokuwepo kwenye uso wa ulimwengu” (Hes. 12:3).

Wapole wataitawala dunia (Mat. 5:5). Je, wewe nawe unaweka jitihaha katika kulifikia lengo la kuwa mpole? Usidanganyike. Siyo vigumu kufahamu iwapo wewe ni mmoja wa watu wapole.

Upole ni tofauti kabisa na fikra za unyonge. Mtu ambaye ni mpole ni mtu afundishikaye kwa urahisi. Ni mtu asiyechukia marekebicho, pasipo kujali yanatokea wapi. Hautaikuta roho ya ukali, isiyopindika ama ipendayo kupinga ndani ya mshika sheria aliye wa kiroho. Mtu aliye mpole familia yake humwendea kwa urahisi, hata marafiki na wachungaji pia.

Musa alipokea maonyo na maelekezo toka kwa mtu aliyekuwa na wadhifa mdogo kuliko yeye. Ijapokuwa alikuwa na uzoefu mkubwa katika serkali kama kiongozi katika jumba la kifalme la Farao pamoja na uwezo usio kifani ambao Mungu alikuwa ameuonyesha kupitia kwake, lakini pale Babamkwe wake

alipomwendea na kumweleza kwamba alikuwa amekosea, Musa alimsikiliza na alijifunza (Kut. 18:13-27).

Hakufuata tabia ambayo baadhi yetu huionyesha pale mtu aliye mdogo kiumri kuliko sisi anapotoa mahubiri, ama kutupa ushauri. Musa hakuwa mtu afuataye maoni yake mwenyewe, ama aliyejiinua kutokana na madaraka yake makubwa, au kutokana na umri wake ama kutokana na yale aliyokuwa kayafikia.

Je, Musa alikuwa ni mwenye huruma? Pale Miriamu alipo pigwa kwa ukoma shauri ya kumpinga Musa, Musa alimlilia Mungu amponye Miriamu maramoja (Hes. 12). Je, huu ndiyo ungekuwa mtazamo wetu?

Kwa Nini Daudi Atatawala

Upole, roho iliyopondeka na yenye toba, pamoja na sifa zingine zote za Mathayo 5 ni baadhi ya vipengele kutoka kwenye rula tuwezayo kuitumia kujipima sisi wenyewe tulivyo mbele ya macho ya Mungu. Haitoshi kulifanya hili kuwa kama kitu cha mazoea ya siku ya Sabato tu, bali inapaswa kuwa ndiyo tabia yetu ya kudumu, lengo letu la daima la kila tendo letu – iwe ni katika uhusiano wetu na waajiri wetu, wake zetu au waume wetu, watoto wetu ama binadamu mwingine yeyote.

Ni nafsi ya aina hii pekee ndiyo itakayoweza kumudu kuutumia uwezo mkuu ambao Mungu anaenda kuuweka kwenye mikono yetu.

Je, wewe ungelipenda mtu mwenye wivu, kijicho, mwenye kisasi akutawale? Yamkini hapana. Basi hata na Mungu hamtaki mtu wa aina kama hiyo.

Je, wewe kimawazo unayo njaa na kiu ya kutenda haki (Mat. 5:6)? Kwa hisia kali, Daudi alisema: “18Yafungue macho yangu nipate kuona mambo ya ajabu katika sheria yako” (Zab. 119:18). Kwa nini? Kwa sababu Daudi aligundua kwamba usalama wake haukuwa katika kutembea mbali na amri za Mungu. Alitambua kwamba ikiwa njia zake zitaongozwa na sheria ya Mungu, asingefanya makosa na kuaibika (aya ya 6, na ya 10).

Lakini ni lipi alilolifanya Daudi pale alipo tukanwa na kutupiwa mawe? Je, aliamua kulipiza kisasi? Jionee nafsi ya kiroho ikiwa kazini pale Abishai, mlinzi wa Daudi, alipomwuliza ikiwa anamruhusu akamwangamize mtu huyo aliyestahili kifo. Daudi alijibu: “10 Ikiwa analaani kwa sababu BWANA amemwambia, ‘Mlaani Daudi,’ nani awezaye kuuliza, ‘Kwa nini unafanya hivi?’” Mwacheni, acha alaani, kwa maana BWANA amemwambia afanye hivyo. 12Inawezekana kwamba BWANA ataona dhiki yangu na kunilipa mema kwa ajili ya laana ninayopokea leo.” (II Sam. 16:10-12). Je, wewe ungetenda namna hiyo iwapo ungejikuta kwenye hali hiyo?

Daudi atakuwa mmoja wa wanafamilia ya Mungu si kwa sababu ya yale aliyoyatenda kupitia jeshi lake ama uwezo wa kimwili, bali ni kwa sababu ya nguvu zake kubwa kiroho pamoja na nafsi yake ambayo Mungu na Kristo wataitambua siku ya mwisho. Yeye aliipenda sheria ya Mungu na akaitafakari daima – hadi, kwa njia ya Roho Takatifu, akafikia kulielewa kusudi la roho ya

sheria ya Mungu.

Yaliyosalia Juu ya Habari Hii

Roho ya sheria ni nini? Mafarisayo walikuwa washika sheria wakali. Lakini Kristo aliwaita wanafiki kwa sababu hawakushika kipengele muhimu cha sheria. Kristo alisema: “23 Ole wenu walimu wa sheria na Mafarisayo, ninyi wanafiki! Kwa maana mnatoa zaka ya mnanaa, bizari na jira, lakini mmeacha mambo makuu zaidi ya sheria, yaani, haki, huruma na uaminifu . . .” (Mat. 23:23).

Umejione maswala yaliyomuhimu zaidi katika sheria, ambayo “ndiyo kiini”, ni pamoja na maamuzi sahihi (ambayo siku hizi tunayaita haki), huruma/rehema, pamoja na imani? Haya ni maswala ya kiroho, na hii ndiyo maana “sheria ni ya kiroho” (Warumi. 7:14).

“Sheria ina mamlaka tu juu ya mtu wakati akiwa hai?” (Warmi. 7:1), Lakini sisi kama Wakristo wa kweli “Tunapaswa tutumike katika njia mpya ya Roho, wala si katika njia ya zamani ya sheria ya andiko” (Aya ya 6).

Waweza usiibe, lakini unayo husuda, unao wivu, u mkaidi ama mpenda kulipa kisasi!

Moja wapo ya matatizo makubwa tuliyonayo katika Kanisa la Mungu siku hizi ni uvunjaji wa sheria ya imani. Lakini Mungu kaeleza kwamba pasipo imani haiwezekani kumpendeza Yeye (Ebr. 11:6).

Je, sasa tunaweza kuanza kuelewa ni kwa nini Daudi alisema, “165Wanaopenda sheria yako wana amani tele, wala hakuna kitu kinachoweza kuwakwaza” (Zab. 119:165)? Au ni kwa nini Isaya alisema, “17Matunda ya haki yatakuwa amani, matokeo ya haki yatakuwa utulivu na matumaini milele” (Isa. 32:17)?

Wote Daudi na Isaya walilielewa kusudi la kiroho la sheria. Walikuwa na nafsi kama ya Kristo! Je, sisi tuko hivyo?

Sifa kuu ya nafsi ya Mungu ni rehema. Ilimsababisha Kristo awe tayari kufa kwa ajili ya na katika mikono ya wale waliokuwa wanapaswa wafe. Ndani ya muda wake huo wa kutisha kupita wakati wowote mwingine, akiwa kaachwa, kapigwa kupita kutambulikana, yeye alisema: “Baba, wasamehe . . .” (Luka 23:34).

Yesu yuleyule alikuwa akinukuru kutoka Hosea 6:6 – nabii wa Agano la Kale – pale aliposema: “Nendeni mkajifunze maana yake maneno haya, Kwa maana nataka rehema, wala si dhabihu” – kwa nini? – “Kwa maana sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi” (Mat. 9:13).

Je, sasa umejifunza inamaanisha nini juu ya kuwa na rehema?

(Maoni ya Mwandishi: Sawa na makala hii hapo juu inavyoonyesha, Yesu aliorodhesha rehema kama mojawapo ya “mambo makuu ya sheria” matatu ikiwa ni pamoja na maamuzi ya haki na imani. Rehema yenyewe ni ya muhimu mno kiasi kwamba kulingana na Yakobo 2:13: “Huruma huishinda

hukumu”. Hivyo rehema, katika maana hiyo, hata ni “kuu zaidi” kuliko hukumu. Rehema (huruma) ni ya muhimu sana kwa Mungu na hivyo yapasa iwe ni ya muhimu sana pia kwa Wakristo).

*Fulfilling
Matthew 24:14
and
Matthew 28:19-20*



Continuing Church of God www.ccog.org
Daily Bible News Prophecy www.cogwriter.com

CCOG.ASIA This is a website targeted towards Asia. It has articles in Mandarin Chinese as well as some in English, plus other Asian languages.

CCOG.IN This is a website targeted towards those of Indian heritage.

CCOG.EU This is a website targeted toward Europe. It has materials in many European languages.

CDLIDD.ES La Continuación de la Iglesia de Dios. This is the Spanish language website for the Continuing Church of God.

PNIND.PH Patuloy na Iglesia ng Diyos. This is a website targeted towards those in the Philippines or those of related heritage.



BibleNewsProphecy channel
www.youtube.com/BibleNewsProphecy

ContinuingCOG channel
www.youtube.com/continuingcog

The leading pastor in Continuing Church of God is a regular radio guest using radio to reach audiences in many areas.

The Continuing Church of God also uses printed and electronic magazines, books, and weekly letters to the Brethren to also support Matthew 24:14 and Matthew 28:19-20

